Rasilimali za Msingi

# Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa




## Kujenga Welewa wa Mahali
## Utafiti wa Kihistoria
## Kuangalia Sanaa

Rasilimali za Msingi

# Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa

Nyenzo za TESSA zimeundwa na kuendelezwa na wataalamu wanaofanya kazi nchi mbalimbali za Kiafrika. Zimetolewa kwa kupitia leseni bunifu ya pamoja na zinaweza kutumika na kurekebishwa kwa mahitaji yako ipasavyo, kuendana na hali halisi kama inavyohitajika.

## Yaliyomo


Namba ya moduli 1 **Kujenga Welewa wa Mahali**

- Sehemu ya 1 Uchoraji wa ramani kwa mazingira ya mahali hapo
- Sehemu ya 2 Makazi na rasilimali
- Sehemu ya 3 Kuchunguza hali ya hewa
- Sehemu ya 4 Utafiti wa mabadiliko wa Mazingira
- Sehemu ya 5: Kuwapeleleza watu wengine na maeneo

Namba ya moduli 2 **Utafiti wa Kihistoria**

- Sehemu ya 1 Utafiti wa historia ya familia
- Sehemu ya 2 Kutafiti namna tulivyoishi zamani
- Sehemu ya 3 Kutumia njia tofauti za ushahidi katika historia
- Sehemu ya 4 Ufahamu wa Chati ya kalenda ya matukio
- Sehemu ya 5 Kutumia kazi za sanaa kujifunza mambo ya kale

Namba ya moduli 3 **Kuangalia Sanaa**

- Sehemu ya 1 Kuchunguza Kazi za Sanaa zionekanazo
- Sehemu ya 2 Kuandaa Shughuli za Sanaa kwa Vitendo-
- Sehemu ya 3 Kutumia ngoma kujifunza
- Sehemu ya 4 Kutumia muziki darasani
- Sehemu ya 5 Sanaa ya kuhadithia hadithi

Rasilimali za Msingi

# Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa

## **Namba ya moduli 1** Kujenga Welewa wa Mahali

**Sehemu ya 1** Uchoraji wa ramani kwa mazingira ya mahali hapo

**Sehemu ya 2** Makazi na rasilimali

**Sehemu ya 3** Kuchunguza hali ya hewa

**Sehemu ya 4** Utafiti wa mabadiliko wa Mazingira

**Sehemu ya 5**: Kuwapeleleza watu wengine na maeneo

**KISWAHILI**

*TESSA (Teacher Education in Sub-Saharan Africa) inalenga kuboresha utekelezaji darasani wa walimu wa msingi na walimu wa sayansi wa sekondari barani Afrika kupitia matoleo ya Rasilimali Huria za Elimu (OERs) ili kuunga mkono walimu kuunda njia zinazowalenga wanafunzi na kuwashirikisha. OER ya TESSA huwapa walimu kitabu cha kurejea pamoja na vitabu vya shule. Zinatoa shughuli kwa walimu kujaribu madarasani pamoja na wanafunzi wao, pamoja na masomo ya utafiti inayoonyesha jinsi walimu wengine wamefunza mada hiyo, na rasilimali husishi za kuwaunga mkono walimu katika kukuza mipango ya masomo yao na ufahamu wa somo.*

OER ya TESSA imeandikwa kwa ushirikiano wa waandishi wafrika pamoja na wa kimataifa *ili kushughulikia mtalaa na muktadha. Zinapatikana kwa matumizi ya mtandaoni na chapa (*http://www.tessafrica.net*). OER Msingi zinapatikana katika matoleona lugha kadhaa (Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu na Kiswahili). Mara ya kwanza, OER ilitolewa kwa Kiingereza na kupatikana Afrika nzima. OER hizi zimebadilishwa na washirika wa TESSA ili kufaa Ghana, Nijeria, Zambia, Rwanda, Uganda, Kenya, Tanzania na Afrika Kusini, na kutafsiriwa na washirika nchini Sudani (Kiarabu), togo (Kifaransa) na Tanzania (Kiswahili) OER ya Sayansi ya Sekondari zinapatikana kwa Kiingereza na zimebadilishwa ili kufaa Zambia, Kenya, Uganda na Tanzania. Tunakaribisha maoni kutoka kwa wale wanaosoma na kutumia rasilimali hizi. Leseni ya uundaji wa ubunifu huwawezesha watumiaji kuchukua na kujanibisha OER zaidi ili kutimiza mahitaji na muktadha wa kindani.*

*TESSA inaongozwa na Open University, Uingereza, na inafadhiliwa kwa sasa na ruzuku za ufadhili kutoka kwa Wakfu wa Allan and Nesta Ferguson, Wakfu wa William and Flora Hewlett na Open University Alumni. Orodha kamili ya wafadhili inapatikana kwenye tovuti ya TESSA (*http://www.tessafrica.net*).*

*Pamoja na rasilimali kuu za mafundisho za kuunga mkono mafunzo katika masomo maalum, ni chaguo za rasilimali za ziada ikiwa ni pamoja na sauti, rasilimali kuu ambazo zinafafanua utendakazi, vitabu na zana maalum.*

**TESSA Programme**
**The Open University**
**Walton Hall**
**Milton Keynes, MK7 6AA**
**United Kingdom**

**tessa@open.ac.uk**

Copyright © 2017 The Open University
Except for third party materials and otherwise stated, this content is made available under a Creative Commons Attribution-Share Alike 4.0 licence: http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0/. Every effort has been made to contact copyright holders. We will be pleased to include any necessary acknowledgement at the first opportunity.

***TESSA_SwPA_SCI_M1 August 2017***

*This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Share Alike 4.0 License*

# Contents

Sehemu ya 1: Uchoraji wa ramani kwa mazingira ya mahali hapo 5
Somo la 1 5
Somo la 2 7
Somo la 3 9
Nyenzo-rejea ya 1: Alama za Ramani 11
Nyenzo-rejea ya 2: Ramani kifani 13
Nyenzo-rejea ya 3: Maswali yanayohusu ramani 14
Sehemu ya 2: Makazi na rasilimali 15
Somo la 1 15
Somo la 2 17
Somo la 3 18
Nyenzo-rejea ya 1: Rasilimali asili na Makazi ya watu Tanzania 20
Nyenzo-rejea 2: Namna ya kudahalisha maada 20
Nyenzo-rejea 3: Kilimo cha kufyeka na kuchoma 21
Nyenzo-rejea 4: Mazingira tofauti 24
Sehemu ya 3: Kuchunguza hali ya hewa 25
Somo la 1 25
Somo la 2 27
Somo la 3 28
Nyenzo-rejea ya 1: Jdi ya Afrika kuhusiana na hali ya hewa, nyenzo rejea ya mwalimu 30
Nyenzo-rejea 2: Jedwali la unchunguzi wa hali ya hewa 32
Nyenzo rejea 3: Kupima mwelekeo na kasi ya upepo 32
Nyenzo rejea 4: Jedwali la uchunguzi 34
Nyenzo rejea 5: Ni jinsi gani hali ya hewa ilimwathiri Bwana Hoja na familia yake 35
Sehemu ya 4: Utafiti wa mabadiliko wa Mazingira 36
Somo la 1 36
Somo la 2 38
Somo la 3 39
Nyenzo-rejea ya 1: Kijitabu cha mimea 40
Nyenzo-rejea 2: Masuala ya maji 41
Nyenzo-rejea 3: Jaribio la mbegu za mahindi 42
Nyenzo-rejea 4: Mzunguko wa maji 44
Nyenzo-rejea: 5: Makala inayohusu kuongezeka kwa joto 44
Nyenzo 6: Barafu ya mlima Kilimanjaro 47

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Sehemu ya 5: Kuwapeleleza watu wengine na maeneo 49
Somo la 1 49
Somo la 2 50
Somo la 3 52
Nyenzo-rejea ya 1: Kuishi kwenye jamii tofauti 53
Nyenzo-rejea 2: Ulinganifu wa Magubike na Gairo 53
Nyenzo-rejea 3: Elimu kwa maendeleo Endelevu (EME) 54

# Sehemu ya 1: Uchoraji wa ramani kwa mazingira ya mahali hapo

**Swali Lengwa muhimu:** Kwa jinsi gani unaweza kutumia mazingira ya mahali hapo ili kujenga welewa wa wanafunzi kuhusu ramani na mahali?

**Maneno muhimu:** mazingira ya mahali hapo; ramani; kazi ya vikundi; alama;

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- umetumia nyenzo rejea za mahali hapo katika kukuza ujuzi wako kwenye ufundishaji kuhusu sura za mandhari zilizoko katika mazingira ya nyumbani na ya shuleni;
- umetumia michezo ili kupanua welewa wa wanafunzi wako kuhusu ramani;
- umetumia kazi ya kikundi kama mkakati wa kufundishia na kujifunzia katika kuyamudu madarasa makubwa na madogo.

## Utangulizi

Wanafunzi wengi wana kiasi cha welewa wa eneo wanakoishi. Wanafahamu njia za kufika kwa haraka zaidi majumbani kwa marafiki zao au kwenye soko la mahali hapo. Unapojenga welewa wao wa mahali na, hususan, ujuzi wao wa kuchora ramani, kwa kawaida ni muhimu kuanza na kitu wanafunzi wanachokifahamu kabla ya kwenda kwenye kitu wasichokifahamu. Hii itawapa wanafunzi hali ya kujiamini, kwa sababu unatumia kitu ambacho tayari wanakifahamu.

Kutumia msingi wa kitu wanachokifahamu wanafunzi kuhusiana na sura za mandhari ya mazingira ya nyumbani na shuleni kwao, kutakurahisishia kuendelea na uchoraji wa ramani za mazingira ya mahali hapo ulio rasmi zaidi. Kufanya hivi kutakupatia mfululizo unaoeleweka wa kutalii alama zitumikazo katika uchoraji wa ramani. Shughuli zilizopo katika sehemu hii zitakusaidia kutia msukumo katika ujuzi wa wanafunzi wako kwenye uchunguzi na itawasaidia kuhawilisha maarifa kwenda kwenye alama rasmi za vielelezo. Vilevile, utajenga ujuzi wako katika kutumia kazi za vikundi kwenye darasa lako.

## Somo la 1

Wanafunzi wengi sana wanajua mengi kuhusu mazingira ya mahali pao na wanaweza kuchora welewa wao wa mahali vitu vilipo kwa namna yao wenyewe. Kwanza, ni muhimu kukuza uwezo wa wanafunzi wako katika kuchunguza mazingira ya mahali pao na kufanya shughuli hizi ziwe na manufaa kwao. Eleza kwamba kuona sura za mazingira katika maeneo yao yanayowazunguka kunawafanya watambue sehemu mbalimbali zinazomhusu kila mmoja wao na kuzielezea kwa ufasaha. Kuwa na dhana ya uelekeo kunawasaidia wanafunzi kufika sehemu mbalimbali kwa kutumia njia zao. Watakapofahamu mazingira yao wenyewe, na njia zao tofauti za kuyafikia, wanafunzi wako wanaweza kuanza kudadisi kuhusu mazingira ya ulimwengu yaliyo mapana zaidi.

Njia mojawapo ya kuchunguza mazingira ya mahali hapo ni kuwahimiza wanafunzi wako kutembea na daftari na kuchora au kuandika vitu vyovyote vinavyovutia wanavyoviona wanapotembea kuzunguka eneo la mahali hapo. Njia nyingine ni kufanya kazi na wanafunzi wako na kutengeneza picha ya darasa ya kuchora au ya kubandika kwenye ukuta wa darasa. Kila siku, wanafunzi wachache wanaweza kuongeza picha (na maneno kutoka kwa wanafunzi wakubwa) za vitu vilivyoko kwenye mazingira ya mahali hapo.

Katika **Uchunguzi Kifani 1**, mwalimu mmoja anaonesha jinsi alivyolisimamia darasa kubwa. Soma Uchunguzi Kifani huu kabla hujajaribu **Shughuli ya 1**.

## Uchunguzi kifani ya 1: Ramani ya shule na mazingira yake

Bibi Kazimoto, mwalimu wa Shule ya Msingi Dabanga nchini Tanzania, anataka kukuza ujuzi wa wanafunzi wake wa Darasa la 3 katika kuchunguza na kubainisha sura muhimu za nchi katika eneo la mahali hapo. Baadaye ataendelea na uchoraji wa ramani.

Bibi Kazimoto ana darasa kubwa; kwa hiyo anawagawa katika makundi manane yenye wanafunzi kumi kwa kila kundi. Anafahamu kwamba utumiaji wa kazi za makundi utamsaidia kulimudu darasa na kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanashiriki. Vilevile, itawasaidia wanafunzi kukuza ujuzi wao wa ujifunzaji shirikishi. (Angalia **Nyenzo rejea ya Muhimu: Utumiaji wa kazi za makundi katika darasa lako** .)

Analiambia kila kundi kuoredhesha vitu vyote vilivyoko katika ardhi ya shule ambavyo huviona wakati wanapokuja shuleni, kama vile miti, majengo, n.k. Anamwambia mtu mmoja toka kila kundi kuandika taarifa zote muhimu. Baada ya dakika chache, analiambia darasa limalize shughuli hiyo na analitaka kila kundi lisome kwa sauti kitu kimoja toka kwenye orodha yao, ambacho anakiandika ubaoni. Anazungukia kila kundi namna hiyo mpaka makundi yote yanamaliza kusoma vitu vyote.

Kisha, Bibi Kazimoto analipatia kila kundi karatasi kubwa na kuwaambia wanakundi waweke umbo-mraba katika ya karatasi kuonesha shule. Halafu kila mwanafunzi anaambiwa aweke kitu kwenye karatasi katika mahali sahihi..

Baada ya kila kundi kumaliza kazi hiyo, Bibi Kazimoto anawatoa nje kwenda kuona kama walichoweka kwenye karatasi ni mahali sahihi na kama kuna kitu cha kukihamisha au kukiongeza. Michoro yao imeboreshwa na kisha inaoneshwa darasani.

Bibi Kazimoto anaona kwamba makundi mawili yamefanya vizuri sana. Makundi mengine yanatakiwa kubadili vitu vichache na anapanga kuwapeleka wanafunzi hawa nje kimakundi kuchora ramani rahisi zaidi ya ardhi ya shule na vitu vinavyoonekana.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Shughuli ya 1: Safari ya kuelekea shuleni –alama na ishara

Waambie wanafunzi wachunguze na kurekodi katika kijitabu chao au daftari lao vitu muhimu 6–10 wanavyoviona njiani wakielekea shuleni siku itakayofuata. Wanafunzi wa umri mdogo wanaweza kufanya kazi ya kuchora.

Darasani, mwambie kila mwanafunzi kupangilia alivyoviona kwa kufuata utaratibu wa cha kwanza kukiona mpaka cha mwisho kukiona.

Waeleze wanafunzi sura ya mandhari ni nini.

Waambie wanafunzi waweke tiki kwenye sura za mandhari katika orodha yao.

Waulize kwa nini baadhi ya vitu walivyovichunguza si sura za mandhari. Je, wanatarajia kuviona vitu hivi kwenye ramani? Jadili kwa nini iko hivi, kwa mfano, vitu vingine kama mbwa na paka vinatembea, kama yanavyotembea magari, kwa hiyo vitu hivi si sura za mandhari (za kudumu).

Waulize wanafunzi wanafuata uelekeo gani wanapokuja shuleni, yaani, Kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi (Ksz, Ks, Ms na Mg). Unaweza kutakiwa kueleza kuhusu uelekeo na kuwa tayari na ramani kwa ajili ya kuwaonesha au kuwakumbusha kuhusu Ksz, Ks, Ms na Mg.

Kutokana na msingi wa uelekeo, unda makundi manne, kila moja liwe na wanafunzi wanaotoka takriban katika mwelekeo mmoja.Based on the directions, (Angalia **Nyenzo rejea Muhimu: Utumiaji wa kazi za makundi katika darasa lako**.) Ikiwa wanafunzi wako wote walikuja shuleni kutoka katika mwelekeo mmoja au miwili, tunashauri uwachukue wanafunzi wako katika matembezi ili kutalii mielekeo mingine.

Waambie kila kundi kutengeneza orodha ya pamoja ya sura za mandhari zilizopo kwenye njia yao kuelekea nyumbani. Je, wanaweza kuziweka katika utaratibu wa mfuatano ambapo wanaweza kuziona wakiwa njiani toka shuleni kwenda nyumbani?

Onesha orodha zote kwenye kuta za darasa, kulingana na uelekeo.

Unaweza kufanya shughuli gani nyingine za kukuza ujuzi wa uchunguzi kwa wanafunzi wako?

# Somo la 2

Kuchunguza sura za mazingira ni hatua ya kwanza katika utengenezaji wa ramani. Ili kuwasaidia wanafunzi wako waelewe ramani, unahitaji kuwabainishia dhana ya alama.

**Uchunguzi kifani 2** unaonesha jinsi mwalimu mmoja anavyotumia mchezo ili kuwasaidia wanafunzi kujifunza kuhusu alama. Kwa kupangilia na kubuni mchezo unaohusu mada inayopendwa na wanafunzi, mwalimu huyu amefanya kuwe na uwezekano mkubwa zaidi wa wanafunzi kuja kushiriki katika zoezi hili, na kwa hiyo, kujifunza zaidi. Utumiaji wa mchezo utawahusisha wanafunzi wako katka ujifunzaji hai; itakuwa burudani kwao na itawasaidia kukumbuka mengi zaidi. Soma **Uchunguzi Kifani 2** bkabla ya kupanga na kujaribu **Shughuli 2**.

## Uchunguzi kifani ya 2: Alama ya kusaka kitu cha thamani

Bi. Jane Ndekule, mwalimu wa wanafunzi wa Darasa la 5 katika Mkoa wa Ruvuma, alitaka kujenga welewa wa wanafunzi kuhusu uelekeo na mazingira ya mahali hapo kwa kubainisha dhana ya utumiaji wa alama kuwakilisha sura za mandhari. Aliamua kufanya mchezo wa kusaka kitu cha thamani.

Kabla ya somo, alichunguza sura sita za mandhari ya shule, akijumuisha mageti, mti mkubwa na ofisi ya Mwalimu Mkuu. Alitafuta vipande sita vya karatasi ngumu na kuchora alama moja kwenye kila karatasi kuwakilisha sura moja ya kitu (mfano, meza ya ofisini kwa mwalimu mkuu). Halafu aliweka namba kwenye karatasi na kuongeza mielekeo kuelekea kwenye alama inayofuata katika kila karatasi. Aliweka vipande hivyo vya karatasi katika sehemu zake mahsusi.

Darasani, wanafunzi waligawanywa katika 'vyama vya kusaka' na kupewa vidokezo vyao vya awali. Walitakiwa kwenda nje ya darasa, na kugeukia upande wa mashariki –mwalimu aliwasaidia kwa kuwaambia maelekezo haya ili waanze. Walipokuta karatasi katika sura ya kitu, hii iliwaongoza kuendelea kwenye mwelekeo mwingine, na kutafuta alama nyingine, na kadhalika.

Wanafunzi waliona mchezo huu unasisimua sana. Walishirikishwa kikamilifu katika kutafakari maana za alama na kuelekea kwenye upande sahihi. Bi. Ndekule aliyafuatilia makundi na alikuwa tayari kusaidia kundi lolote lililokuwa likihangaika kutambua maana za alama au kutafuta upande upi wa kufuata.

Kila mmoja aliifikia karatasi ya mwisho. Bi. Ndekule alifurahi kwa sababu alijua wamemudu kutafsiri alama zote na wameelewa vema uelekeo.

## Shughuli ya 2: Utumiaji wa alama

Anza somo lako kwa maelezo mafupi kuhusu matumizi na umuhimu wa alama za ramani. Waambie wanafunzi wakupe mifano ya alama maarufu ambazo wanazifahamu zinazotumika miongoni mwao (mfano barabara) na tumia majibu yao kuunda orodha ya alama mahsusi. (Angalia **Nyenzo rejea 1: Alama za ramani** kwa mifano zaidi.) Unaweza kuunda orodha kwa muda wa hadi wiki moja na kisha kufanya maonesho kwa darasa zima.

Waulize wanafunzi watafakari kuhusu kwa nini alama zitumike kuliko maneno. Uulizaji wa aina hii utawasaidia kufikiri kuhusu thamani na umuhimu wa alama. (Angalia **Nyenzo rejea Muhimu: Kutumia uulizaji katika kukuza tafakuri** .)

Sasa mwambie kila mwanafunzi afikirie sura tatu za mandhari anazoziona anapokuwa njiani kwenda shuleni (angalia **Shughuli 1**) na kisha achore alama kwa kila moja. Baada ya dakika chache, waambie wanafunzi wabadilishane alama zao na majirani. Je, majirani wanaweza kukisia alama zina maana gani?

Waambie baadhi ya wanafunzi kuja na kuchora alama zao ubaoni. Je, wanafunzi wengine wanaweza kutambua zinamaanisha nini?

Maliza somo kwa kuona kama wanafunzi wanaweza kuamua kuhusu kitu gani kinafanya alama iwe nzuri.

Orodhesha sababu zao ubaoni.

# Somo la 3

Ukuzaji wa maarifa na welewa wa alama maarufu ambazo hutumika kwenye ramani ulimwenguni kote utawasaidia wanafunzi wako kutalii sura za mandhari ya sehemu yoyote duniani. Vilevile, ukuzaji huo utawasaidia kuelewa jinsi ramani zinavyochorwa na thamani yake katika maisha ya kila siku, hususan kwa kadri wanavyokua na kusafiri katika maeneo mapya.

Hata hivyo, ni muhimu kutumia mbinu za kufanyia kazi ambazo zitawashirikisha wanafunzi kikamilifu katika kuyatalii maeneo yanayowazunguka na kutafakari kwa kina kuhusu tatizo wanalojaribu kulitatua. Utumiaji wa nyenzo na wataalamu wa mahali hapo unawasaidia wanafunzi kuelewa zaidi kwani mazingira wanamojifunza yanafahamika kwao. Inawezekana ukamtafuta mtu anayefahamu masuala ya ramani za mahali hapo kuja na kuzungumza na wanafunzi kuhusu jinsi ramani za mahali pao zilivyochorwa na kufafanua maana za alama ambazo zinaonesha sura za mandhari ya mahali hapo.

**Uchunguzi Kifani 3** unaonesha namna mbalimbali ambazo mwalimu mmoja alifanya kazi na wanafunzi wake ya kuelewa ramani za mahali hapo. Soma sehemu hii kabla ya kuanza **Shughuli ya Msingi** .

## Uchunguzi kifani ya 3: Uchanganuzi wa ramani ya eneo la mjini la mahali hapo

Bwana Juma ni mwalimu wa shule ya msingi ya mjini katika Mkoa wa Tanga, Mashariki mwa Tanzania. Alitaka wanafunzi wake waweze kusoma ramani na kutambua sura za mandhari za sehemu yoyote.

Bwana Juma aliamua kutumia ramani halisi ya jiji, na kwa hiyo, wiki mbili kabla ya kupanga kufanya kazi hiyo alitembelea halmashauri ya mipango ya jiji ili kupata ramani mbalimbali za mahali hapo. Kwa kufuatisha toka kwenye ramani hizo, alichora kwenye karatasi ya kufanyia kazi kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi wake. Kwa vile kazi hii ingehitaji alama, alichora pia chati ya alama ambayo alipanga kwenda kuionesha darasani.

Kwa kuwa halmashauri ya mipango ya jiji waliweza kumpa picha au ramani tano tu za mandhari ya nchi, aligawa darasa lake katika makundi matano. Bwana Juma aliwaonesha wanafunzi wake chati ambayo inabainisha alama na alitoa ramani na moja kati ya karatasi zake za kufanyia kazi kwa kila kundi. Alionesha barabara kadhaa, bustani, hospitali, baadhi ya hoteli na kituo cha mafuta, vyote hivi, makundi yalitakiwa kuvitafuta kwenye ramani.

Halafu, aliwaambia wanafunzi wakadirie kipimo. Alifafanua kwamba vipimo vya ramani hulinganisha ukubwa wa ramani na ukubwa halisi wa eneo. Bwana Juma aliwaonesha wanafunzi wake jinsi ya kusoma taarifa zilizooneshwa kwenye maelezo ya vipimo na kielelezo cha vipimo.

Wanafunzi walipomaliza kuchanganua ramani na kukamilisha kujaza karatasi za kufanyia kazi, walibadilishana karatasi hizo na makundi mengine, na kuangalia kama wamepata majibu yaleyale. Mahali ambako hakukuwa na kufanana, Bwana Juma aliwaambia wanakikundi washauriane na kukubaliana kuhusu jibu.

Mwishoni mwa somo, alipitia alama zote pamoja na darasa zima. Mahali ambako wanafunzi walipata majibu tofauti, walijadili sababu za majibu hayo na kukubaliana kuhusu jibu la mwisho.

**Nyenzo rejea 2: Ramani Kifani** na **Nyenzo rejea 3: Maswali kuhusu ramani** toa mifano ya aina za nyenzo rejea ambazo zinaweza kutumika.

## Shughuli muhimu: Kutengeneza picha kubwa ya mahali hapo

Liambie darasa kwamba utachora ramani kubwa pamoja nao, na njia tofauti tofauti wanazopita wakati wa kuja shuleni na sura za mandhari yanayozunguka shule.

Gawa darasa lako katika makundi manne, kulingana na uelekeo wanaofuata kutoka majumbani hadi shuleni (Ksz, Ksn, Ms na Mgh)

Liambie kila kundi liorodheshe sura za mandhari ambayo huyaona wanapokuja shuleni (Angalia **Shughuli 1**).

Weka alama kwenye nafasi nne ardhini –au katika kipande kikubwa cha karatasi au kipande cha nguo kisicho na alama yoyote –Ksz, Ksn, Ms na Mgh.

Waambie wanafunzi wajitolee kuwa wa kwanza kuchora sura hizo zilizoko kwenye upande wao katika nafasi walizopewa.

Kisha kila kundi liongezee kwenye kile kilichochorwa na wanafunzi wenzao waliojitolea.

Mara picha kubwa itakapokamilika, jadiliana na wanafunzi jinsi sasa mbele yao walivyo na ramani kubwa ya eneo zima linaloizunguka shule.

Waambie wanafunzi kutoka katika makundi tofauti kuangalia ramani kutoka upande mwingine na kuona kama wanaweza kubainisha alama zilizomo zinamaanisha nini.

Ukiwa na wanafunzi wadogo, unaweza kwanza kujadili alama zitakazotumika na kuzichora ubaoni. Halafu waambie watumie alama hizo kwenye ramani zao.

Mwisho, waambie wanafunzi wachore ramani zao ndogo za shule na mazingira yake, kwa kutumia ramani kubwa kama mfano wa kuwaongoza.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

# Nyenzo-rejea ya 1: Alama za Ramani

**Taarifa za msingi/ welewa wa somo wa mwalimu**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Barabara:Barabara Ndefu na Pana zaidi ya Taifa | | Kioleza cha trigonometria (namba ya kioleza inaonesha kimo) | △124 |
| Barabara: Barabara ya taifa | | Maeneo ya mjini yaliyojengeka | |
| Barabara: Barabara kuu kwenda nje na kuingia ndani ya mji | | Majengo (makuu au yaliyojitenga) | |
| Barabara: Barabara kuu za ndani ya mji | | Daraja | |
| Barabara: Barabara ndogo | | Ardhi iliyolimwa | |
| Reli (inaonesha kituo) | | Safu za miti (mahali ambapo ni pa muhimu) | |
| Mto: Wa kudumu (una maji mwaka | | Kisima cha | |

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net


| | | | |
|---|---|---|---|
| mzima) | | upepo | |
| Mto: Usio wa kudumu | | Mnara wa mawasiliano | |
| Bwawa | | Eneo lililomomonyoka | |
| Mtitio wa ardhi: Wa kudumu | | Mpaka: Wa Kimataifa | |
| Mtitio wa Ardhi: Usio wa kudumu | | Mpaka: Kimkoa | |
| Mtitio wa ardhi: Mkavu | | Mpaka: Shamba la Kadastri (shamba la awali) | |
| Mfereji | Canal | Mpaka: Hifadhi ya Wanyama | |
| Mkondo wa umeme (mikondo mikuu tu) | | Mpaka: Msitu wa taifa | |
| Alama ya kimo (mwinuko katika ncha) | ·152 | Kontua | |
| Makanisa | | Mti: Wa kupukutisha majani | |
| Mti: Mchikichi | | Mti: Wa kijani wakati wote | |

*Chanzo asilia: [OneWorld–Nations],Website*

# Nyenzo-rejea ya 2: Ramani kifani

**Nyenzo rejea ya mwalimu kwa ajili ya kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

Ramani hii inaonesha mji wa Tanga.




*Scale = kipimo

To Bus Station = kwenda kituo cha mabasi

Uchoraji wa ramani kwa mazingira ya mahali hapo: Nyenzo-rejea ukurasa 4

To Korogwe, Moshi, Dar es Salaam & Airport = Kwenda Korogwe, Moshi, Dar es Salaam na Uwanja wa

Ndege

Railway Station = Kituo cha treni/reli Uhuru park = Bustani ya Uhuru Sation Road = Barabara ya Stesheni Stadium = Uwanja wa Michezo

Bank = Benki

Four Ways Hotel = Hoteli ya Four Ways Patwas Restaurant = Mgahawa wa Patwas Market = Soko

Planters Hotel = Hoteli ya Planters Bandarini Hotel = Hoteli ya Bandarini Marina Inn = Hoteli ya Marina

Market Street = Mtaa wa Market

Independence Avenue = Mtaa wa Uhuru

Clock Tower = Mnara wa Saa

Post Office = Posta

Tanga Library = Maktaba ya Tanga

Chinese Restaurant = Mgahawa wa Kichina

St. Anthony's Cathedral = Kanisa Kuu la Mtakatifu Anthoni

Government Offices = Ofisi za Serikali

National Bank of Commerce = Benki ya Taifa ya Biashara

To Beaches, Cement Factory & Tanga Bathing Club = Kwenda Fukweni, Kiwanda cha Saruji na Klabu ya Kuogelea

Chanzo asilia: [Crowther G na Finlay H], [Afrika ya Mashariki – a travel survival kit Toleo la 3. Mfuatano: Lonely Planet travel survival kit],[Lonely Planet Publications]

## Nyenzo-rejea ya 3: Maswali yanayohusu ramani

**Nyenzo rejea ya mwalimu kwa ajili ya kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

Katika kundi lako, tazama ramani na kisha jibu maswali yafuatayo:

1. Hoteli ya Planters ipo katika mtaa gani?

2. Kanisa Kuu lililooneshwa katika ramani hii linaitwaje?

3. Benki ngapi zinaweza kuonekana katika ramani hii?

4. Hoteli nyingi sana ziko katika mtaa gani?

5. Ungepita mtaa gani kama ungetaka kwenda kituo cha mabasi?

6. Ofisi za serikali ziko upande gani wa Mnara wa Saa?

7. Ungetembelea mtaa upi kama ungekuwa na njaa? Kwa nini?

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

# Sehemu ya 2: Makazi na rasilimali

**Swali Lengwa muhimu:** Shughuli gani unaweza kutumia kutafiti sababu za watu kuishi katika sehemu fulani?

**Maneno muhimu:** nyenzo;uchunguzi kifani;kazi za kundi;makazi;mdahalo;maswali

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- umetumia kazi ya kikundi na mdahalo kusaidia wanafunzi kuelewa rasilimali zinazohitajika katika maisha;
- umetumia picha na ramani kutafiti uhusiano baina ya rasilimali zilizopo na makazi ya watu.

## Utangulizi

Kila siku ya maisha yetu tunatumia rasilimali za aina zote na kadili idadi ya watu duniani inavyongezeka na uhitaji wa rasilimali unaongezeka.

Kama mwalimu unayetafiti mawazo haya, ni muhimu kuanza kwa kutafiti nini tayari wanafunzi wanakifahamu kuhusu rasilimali katika mazingira yao. Sasa itawezekana kupanga namna ya kupanua ufahamu wao na kuwahusisha katika kufikiri kiundani kuhusu mada. Chunguzi kifani katika sehemu hii inaonesha baadhi ya walimu walielezea mawazo haya na itakusaidia kufikiria kuhusu utakachofanya katika shughuli hii.

## Somo la 1

Wakiwa njiani kuelekea shuleni, wanafunzi wako wataona rasilimali nyingi za asili zinazotumika katika maisha ya kila siku. Katika sehemu hii utawauliza wanafunzi ku pendekeza baadhi ya rasilimali hizi na namna watu wanavyozitumia. Kwa kuzipanga kutegemeana na umuhimu wake kwa watu wanaoishi mazingira fulani, wataona jinsi rasilimali hizi zilivyo muhimu. Hii itawasaidia wanafunzi wako kukuza ujuzi wa kuchunguza na kufikiria kuhusu matumizi yake; pia katika kutumia rasilimali kwa busara. Utahitaji kutafiti ufahamu wao wa utofauti baina ya rasilimali asili na rasilimali zilizotengenezwa na watu.

Utatafuta pia njia za makundi katika kuliongoza darasa. Kufanya kazi kwa namna hii kutawasaidia kushirikishana mawazo na kujifunza pamoja.

Soma uchunguzi kifani1 kabla ya kujaribu shughuli 1: hizi zinaonesha njia mbalimbali za kutafiti wanachojua wanafunzi. Unaweza kujaribu njia zote kwa nyakati tofauti ukiwa darasani.

## Uchunguzi kifani ya 1: Uchunguzi wa rasilimali tunazohitaji kwa maisha na maendeleo

Nchini Tanzania, wanafunzi wengi wanatoka vijijini. Bwana, Kaizilege ni mwalimu katika shule ya msingi Kitahya, iliyo karibu na kijiji cha Ileme, Tanzania.

Kijiji kipo katika mazingira ambayo yana rasilimali asili kama miti, maji, na mashamba yanayolimwa. Bwana Kaizilege anategemea kuendeleza uwezo wa wanafunzi katika kuchunguza na kutambua rasilimali halisi katika mazingira yanayozunguka kijiji chao. Anategemea hili litawasaidia kuelewa kazi na wajibu wao katika matumizi kulingana na rasilimali hizi za asili.

Mwishoni mwa siku aliwataka wanafunzi kuorodhesha rasilimali zote walizoziona kijijini wakirudi nyumbani na kuleta orodha shuleni. Siku inayofuata aligawanya wanafunzi katika makundi ya watu nane na kuandika swali lifuatayo ubaoni

Ni rasilimali gani tunazo katika mazingira yetu?

Mwanafunzi kutoka kila kundi hunukuu swali katika kipande cha karatasi na kila kundi hushirikisha utafiti kutoka siku iliyopita ya zoezi la utafiti, kuchora au kuandika matokeo kuhusu swali. Bwana Kaizilege huonyesha matokeo ubaoni na kwa pamoja huakisi namna mawazo yao yanavyofanana. Bwana Kaizilege hujaza nafasi zilizopo kwenye jedwali. Kwa mfano, hakuna aliyetaja jua au machimbo ya kokoto.

Bwana Kaizilege anaandika sentensi ubaoni. Kila sentensi inaonyesha matumizi ya rasilimali moja inayopatikana kwenye kijiji; Kisha aliwataka wanafunzi katika makundi kulinganisha kila sentensi na rasilimali. Makundi hushirikishana mawazo na kufikia makubaliano kabla ya kunakili kwenye madaftari yao.

## Shughuli ya 1: Kutambua rasilimali za mahali na kutafiti umuhimu wake kulingana na mahitaji

Andika ‘rasilimali mahali’ katikati ya ubao. Hakikisha wanafunzi wanafahamu kuhusu maana ya rasilimali. Watake wanafunzi kutumia dakika tatu kuongelea kuhusu rasilimali wanazotumia katika kijiji.

Halafu, watake jozi tofauti za wanafunzi kutoa mawazo.

Andika mawazo yao katika orodha mbili ubaoni-‘Rasilimali asili’ na ‘Rasilimali zilizotengenezwa na watu’.

Sasa gawanya darasa katika makundi madogo na waeleze kila kundi kujadili baadhi ya tofauti baina ya rasilimali asili na zile zilizotengenezwa na watu.

Watake kila kundi kutoa majibu yao kwa darasa. Jadili pamoja na darasa dondoo muhimu walizotoa.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Waamuru kila kundi kupanga orodha ya rasilimali zote zinazopatikana katika kijiji chao, kutoka zile muhimu sana kwa jamii hadi zile zenye umuhimu kidogo.

Litake kila kundi kuwasilisha na kutetea mpangilio wao kwa wanadarasa wengine.

Kama darasa, kubaliana na orodha moja. Unaweza kuamua kwa kutumia kura

Watake wanafunzi kufikiri kuhusu rasilimali zinazopatikana na rasilimali ambazo ni ngumu kuzitunza/kuhifadhi au ni za gharama.

Je wanafunzi waliona utofauti kati ya rasilimali asili na zile zilizotengenezwa na binadamu? Kuna yoyote anahitaji msaada zaidi?

## Somo la 2

Watu kwa kawaida wamekuwa wakiishi sehemu ambazo wanaweza kupata rasilimali asili kama maji, kuni na urahisi wa kupata chakula, labda ardhi kwa ajili ya kulima mazao au kufuga ng'ombe au kuvua samaki kutoka ziwani au baharini.

Kusaidia wanafunzi kuelewa kwanini watu wanachagua sehemu fulani kwa kuishi, utatumia mfano wa kihistoria kutafuta masuala ya maji. Unaweza husisha mawazo muhimu na maisha yao ya kila siku.

Kwa kutumia kazi za kikundi utaongeza mijadala ambayo itawasaidia wanafunzi kutafiti fikira zao na kupanua zaidi ufahamu wao.

## Uchunguzi kifani ya 2: Matumizi ya historia ya mwanzo ya Tanzania

Bibi Byabato alikuwa anafundisha darasa la 6 kuhusu uhusiano kati ya rasilimali asili na makazi ya watu. Aliamua kutumia mfano kutoka Tanzania ya zamani.

Aliandaa baadhi ya makala kuhusu Tanzania katika siku za zamani na aliandika historia hiyo ubaoni. (Rejea Nyenzo 1: Rasilimali asili na makazi ya watu Tanzania.) aliwaamuru wanafunzi katika jozi kutambua rasilimali kuu za asili zilizopo Tanzania na kujadili kwa nini watanzania huishi sehemu mbalimbali. Walikuwa na uwezo wa kutambua umuhimu wa maji kama rasilimali asili katika kuamua wapi waishi nchini

Halafu, aliwataka wanafunzi kutengeneza makundi ya watu nane na kila kundi kujadiliana juu ya umuhimu wa maji katika vijiji vyao. Aliwataka watambue wapi vijiji vinapata maji na namna maji yanavyoathiri maisha ya watu. Makundi yalishirikishana tafiti zao na wanafunzi wengine na Bibi Byabato aliandika mawazo yao ubaoni. Walijadiliana kuhusu umuhimu wa kila wazo.

Bibi Byabato alifurahishwa sana na majadiliano yaliyoonesha ufahamu wa wanafunzi-hii ina maana kuwa walielewa uhusiano kati ya rasilimali asili na makazi ya watu.

## Shughuli ya 2: Kuhusianisha rasilimali na makazi

Gawanya darasa katika makundi na watake kila kundi kufikiri kuhusu mahitaji na wakazi (mfano maji,chakula na malazi). Mwite mwanafunzi mmoja kutoka kila kundi kuorodhesha mawazo ya kikundi.

Litake kila kundi kufikiri ni sehemu gani ingekuwa nzuri kwa makazi mfano karibu na mto lakini mbali na maeneo yanayoweza kukumbwa na mafuriko.

Litake kila kundi kuwasilisha utafiti wake kwa wanafunzi wengine na kutambua sababu zinazolingana na makundi mengine.

Halafu, kila kundi lifikiri na kuandika shughuli ambazo zinazoweza kuwa zilifanywa na watu wengine katika makazi haya.

Sasa litake kila kundi kubuni vijiji vyao. Lipe kila kundi kipande kikubwa cha karatasi. Waambie waonyeshe:

mto nyumba

eneo lenye mwinuko;

barabara

Wahamasishe kutumia alama kwenye ramani na kujumuisha maumbo mengine kadili wanavyo taka.

Toa muda mwishoni mwa kipindi kwa makundi kuwasilisha ramani za vijiji na kueleza ambako watu katika kijiji wanapata rasilimali.

## Somo la 3

Rasilimali nyingi ni haba na hivyo zinahitaji kutunzwa vizuri. Baadhi ya rasilimali, mara zikitumika, haziwezi kubadilishwa. Nyingine ni nyingi kwa sasa lakini zinaweza kuisha kama hazikutumika vizuri.

Katika uchunguzi kifani 3, mwalimu hutumia mdahalo wa darasa kutafiti rasilimali ulani. Kama unawanafunzi wakubwa unaweza kujaribu njia hii, chagua mada yoyote inayoelekeana na jamii yako. Mafanikio ya mdahalo yatategemea muda waliopewa wanafunzi kupanga mdahalo wao vizuri na kuwaandaa wanafunzi ili wajue majukumu yao katika mdahalo huo.

Katika shughuli muhimu, utawahamasisha kutumia njia nyingine ya kutafiti rasilimali katika eneo lao.

## Uchunguzi kifani ya 3: Mdahalo juu ya matumizi ya rasilimali

Bibi Masawda aliwataka wanafunzi wa darasa la sita katika mkoa wa Usambara kutafiti faida na hasara za matumizi ya rasilimali asili. Aliamua kuitisha mdahalo darasani juu ya suala kilimo cha kufyeka na kuchoma, kinachotokea sehemu nyingi duniani.

Alianza kipindi kwa kuandika ubaoni madhara ya kilimo cha kufyeka na kuchoma kwa mazingira.

Halafu Bibi Masawda alielezea namna mdahalo unavyofanya kazi (**Rejea Nyenzo 2: Namna ya kudahalisha mada**) aliwataka wanafunzi atatu kukubali mada na wanafunzi wengine watatu kutokukubali mada. Alielezea kwa makundi yote kuwa wanatakiwa kutoa ushahidi kujenga hoja zao. Kuwasaidia kupata ushahidi alihamasisha kila kundi kuongea na wazee katika jamii juu ya kwa nini wakulima wanatumia njia ya kufyeka na kuchoma katika kuandaa mashamba. Pia aliwapa baadhi ya taarifa alizozipata kwenye mtandao zinazozungumzia kufyeka na kuchoma na baadhi ya matokeo yake kwenye mazingira.(**Rejea Nyenzo 3: Kilimo cha kufyeka na kuchoma**)

Aliwapa muda wa majuma mawili kujiandaa kwa mdahalo ikijumuisha muda wa kipindi kwa wanafunzi wote kufikiri juu ya faida na hasara za kuchoma misitu. Wanafunzi wengine walijaribu kutafiti kile walichoweza kutoka kwa jamii yao na kushirikishana na pande zote mbili za mdahalo. Siku ya mdahalo, Bibi Masawda aliwakumbusha wanafunzi taratibu za mdahalo na umuhimu wa kuuliza maswali kama hawakuelewa.

Mwishoni mwa mdahalo, kura zilipingwa na mada iliamuliwa kutokana na kuungwa mkono na wengi. Bibi Msawda aliwakumbusha wanafunzi kuwa ilikuwa muhimu kuheshimu kila mawazo ya wanafunzi na sio kushangilia kuwa ‘Washindi’. Alifurahishwa na makundi yote kwa kutoa mawazo yakuvutia ikiwa kukubali au kupinga mada

Katika kipindi kilichofuata, Bibi Masawda aliwataka wanafunzi kutoa mawazo kuhusu kukuza uelewa wa jamii juu ya madhara ya kuchoma misitu na kuwapa njia mbadala za kutumia ardhi katika jamii yao. Aliandika mawazo yake ubaoni na kuwahamasisha wanafunzi kujadili mawazo hayo na familia zao.

## Shughuli muhimu: Kulinganisha maeneo

Chagua moja ya maelezo yaliyopo kwenye **Nyenzo 4 Mazingira tofauti** na ubandike darasani. Kama unapicha zilipigwa ziarani sehemu tofauti za Tanzania au kama unaweza kupata maelezo katika kitabu au magazeti unaweza kutumia. Jaribu kuchagua sehemu iliyotafauti sana na mazingira ya shule.

Waeleze wanafunzi picha ni ya wapi

Wapange katika makundi ya wanafunzi watatu au wane na watake kufikiri kati ya maneno manne hadi sita ya kuelezea eneo

Baada ya dakika tano, litake kila kundi kutoa neno moja. Andika maneno hayo ubaoni au kwenye karatasi

Halafu watake wanafunzi kufanya kazi katika makundi yao na kuorodhesha maumbo ya eneo hili yanayofanana na yanayotofautiana na mazingira yao.

# Nyenzo-rejea ya 1: Rasilimali asili na Makazi ya watu Tanzania

**Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi**

Kutoka siku za nyuma hadi leo, mfumo wa makazi ya watu umekuwa ukisababishwa na upatikanaji wa rasilimali asili. Chakula maji na makazi ni mahitaji muhimu ya binadamu na zinaonesha uwezo wa kustawi au kutostawi kwa jamii katika mazingira iliyopo. Jamii za zamani kama Lakoja ziliishi mabondeni ambako zilikuwa na uhakika wa kupata chakula na maji na pia zilipata njia za usafikiri kibiashara. Vile vile, ulinzi na matumizi bora ya rasilimali hatimaye yalionesha namna jamii ilivyojiimarisha na uwezo wa kuzitunza rasilimali kwa vizazi vijavyo

Moja ya tatu ya watanzania hupata chini ya milimita 800 za mvua, na hivyo ni jangwa au nusu jangwa. Moja ya tatu tu ya nchi inapata mvua zaidi ya mm 1000. Hata hivyo asilimia 7 ya ardhi ya Tanzania ni maziwa. Hii inajumuisha ziwa Viktoria (ziwa la pili kwa ukubwa duniani lenye maji yasiyo ya chumvi) ziwa Tanganyika (ziwa la pili kwa kina kirefu duniani) na ziwa nyasa. Maziwa ya ndani ni Rukwa, Eyasi na Manyara. Pia kuna mito mikubwa inayotiririsha maji kwenye maziwa. Watanzinia walioishi zamani wangeanzisha mfumo wa kilimo cha umwagiliaji kutoka kwenye vyanzo hivi vya maji wangezalisha zaidi mazao yao. Kwa mfano wachagga walianzisha mtandao wa umwagiliaji kwa kutumia mifereji au mfongo ambayo inakusanya maji kutoka vijito vya Kilimanjaro na kupeleka eneo la mashambani

# Nyenzo-rejea 2: Namna ya kudahalisha maada

**Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi**

Mdahalo ni majadiliano yaliyo rasmi. Upande mmoja unapinga mada na mwingine una kubaliana na mada. Kunawazungumzaji wakuu wa tatu kila upande na kuna muda maalumu ambao wanatakiwa kuwasilisha mitazamo yao. Mdahalo ni shughuli rasmi na ina taratibu Fulani ambazo lazima zifuatwe.

- Mwenyekiti huanzisha mada na wazungumzaji sita.
- Mzungumzaji wa kwanza kutoka kundi linalikubali mada huzungumza kwanza. Mzungumzaji wa kwanza huanzisha mada wanaweza kuongea kwa muda uliopangwa (kwa mfano, dakika 3 hadi 5 kila mmoja)
- Halafu, mzungumzaji kutoka kundi linalopinga mada huzungumza. Mzungumzaji huyu pia huanzisha mada lakini kutoka upande wa wanaopinga.
- Wanafuatiwa na wazungumzaji wa pili kutoka kila upande. Majukumu ya mzungumzaji wa pili ni kuendeleza mawazo kwa kutoa mifano halisi na ushahidi kushadidia mtazamo wa upande wake.
- Mwenyekiti hufungua mdahalo kwa watu wengine ambao huweza kuuliza maswali kwa mzungumzaji kutoa changamoto juu ya mawazo.
- Mzungumzaji wa tatu kutoka upande unaopingana na mada hutoa majumuisho ya mawazo ya kundi.
- Mzungumzaji wa tatu kutoka upande wa wanaokubaliana na mada hutoa majumuisho ya mawazo ya kundi. Darasa hupiga kura juu ya mada, kuzingatia uzito wa mawazo yaliyojadiliwa.

# Nyenzo-rejea 3: Kilimo cha kufyeka na kuchoma

**Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi**

Nini maana ya kilimo cha kufyeka na kuchoma?

Kilimo cha kufyeka na kuchoma ni pale ambapo msitu wa asili au wa kupandwa unapochaguliwa na kukatwa uoto wote kuruhusu ukauke. Miti mikubwa mara nyingi hubanduliwa magana kuruhusu ikauke ikiwa imesimama. Baadhi ya miti huachwa imesimama hasa ile inayoonwa kama ni muhimu kama miti inayozalisha chakula au ni muhimu kiuchumi. Sehemu ya miti hukatwa kuwa mbao au hukusanywa kutumika kama kuni na kutengeneza mkaa. Baada ya muda (juma ama mwezi) mabaki yaliyokauka huchomwa. Sehemu hiyo hulimwa mwa muda mchache (kwa kawaida mwaka mmoja hadi mitano) halafu inaachwa kwa kuwa rutuba imeisha na mazao hayawezi kustawi na magugu huota.

Mashamba haya yaliyoachwa mara nyingi hutumika kama malisho ya mifugo. Kama shamba limeachwa lioteshe uoto, malisho yatakuwa ni kwa muda tu. Hivyo misitu mara nyingine huachwa iote yenyewe kwa lengo la kufyeka na kuchoma kwa mara nyingine siku za usoni.

Uchomaji huondoa uoto na unaweza kutoa virutubisho vitakavyorutubisha udongo. Majivu pia huongeza kipimo cha Haidrojeni ya udogo mchakato unaofanya baadhi ya virutubisho( hasahasa fosiforasi) viwe vinapatikana kwa muda mfupi. Uchomaji pia huua muda wadudu wa ardhini, wadudu na mimea iliyokuwepo muda mrefu na kuwa majivu ambapo mazao mapya hupandwa. Kabla ya mbolea za chumvichumvi hazijawepo, moto jamii nyingi zilitumia moto kurutubisha ardhi.

Kilimo cha kufyeka na kuchoma huhitaji eneo lenye watu wachache au kuendelea kupata eneo jipya, kwa vile misitu kurudia katika hali yake ya zamani inaweza kuhitaji miongo au hata kizazi na kizazi. Katika misitu mingi ya kitropiki njia endelevu za kufyeka misitu na kuchoma zimekuwa zikitumika kwa miaka mingi, lakini ongezeko la watu na kukua kwa sekta ya viwanda kumefanya ukataji na uchomaji asilia usiwe endelevu na

Ingawa ni njia panda kwa nchi za tropiki zilizo na wingi mkubwa wa watu, kilimo cha kujikimu kinaweza kuwa ni njia nyepesi ya kulisha familia zao. Matokeo ya hukataji na kuchomaji misitu kwa mfumo wa ikolojia ni mbaya unapotumika kwa kiasi kikubwa. Kinachoathirika sana ni udongo usio na rutuba, unaopitisha maji kirahisi katika misitu ya kitropiki. wakati mboji imeondolewa hata kwa kuvuna kuni au mkaa-mabaki kwenye udongo huathiriwa kwa kiasi kikumbwa hivyo kuathiri uoto wa aina yoyote. Mara nyingine kuna mizunguko mingi ya ukataji na uchomaji misitu ndani ya mwaka mmoja; kwa mfano, mashariki mwa Madagaska jambo lifuatalo hujitokeza mara kwa mara. Katika hatua ya kwanza inaweza kukata miti yote kwa matumizi ya kuni au kujengea. Miaka michache baadae miti michanga iliyoota huvunwa kwa ajili ya mkaa, na miaka michache baadae shamba huchomwa kurutubisha haraka ardhi kwa ajili ya kuotesha nyasi za mifugo. Kama mashamba ya jirani yametengenezwa kwa mtindo unaofanana na huu, mmomonyoko wa udongo huweza kutokea kwasababu hakuna mizizi au hifadhi ya maji ya muda katika matawi kupunguza mtiririko wa maji juu ya uso wa dunia. Kwa jinsi hiyo kiasi cha virutubisho vilivyosalia ardhini vinasafishwa. Eneo hili ni mfano wa jangwa na hakuna uoto wowote unaoweza kuota kwa karne nyingi zijazo

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Urudishaji hali ya kawaida wa mfumo-ikolojia wa mandhari ya hapo juu umekuzwa zaidi kwasababu misitu ya tropiki ni makazi ya mifumo-ikolojia mchanganyiko, ulio na idadi kubwa ya aina ya viumbe vinavyoelekea kupotea. Kwa hiyo madhara ya kukata na kuchoma mimea ni makubwa kwa sasa duniani.

*Imenukuliwa kutoka: Wikipedia Slash and Burn, Website*

**Misitu ya malagasi yarudi hali yake**

**Taarifa kutoka shirika la habari la Uingereza-BBC**

Madagaska inapoteza kwa haraka misitu. Lakini wanavijiji wanakasirishwa na hatua zinazowazuia wao kukata miti katika hifadhi zilizotengenezwa hivi karibuni.

Madagaska ni kisiwa kikubwa katika bahari ya Hindi sehemu iliyosheheni aina 200000 za mimea na wanyama-robo tatu yake hazipatikani popote duniani na ni matokeo ya miaka mingi ya madadiliko tangu kisiwa kijitenge kutoka Afrika wakati mabara yanaundwa kwa mara ya kwanza.

Vilima vimefunikwa kwa misitu minene ya kijani iliyoenea kila kona. Miti hutanda juu kwa namna ya pekee kuzuia uoto chini yake. Anga hufunikwa na aina mbalimbali za ndege wa rangi tofauti.

Kakini si muda mrefu ambapo mandhari yatabadilika kuwa kame, yasiyo na uoto. Sehemu nyingine mmomonyoko wa udongo ni mkubwa unaoacha makorongo kwenye kingo za vilima.

Mimea michache sana humea hapa na hakuna wanyama.

**Hii lazima ifike mwisho**

Wanamazingira wanasema kilimo cha kukata na kuchoma -ambapo misitu hukatwa na kuchoma kusafisha kwa kupanda mazao-inaharibu misitu yakipekee na kuhatarisha maisha ya wanyama waishio humo.

‘Hii ni njia yetu ya maisha. Kama hatukati miti, hatuwezi pata chakula’. Dimanche Dimasy, mzee wa Mahatsara.

Katika mkutano wa dunia wa mazingira, uliokaa Afrika kusini mwaka

2003, Raisi Marc Ravalomanana alifurahishwa na wanamazingira na aliahidi kuongeza zaidi hifadhi ya rasilimali za Madagaska kutoka m1.7 hekta hadi m6 hekta ifikapo mwishoni mwa mwaka 2008.

‘[Kuna] kuna ujumbe mzito kutoka serikalini na kutoka kwa raisi mwenyewe ambaye anafuatilia hili na kuweka misingi,’ asasema Helen Crowley, mkurugenzi wa chama cha kuhifadhi mali asili-New York

Amelinganishwa na [raisi wa zamani wa Marekani] Teddy Roosevelt mwanzoni mwa karne iliyopita, ambaye aliona maliasili (misitu) ya nchi ikiharibiwa na kusema “Hii lazima ikome”.

**Uchomaji misitu kizazi na kizazi**

Lakini wafanyakazi wanasema kutekeleza mipango ya kuhifadhi mali asili katika kisiwa ambacho robo tatu ya wakazi wanaishi katika umasikini wa kutupwa itakuwa vigumu.

Serikazi imekwisha weka ramani kwa maeneo inayotaka kuyahifadhi na imeanza kuzungumza na jamii za mahali kabla ya kuwakataza kukata miti.

Hatua kadhaa zimekwisha chukuliwa kuhamasisha jamii ziishizo vijijini kuhusu umuhimu wa kutunza misitu

Lakini nilipoenda kutembelea hifadhi iliyotengenezwa hivi karibuni, ambamo kilimo cha kukata na kuchoma kimekatazwa, sikuona ushahidi wa watu wa mahali hapo kujulishwa.

“Kijiji chetu kimekuwa kikichoma misitu kulima mpunga kizazi na kizazi. Halafu wanakuja na kutuambia haturuhusiwi kufanya tena”. alisema Dimanche Dimasy, mzee wa kijiji cha Mahatsara, kilichopo ndani mwa hifadhi ya misitu ya mashariki mwa Mantadia.

‘Hii ni njia yetu ya maisha. Kama hatukati miti, hatuwezi pata chakula’.

‘‘Serikali inataka kuzuia misitu lakini hakuna mtu anayewajali na kuwatetea wakulima waishio hapa’

Wanamazingira wanasema kuna faida za muda mrefu kwa masikini kama watahifadhi misitu kama ardhi itatunza maji na virutubisho. Udongo ambapo miti imekatwa humomonyoka haraka, kupelekea isitumike, hivyo kuhitaji sehemu nyingine kusafishwa

**Mahitaji ya kila siku**

Lakini maafisa wa serikali wanasema kushawishi jamii za wakulima kuhusu umuhimu wa kutunza misitu ya Madagaska kunahitaji kubadilika kifikra.

‘Siyo kazi rahisi kubadili fikra za wakulima waishio vijijini’. Sylvain Rabotorison, waziri wa mazingira

Watu wanapokuwa masikini wanafikiri tu mahitaji yao ya kila siku’, anasema waziri wa mazingira, Sylvain Rabotorison

‘tunahitaji kuwaelimisha watu juu ya kwanini kutunzamazingira. Lakini siyo rahisi kubadili fikra za watu waishio vijijini-ina maana kubadili baadhi ya tabia za kizamani zisizo na tija.’

Yaweza maanisha pia kutafuta kitu mbadala kwa wao kufanya.

Mipango iko mbioni kuwafundisha njia bora za kilimo cha mpunga kinachoongeza mavuno lakini kinachotumia ardhi kidogo, na makundi ya utunzaji mazingira yanatoa majiko yanayotumia mkaa kidogo hivyo kupunguza ukataji miti.

Lakini mengi yanategemea kama faida za muda mfupi zinaweza kuletwa kwa watu masikini wa madagaska.

Bila ushirikiano wao, ahadi ya Raisi Ravalomanana itakuwa vigumu kufanikiwa.

*Imenukuliwa kutoka chanzo: BBC World, Website*

# Nyenzo-rejea 4: Mazingira tofauti

**Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi**



*Imenukuliwa kutoka chanzo: K43 Pbase, Website*

Urban Tanzania



*Imenukuliwa kutoka chanzo: K53 Pbase, Website*

Rural Tanzania

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

# Sehemu ya 3: Kuchunguza hali ya hewa

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kufanya ujifunzaji wa hali ya hewa kwa upana na kwa vitendo zaidi?

**Maneno muhimu:** kutatua tatizo, hali ya hewa, kazi ya kundi,mpangilio, uchunguzi, kuchangia mawazo

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- Umejenga uwezo wa wanafunzi wa kuchunguza, kukusanya data na utambuzi wa mpangilio wa hali ya hewa ili kuweza kutabiri hali ya hewa;
- Umetumia kazi za makundi kuhimiza ushirikiano wakati wanafunzi wanapobuni na kuandaa vifaa vya hali ya hewa.

## Utangulizi

Kwa watu walio wengi, kufuatilia hali ya hewa ni sehemu muhimu ya maisha ya kila siku. Kwa mfano, wakulima wanahitaji kutambua wakati muafaka wa kupanda mazao yao na wavuvi nao wanahitaji kujua ni wakati gani waingie baharini. Mlolongo wa hali ya hewa unatofautiana katika eneo la kusini mwa jangwa la Sahara, na vipindi vya mvua na vikavu navyo vinatofautiana. Ukiwahimiza wanafunzi wako kuchunguza mabadiliko ya mpangilio huo-hata yakiwa kidogo-kutawasaidia kuelewa uhusiano uliopo kati ya hali ya hewa, watu na mazingira yao.

Katika sehemu hii, utatumia kazi za makundi kujenga uwezo wa wanafunzi wa kushirikiana na kufikiria. Utapanga shughuli kwa vitendo ili kuhimiza ushirikiano kati yao.

## Somo la 1

Kuna imani nyingi na mashairi juu ya hali ya hewa katika sehemu mbalimbali duniani, ikiwemo Afrika. Kwa kutumia hivi kama kianzio cha kuchunguza hali ya hewa kutasisimua shauku ya wanafunzi wako ya kujua hali ya hewa ya mahali hapo na kuwahimiza kuwa makini na kukabiliana na mabadiliko katika mazingira yao ya asili. Kwa mfano, Nigeria, watu wa kabila la Yoruba inasemekana waliamini kuwa radi ni mzimu wenye nguvu ambao ulibeba nguvu za kichawi. Mzimu huo uliwakaripia kwa kutumia moto wa mwanga uliotoka mdomoni mwake. Uchunguzi kifani 1 unaonyesha njia moja ya kutumia misemo ya mahali hapo na wanafunzi wako

Ufundishapo kuhusu hali ya hewa, una utajiri wa nyenzo nje ya darasa lako. Kwa kuwaambia wanafunzi wako wakusanye data za hali ya hewa na kuangalia mpangilio katika data kwenye Shughuli 1, utakuwa umewahimiza wajijengee ujuzi wa kuchunguza.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Uchunguzi kifani ya 1: Kutumia elumu ya mila na desturi katika kujadili hali ya hewa

Bi. Ogun kutoka Abeokuta Nigeria alitaka kuwafundisha wanafunzi wake juu ya hali ya hewa na aliamua kuanza kwa kuwataka wamwambie walichokuwa tayari wanakifahamu kuhusu mada hiyo. Siku moja kabla ya kuanza mada hiyo, aliwaambia wanafunzi wake waulize familia zao na ndugu zao juu ya mashairi yoyote waliyokuwa wanajua yanayohusu hali ya hewa na kuyaleta shuleni.

Siku iliyofuata, aliwaambia wanafunzi wawili au watatu kuimba mashairi waliyopata Pia aliandika ubaoni mila na desturi chache zinazohusu hali ya hewa kutoka sehemu nyingine za Afrika (angalia **Nyenzo rejea 1: Elimu ya Mila na desturi za Kiafrika juu ya hali ya hewa** , zinazohusu maelezo ya kisayansi) na akajadili maana zake, ambazo si za kisayansi.

Halafu, aliwauliza ni kwa nini walidhani kuwa kuna mila na desturi tofauti zinazohusu hali ya hewa. Wanafunzi wake walitoa ushauri kuwa watu wa zamani hawakuelewa sababu za mabadiliko ya hali ya hewa na kwa maana hiyo, walibuni mila na desturi ili kuelezea mabadiliko hayo;

Bi. Ogun aliwauliza wanafunzi wake kwanini walidhani kuwa ni lazima kuelewa mpangilio wa hali ya hewa. Wanafunzi walishauri mawazo yafuatayo , ambayo aliyaandika ubaoni:

Kujua nguo za kuvaa. wakulima kujua mpangilio wa hali ya hewa, ili wapande mbegu, na kuvuna kwa wakati muafaka wa mwaka.

Kujipanga kwa ajili ya maafa ambayo yangeweza kutokea kutokana na hali ya hewa mbaya.

Aliwaambia wanafunzi wafanye kazi katika makundi ya watu sita, na kwa kutumia moja kati ya mawazo ya ubaoni,wabuni hadithi fupi inayohusu hali ya hewa. Baadhi ya wanafunzi waliandika hadithi zao na wengine waliamua kuziigiza darasani.

## Shughuli ya 1: Jedwali la hali ya hewa,utabiri na mabadiliko ya hali ya hewa

Mwambie kila mwanafunzi arekodi joto, hali ya anga, mvua na kasi ya upepo (marambili kwa siku) mabadiliko ya hali ya hewa kwa muda wa siku tano mfululizo. (Angalia Nyenzo **rejea muhimu 2: Jedwali la uchunguzi wa hali ya hewa** ). Wanafunzi watahitaji kutumia kati ya dakika tano hadi kumi, wakati uleule kila siku nje ya darasa kufanya uchunguzi na kujaza majedwali yao. Kwa wanafunzi wadogo, unaweza kuwapa baadhi

ya maneno yatakayoweza kuwasiadia kuelezea hali ya hewa, kwa mfano, upepo mkali, upepo mwanana, na hali tulivu.

Waonyeshe wanafunzi wako jinsi ya kusoma kipima joto na kurekodi hali ya joto ( kama huna kipima joto, waambie wakadirie hali ya joto, kama vile joto sana,vuguvugu n.k)

Mwishoni mwa wiki, waambie wanafunzi wakae kwenye makundi ya watu sita na walinganishe data zao walizokusanya. Zinashabihiana kwa kiasi gani? Kuna tofauti yoyote? Kama zipo, wanadhani zimesababishwa na nini? (Angalia **Nyenzo rejea muhimu: Kufanya kazi kwa makundi darasani kwako** .)

Halafu, waambie wabashiri hali ya hewa ya wiki inayofuata na warekodi utabiri wao kwa ajili ya kuonyeshwa darasani. Waambie watoe sababu za ubashiri wao.

Rekodi hali ya hewa ya wiki ijayo kama ilivyokuwa awali. Mwishoni mwa wiki,angalia hali halisi ya hewa ukilinganisha na ubashiri wao. Jadiliana nao ni kwa jinsi gani walikuwa sahihi, na namna gani wangeweza kufanya utabiri wao uwe sahihi zaidi.

## Somo la 2

Sayansi ya kujifunza hali ya hewa inaitwa metorolojia. Wana metorolojia hupima joto, mvua, mgandamizo wa hewa, upepo, hali ya unyevunyevu angani n.k. Kwa kuangalia data na mpangilio wanaopata, wanatabiri jinsi hali ya hewa itakavyokuwa siku za usoni. Hii ni muhimu kwa ajili ya kuwapa watu kiashirio mapema cha hali mbaya ya hewa kama vile mafuriko na

pepo za baharini, pia utabiri ni wa msaada sana kwa watu wengine kama wakulima.

Sehemu hii inapeleleza jinsi gani kutumia watalaamu wa mahali hapo kunaweza kuleta mvuto kwa wanafunzi na kuonyesha njia na uhalisia wa kujifunza hali ya hewa. **Shughuli 2** inatumia kutatua tatizo kama mbinu ya kuwasaidia wanafunzi kufikiri zaidi juu ya hali ya hewa.

Kama unaishi eneo lenye mvua za uhakika, ungeweza kuwaambia wanafunzi waandae kitu cha kupima mvua kila siku kwa muda wa majuma mawili.

### Uchunguzi kifani ya 2: Kutembelea kituo cha hali ya hewa

Bi Mboma alikuwa na bahati kwa kuwa kulikuwa na kituo cha hali ya hewa kilomita chache kutoka shuleni na aliweza kuandaa safari. Wiki chache kabla ya kutembelea huko, na baada ya kuwa ana ruhusa kutoka kwa mwalimu mkuu na kuwaeleza wazazi, aliwapigia simu watu wa kituo cha hali ya hewa ili kupanga tarehe na kuwaeleza nini angependa kufanya. Mhusika alikubali kuliongoza darasa kuzunguka kituo hicho, kuwaonyesha vifaa na kuelezea matumizi yake. Bi Mboma alimweleza kuwa darasa lilikuwa limeanza kujifunza juu ya hali ya hewa na lilikuwa na uelewa mdogo sana wa vifaa vya kupima hali ya hewa.

Kabla ya safari, Bi Mboma aliwaambia wanafunzi wake walichokuwa wanategemewa kufanya, walichotakiwa kwenda nacho na nini wangetakiwa kufanya ili kuhakikisha usalama wao wakiwa safarini.

Kituoni, wanafunzi waliona vifaa mbalimbali vya kupima hali ya hewa, ikiwa ni pamoja na kipimahewa, kipimamvua na vifaa vya kupima upepo. Bi Mboma aliwahimiza wanafunzi wake waulize maswali mengi. Kwa msaada wa afisa wa kituo, walijaribu kutumia baadhi ya vifaa. Vile vile waliweza kuangalia baadhi ya rekodi na kuona mpangilio wa hali ya hewa. Afisa alimpa Bi Mboma baadhi ya nakala za data ili atumie darasani.

Waliporudi darasani, Bi. Mboma aliwaambia kila kundi la wanafunzi sita wafikirie ni jinsi gani wangeweza kuunda kituo chao kidogo cha hali ya hewa na namna gani wangeweza kuchukua vipimo sahihi. Makundi yakatengenezwa na darasa zima likaanza kazi.

Somo liliisha kwa darasa kutoa ahadi ya kuihusisha jamii kuanzisha kituo chao cha hali ya hewa.

## Shughuli ya 2: Kupima upepo

Kwanza kabisa tengeneza propela na kipimaupepo. Hii inaweza kufanyika kwa kutumia vifaa rahisi na ungeweza kuomba msaada kutoka kwa mtu kutoka kwenye jamii ambaye anaweza kutengeneza. Ni vizuri kutumia muda mwingi kwa ajili ya hili kwa sababu vifaa vya kufundishia vinaweza kutumiwa na mwalimu mwingine na katika miaka ijayo (angalia **Nyenzo rejea 3: kupima upepo na kasi yake** kwa maelekezo ya kutengeneza hivi vifaa).

Toa tatizo la kutatuliwa na wanafunzi wako. Waulize, 'unadhani kuwa upepo uko sawa katika viwanja vyote vya shule? Unawezaje kutambua?'

Waache waliongelee hili kwenye makundi yao kuhusu kuchunguza hili.

Wazungukie na kusikiliza maelezo yao, ukiwauliza maswali kama italazimu. Tumia maswali kama 'Ungeweza kusimama wapi ili kuhisi upepo mkubwa?' 'Ungeweza kusimama wapi ili kuhisi upepo mdogo?'

Hakikisha kwamba kila kundi limeandaa mpango.Huu lazima uwe na matumizi ya mahali mbalimbali kuzunguka shule.

Mpango wa kila kundi unapokuwa tayari, waruhusu wakafanye uchunguzi. Ungeweza kuwapeleka nje kundi moja baada ya jingine. Inabidi warekodi uchunguzi wao kwenye jedwali (angalia **Nyenzo rejea 4: Jedwali la uchunguzi** ) kwa mfano).

Jadili matokeo na darasa zima:

Ni sehemu gain hapa shuleni unafikiri zina upepo mkubwa? Ni sehemu gain ya ya shule ina upepo mdogo?

Kwa nini kuna tofauti kati ya maeneo haya?

Waulize wanafunzi wako namna gani wangeweza kuona hali hiyo kwa mwaka mzima.

## Somo la 3

Wakati ni rahisi kukusanya data za hali ya hewa darasani kwa kipindi fulani, si rahisi kuchunguza madhara ya hali ya hewa kwa kipindi kirefu.

'Tabia ya nchi' huelezea mpangilio wa hali ya hewa wa mahali fulani kwa kipindi cha miaka mingi.

Njia moja ya kuwasaidia wanafunzi kuchunguza madhara ya muda mrefu ya hali ya hewa yaweza kuwa kutumia hadithi, kama **Uchunguzi kifani 3** unavyofanya. Hapa, wanafunzi wanaweza kufikiri juu ya mambo mapana zaidi. Nini kingeweza kutokea kama hali fulani ya hewa ingeendelea? **Shughuli muhimu** inatumia njia nyingine. Wanafunzi wanahimizwa kufikiri juu ya matatizo yanayoweza kutokana na hali ya hewa.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kuangalia madhara ya hali ya hewa kwenye maisha ya watu mbalimbali

Bi Mboma na wanafunzi wa darasa lake la tano walikuwa makini kuchunguza namna hali ya hewa ingeweza kuathiri watu na nyenzo nyingine katika njia tofauti. Aliamua kulihadithia darasa hadithi kwenye **Nyenzo rejea 5: Namna gani hali ya hewa ilimwathiri Bwana Hoja na familia yake**.

Alipokwisha kusoma hadithi yake kwa wanafunzi wake, Bi Mboma aliwapanga katika makundi, baadae akawapa mlolongo wa maswali.

Ni aina gani za hali ya hewa ambazo familia ya Bwana Hoja ilikumbana nazo?

Kwenye hadithi hii, hali ya hewa imebadilika mara ngapi?

Ni kwa vipi mkulima, Bwana Hoja, alijisikia kutokana na mvua kuongezeka ghafla?

Mvua ilikuwa na madhara gani kwenye mazao ya Bwana Hoja?

Unadhani ukosefu wa mvua katika eneo lake ungesababisha madhara gani kwa familia ya Bwana Hoja?

Ungejisikiaje kama ungepatwa na mabadiliko ya hali ya hewa yaliyoelezwa kwenye hadithi hii?

Mwalimu Mboma alimwambia mwanafunzi mmoja kutoka kwenye kila kikundi kuandika dondoo kutoka kwenye majadiliano yao ili kutoa mawazo ya kikundi kwa darasa zima mwishoni mwa muda wa majadiliano.

## Shughuli muhimu: Kuchunguza hali mbaya ya hewa

Changia mawazo na wanafunzi wako juu ya mifano ya hali mbaya ya hewa, kama vile, tufani, ukame, mafuriko, baridi sana, pepo kubwa.

Jadiliana na wanafunzi juu ya nini hutokea kwa kila janga. Ligawe darasa lako katika makundi. Waambie kila kundi kuchukua mfano mmoja wa hali mbaya ya hewa.

Itabidi wajaribu kufikiri juu ya matatizo ambayo hali hii ya hewa ingesababisha na kuyaandika kwa ufupi kuonyesha jinsi maisha yangeathirika.

Wape wanafunzi muda wa kutosha na wahimize watengeneze hiyo taarifa. Uliza maswali kama vile ‘Nini kingetokea kwenye mgawanyo wa maji?’ ‘Je kungekuwa na nishati? Chakula?’

# Nyenzo-rejea ya 1: Jdi ya Afrika kuhusiana na hali ya hewa, nyenzo rejea ya mwalimu

**Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi**

| **Nchi au eneo na aina ya hali ya hewa** | **Kiasili** | **Maelezo ya kisayansi** |
|---|---|---|
| Africa: Radi | Jadi: watu waliopigwa na radi walidhaniwa na waafrika wa zamani walio wengi kuwa ni kwa ajili ya hasira za miungu. miale ya radi ilifikiriwa kuwa ni‘miale ya haki’. | Sayansi: Radi hutokea pale ambapo umeme unasafiri kati ya maeneo mkabala yenye chaji ya umeme kwenye wingu, kati ya mawingu au kati ya wingu na ardhi. Miale ya radi kutoka kwenye wingu hadi ardhini (miale ya haki) inaanza kwa elektroni (chembechembe ambazo zimechajiwa asi (negative)) zikishuka kwa mwendo wa kuyumbayumba kutoka kwenye wingu, na zinatengeneza utepe wa ayani zilizochajiwa chanya kutoka ardhini.Ayani na elektroni zinapokutana, wimbi kubwa la chaji chanya husafiri kwenda juu kwaumbali wa kama km 96,000 (kama maili 60,000) kwa sekunde! Mchakato huu unaweza kurudia mara kadhaa kwa kipindi cha nusu sekunde, na hivyo kufanya radi ionekane kama inawaka. |
| Ethiopia: upepo | Jadi: watu wengi waliamini kuwa mapepo mabaya yaliishi katika pepo zivumazo, hivyo wangeweza kuufukuza upepo kwa visu. | Sayansi: Upepo unasababishwa na mkusanyiko wa nguvu changamani. Kupata joto na kupoa kwa hewa, husababisha mabadiliko ya uzito, au mgandamizo. Hewa huwa ina tabia ya kusafiri kutoka kwenye maeneo yenye mgandamizo mkubwa kwenda kwenye maeneo yenye mgandamizo mdogo. Hata tofauti ndogo ya mgandamizo kutoka eneo moja na lingine, inaweza kusababisha upepo wenye nguvu kuvuma. Msuguano kutoka kwenye vitu kama miti, milima na majengo huathiri upepo, hupunguza kasi yake, hutengeneza mawimbi, vikwazo n.k. Pia, kuzunguka kwa dunia hutengeneza kile kinachoitwamadhara ya Koriolisi ambapo pepo za kaskazini mwa ikweta hupinda kulia na zile za kusini mwa ikweta hupinda kushoto. |

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

| | | |
|---|---|---|
| Misri:<br>Jua | Jadi: wamisri wa kale, wakisafiri kutumia mto Nile, waliamini kuwa jua lilisafiri kukatisha anga kwa kutumia mtumbwi usio na kina kirefu. | Sayansi: Wakati jua linaweza kuwa linasfiri kukatisha anga, ni sisi ambao tunatembea kwenye uso wa nchi, kadri dunia inavyozunguka kwenye mhimili wake na kulizunguka jua. Mzunkuko mmoja huchukua masaa 23 na dakika 56, au siku moja na mzunguko mmoja wa kulizunguka jua huchukua siku 365.26, au mwaka mmoja wa kalenda. |
| Kenya:<br>Ngurumo za radi | Jadi: Mungu wa ngurumo za radi, Mkunga Mburu, anaaminika kusafiri katika mbingu kwa kutumia ng'ombe dume mkubwa mweusi akiwa na mkuikiradi kwenye mikono yake yote, tayari kuitupa mawinguni ili itoe sauti kubwa | Sayansi: Kelele tunazoita "Ngurumoza radi"-zinatokana na hewa iliyopata joto la zaidi ya nyuzi 43,000 °F wakatiradi inawaka ngurumo zinaongezeka na baadae taratibu kupungua radi inapoacha. |
| Nigeria:<br>Radi | Jadi: Wayoruba inasemekana kuwa waliamini kuwa radi ilikuwa ni mzimu wa dhoruba ambao ulibeba nguvu kali za uchawi. Mzimu uliwakemea kwa kutumia miale ya moto ya radi kutoka mdomoni mwake. Iliaminika kuwaadhibu watu kwa matendo yao mabaya kwa kuwaharibia vitu vyao ardhini au kwa kumpiga mtu kwa miale yake ya mwanga. | Sayansi: Radi hutokea pale ambapo umeme unasafiri kati ya maeneo mkabala yenye chaji ya umeme kwenye wingu, kati ya mawingu au kati ya wingu na ardhi. Miale ya radi kutoka kwenye wingu hadi ardhini (miale ya haki) inaanza kwa elektroni (chembechembe ambazo zimechajiwa kinegative) zikishuka kwa mwendo wa kuyumbayumba kutoka kwenyewingu, na zinatengeneza utepe wa ayani zilizochajiwa chanya kutoka ardhini.Ayani na elektroni zinapokutana, wimbi kubwa la chaji chanya husafiri kwenda juu kwa umbali wa kama km 96,000 (kama maili 60,000) kwa sekunde! Mchakato huu unaweza kurudia mara adhaakwa kipindi cha nusu sekunde, na hivyo kufanya radi ionekane kama inawaka. |
| Afrika za kusini mashariki:<br>Upinde wa mvua | Jadi: Wengi wa wazulu wa zamani walifikiri kuwa upinde wa mvua ni nyoka aliyekunywa maji kutoka madimbwi ya maji ya ardhini. Kutokana na hii hadithi, nyoka huyu angeweza kuishi kwenye dimbwi lolote ambalo alikuwwa anakunywa na kummeza yeyote ambaye angetokea kwenda kuoga kwenye dimbwi hilo. | Sayansi: Pinde za mvua zinatokana na mvua. Matone ya mvua huwa kama vimche vidogodogo yanapopigwa na jua, huupindisha mwanga wa jua na kuugawa katika rangi tofauti. Upinde wa mvua huonekana kutoka angani hadi kukutana na uso wa nchi. Ili kuuona upinde wa mvua, ni lazima uwe umesimama jua likiwa nyuma yako, ukiiangalia mvua inanyesha kutoka upande mwingine wa anga. Upinde wa mvua unaweza kumaanisha kuwa mvua inaelekea kwisha, kwa sababu jua lazima liwe linachomoza kupitia mawinguni ili upinde uonekane. |

*Imenukuliwa kutoka chanzo: NASAhttp://scijinks.jpl.nasa.gov/weather/*

# Nyenzo-rejea 2: Jedwali la unchunguzi wa hali ya hewa

**Kwa matumizi ya mwanafunzi**

| **Wiki 1: Hali halisi** | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Muda wa siku** | **kipimo** | **Siku 1** | **Siku 2** | **Siku 3** | **Siku 4** | **Siku 5** |
| Asubuhi | joto<br>hali ya anga<br>Mvua<br>Kasi ya upepo | | | | | |
| Mchana | joto<br>hali ya anga<br>Mvua<br>Kasi ya upepo | | | | | |

| **Wiki 2: Utabiri** | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Muda wa siku** | **Vipimo** | **Siku 1** | **Siku 2** | **Siku 3** | **Siku 4** | **Siku 5** |
| Asubuhi | joto<br>hali ya anga<br>Mvua<br>Kasi ya upepo | | | | | |
| Mchana | joto<br>hali ya anga<br>Mvua<br>Kasi ya upepo | | | | | |

# Nyenzo rejea 3: Kupima mwelekeo na kasi ya upepo

**Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi**

**Kutengeneza kipimo cha mwelekeo wa upepo**

Utahitaji:

- Pini iliyonyooka
- Kipande cha kadi
- bua
- mkasi
- penseli yenye kifutio
- utepe


Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net


**Fanya hivi:**

1. Kata kichwa na mkia wa mshale kutoka kwenye kipande cha kadi.
2. Zifunge kwenye ncha mbili za bua.
3. Kandamizia pini katikati ya bua.
4. Chomeka pini kwenye kifutio cha penseli. Hakikisha kuwa bua linaweza kuzunguka bila kikwazo.

*Chanzo halisi: Galaxy Net, Website*

**Kutengeneza anemometa kwa ajili ya kupima kasi ya upepo**



Anemometa ni kifaa kinachokueleza kasi ya upepo unaovuma. Anemometa halisi itaweza kupima kwa usahihi zaidi. Mfano uliotengeneza unaweza kukupa mwelekeo wa kasi ya upepo unaovuma, lakini hautakuwa sahihi kama anemometa yenyewe.

**Unahitaji:**

1. mkasi
2. vikombe vidogo vya karatasi
3. kalamu
4. vipande viwili vigumu vya kadibodi-vyenye urefu sawa
5. pini ya kuchorea
6. fimbo
7. udongo wa mfinyanzi kidogo
8. saa inayoonyesha sekunde

**Fanya hivi:**

1. Kata ncha za vikombe vya karatasi zilizojikunja ili kuvifanya viwe vyepesi.
2. Paka rangi kikombe kimoja kwa nje kwa kalamu ili uweze kukiona kila kinapozunguka.
3. Pishanisha vipande vya kadibodi ili vitoe alama ya (+). Vishikishe pamoja na uweke alama katikati.
4. Chomeka au pigilia mpishano wa kadibodi juu ya fimbo.
5. Puliza vikombe kuhakikisha kuwa kadibodi inazunguka sawasawa.
6. Uweke udongo wa mfinyanzi nje, kama vile kwenye ukingo wa miti, ukuta au mwamba. Chomeka ncha kali ya penseli kwenye udongo isimame wima.

**Kupima kasi ya upepo:**

Kwa kutumia saa, hesabu idadi ya mizunguko ya kikombe chenye rangi katika dakika moja. Unapima kasi ya upepo kwa kutumia idadi ya mizunguko kwa dakika. Anemometa ya watabiri wa hali ya hewa hubadili hii kasi kuwa maili kwa saa (au kilkomita kwa saa).

## Nyenzo rejea 4: Jedwali la uchunguzi

**Kwa matumizi ya mwanafunzi**

| | Mahali 1 | Mahali 2 | Mahali 3 | Mahali 4 | Mahali 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Kasi ya upepo** | | | | | |
| **Mwelekeo wa upepo** | | | | | |

# Nyenzo rejea 5: Ni jinsi gani hali ya hewa ilimwathiri Bwana Hoja na familia yake

**Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi**

Bwana Hoja ni mkulima na ni mkuu wa familia yenye watoto sita.

Siku moja, familia ya Hoja iliamka kwenye hali ya hewa safi na ya jua. Wakiwa njiani kwenda shambani, mtoto mdogo kuliko wote alikuwa akilalamika kuwa jua kali, na alivua shati lake kwa sababu ya joto.

Kipindi cha mchana, wakati kila mtu alikuwa anafanya kazi shambani, mvua ilianza kunyesha.Kila mtu alilowa kwa maji ya mvua na waliacha kufanya kazi hadi hapo mvua ilpoacha kunyesha kwa muda kama wa saa zima. Wakati huo, mtoto mdigo alikuwa akifurahia mabadiliko ya hali ya hewa na alikimbia shambani akicheza na maji na majani ya miti.

Baada ya mvua, watoto ghafla waligundua kuwa joto lilikuwa limepoa. Hii hali iliwahamasisha kufanya kazi kwa masaa mengine mawili kabla hawajaondoka kurudi nyumbani.

Bwana Hoja hakuwa anategemea mvua siku hiyo na hivyo hakuwa na furaha kwa sababu mvua ilimharibia mipango yake ya siku hiyo shambani, lakini alimshukuru Mungu kwa kuwa mvua ingeboresha mazao yake.

Usiku ule, hali ya hewa ikawa ya baridi sana na familia ilibidi iwashe moto mkubwa na kuuzunguka ili kupasha miili yao joto kabla ya kwenda kulala.

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

# Sehemu ya 4: Utafiti wa mabadiliko wa Mazingira

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kukuza upeo wa masuala ya rasilimali na uchafuzi wa mazingira?

**Maneno muhimu:** mazingira; tafiti kundi; ziara; rasilimali; ongezeko la joto; uchafuzi

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- umetumia njia tofauti kukuza ufahamu juu ya uchafuzi na mabadiliko ya hali ya hewa.;
- umetumia mbinu za utafiti kusaidia wanafunzi kupeo kuelewa madhara ya uchafuzi;
- umetumia kazi za makundi na ziara rahisi kukuza ufahamu wa wanafunzi juu ya rasilimali asili.

## Utangulizi

Ukuzaji wa ufahamu wa wanafunzi wako kuhusu mazingira yao na hitaji la kulinda na na kuhifadhi mazingira ni muhimu katika kuelewa majukumu yao ya kutunza mazingira kwa ujumla. Sehemu hii inalenga kukusaidia kuandaa kipindi na shughuli zitakazo husisha kuifadhi mazingira ya mahali fulani na matatizo ya uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa duniani. Kuwasaidia wanafunzi wako, unatakiwa kusoma kuhusu masuala ya mazingira. Hii itakupa mchango wa mawazo kuhusiana na kipindi na kukufanya uwe na mtazamo wa kisasa.

kadili wanavyohusishwa na shughuli zenye maana kwao kwa kutafiti masuala kama uchafuzi wa mazingira katika maisha halisi na kwa kufanya majaribio, wanafunzi wako watafurahia kujifunza,

## Somo la 1

Wanafunzi wako wanajua nini kuhusu rasilimali za mahali? Sehemu hii inahusu kuongeza ufahamu wa wanafunzi wako juu ya rasilimali asili- hasahasa mimea inayopatikana kwenye maeneo yao.

Njia nzuri ya kufanya hivi ni kukusanya wataalam wa maeneo hayo kuzungumzia juu ya rasilimali asili kama ilivyo katika uchunguzi kifani 1. Wataalamu huleta elimu fulani ambayo wewe na wanafunzi wako mtajifunza. Kutumia wataalamu hufanya ujifunzaji uwe wa kusisimua kwa sababu ni tofauti na ilivyozoeleka.

Katika shughuli 1, unapanua upeo wa wanafunzi wako wa mazingira yao kwa kutumia ziara za kimasomo ambapo wanahusishwa kikamilifu katika ukusanyaji wa taarifa. (kama unafanyia mazingira ya mjini au kama mazingira siyo salama kwa wanafunzi kutembea, unaweza kubadili shughuli na kuangalia chakula sokoni. Mtake kila mwanafunzi kutaja majina matano ya vyakula vinavyotokana na mimea na kujaribu kutafiti wapi vinazalishwa.)

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Uchunguzi kifani ya 1: Kutafiti rasilimali muhimu za mahali

Bibi Hlungwane hufundisha shule ya msingi Hoxane iliopo mji wa Limpopo Afrika Kusini na huwataka wanafunzi wake kupanua ufahamu wao kuhusu mazingira na rasilimali asili zake. Alisoma kuhusu wataalamu wa mahali na elimu kuhusu mimea ya dawa, na anafikiri kuangalia mimea ya mahali hapo, ikijumuisha ile inayotumia kuponya, inaweza kuwa njia nzuri ya kupanua mawazo kuhusu rasilimali kutoka **sehemu ya 2.** Aliamua kuwasiliana na wataalam saba wa mimea wanaoishi karibu na shule na kuwaalika kuja shule kuhojiana na wanafunzi katika siku iliyopangwa. Walikubali kukusanya baadhi ya mimea muhimu iliyopo katika maeneo yao ili kuwaonesha wanafunzi.

Bibi hlungwane aliwagawa wanafunzi katika makundi saba, kila kundi na mgeni wake. Alijadili na wanafunzi wake umuhimu wa kuonesha heshima kwa wageni. Kwa pamoja waliandika orodha ya maswali ya kuuliza. Alipendekeza kwamba watafiti vitu vitatu kwa kila mmea:

mmea unaitwaje;

huota wapi katika kijiji chao

Mmea wa chakula au wa dawa

Baada ya kuwashukuru na kuwaaga wageni wake, kila kundi kilitoa mlishonyuma (feedback) na Bibi Hlungwane aliandika taarifa hizo ubaoni katika sehemu tatu:

mimea ninayoiona jirani na shule

Je niyakupandwa? ( Rejea nyenzo 1: kijitabu cha taarifa za mimea)

Halafu, hujadili namna ya kutunza mimea hii kwa kuwa ni rasilimali muhimu kwa jamii. Wanaamua kuwa kujifunza kwa kutambua mimea bila kuitoa mahali ilipo ni muhimu. Pia kwamba wasiikanyage au wasiharibu mazingira inamoota

Mwisho, Bibi Hlungwana huwataka wanafunzi katika makundi kutengeneza majumuisho ya mimea muhimu kuonesha matumizi ya kila mmea na wapi unapatikana.

## Shughuli ya 1: Utafiti wa rasilimali mimea ya mahali

Jedwali litawasaidia wanafunzi kuona nini hasa wanatakiwa kufanya.

Mtake kila mwanafunzi kuchora jedwali na kuandika uchunguzi wake. Chora jedwali ubaoni ili wao wanukuu.

**Jina la mmea unapatikana wapi? Tunautumia? Kwa namna gani?**

Wapeleke nje katika jozi kwenye mazingira yanayoizunguka shule, kwa dakika kama 30 na watake kujaza kwa uchache misitari mitano ya jedwali. Tembea na wanafunzi na wasaidie.

Kama wanafunzi hawajui jina la mmea, wahamasishe kutoa maelezo au kuuchora kwa utambuzi baadae.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Wanaporudi darasani chora jedwali kubwa ubaoni. Zunguka darasa na jaza taarifa za wanafunzi wote kwenye jedwali hilo

Waulize wanafunzi nini wamejifunza kutokana na kipindi cha leo kuhusu mazingira asilia na aina za rasilimali ilizonazo kwa jamii.

## Somo la 2

Kwa kuwa mazingira asili yetu yanaweza kutupatia mahitaji yetu, unahitajika kuwashawishi wanafunzi wako kufikiri juu ya namna ya kutunza mazingira ili yaendelee kutupa tunachohitaji.

Ili wanafunzi wako waanze kufikiri kuhusu uharibifu wa mazingira unaofanyika, unaweza kuwaonyesha madhara ya uchafuzi wa mazingira. Hiki ndicho mwalimu katika **uchunguzi kifani 2** alifanya kwa darasa lake. **Shughuli 2** inaonesha njia nyingine-kufanya jaribio linaloonesha madhara ya uchafuzi wa maji au uhaba wa maji katika ukuaji wa mimea. Mara wanafunzi wakiona madhara yaliyotokana na uchafuzi huo, watakuwa katika hali nzuri ya kukuza mtazamo chanya juu ya utunzaji wa mazingira

## Uchunguzi kifani ya 2: Kutumia ziara za mafunzo kutafiti uchafuzi

Hema Joto, mwalimu wa darasa la sita katika shule ya msingi Wema, anataka kukuza upeo wa wanafunzi juu ya madhara ya uchafuzi ya maji (Rejea **Nyenzo 2: masuala ya maji** kwa taarifa za msingi). Anagundua kuwa anaweza kufanya hili kwa kuwapeleka ziara ya mafunzo kwenye mto uliojaa takataka.

Mtoni, anawataka wanafunzi kutengeneza orodha ya kila kitu wanachokiona kinachafua maji. Wanafunzi walipokuwa wamefanya hilo, walikaa kwenye ukingo wa mto na Hema aliwauliza maswali ya msingi kuwahamasisha kufikiri zaidi ya kile wanachokiona. Kwa mfano aliwauliza kuwa, watu wangapi wanategemea mto huu?

Nini kingetokea kwa watu wote kama maji ya mto yangechafuliwa? Wanatumiaje maji haya?

Darasani, aliwataka kila kundi kueleza njia za kusaidia kusafisha mto na mazingira yake. Kadili anavyozunguka zunguka darasani, husikiliza na

kuwasaidia. Alishangazwa na mawazo waliyokuwa nayo wanafunzi. Mawazo hayo yalijumuisha, kuihusisha jamii na shule kuzuia uchafuzi sio kwenye mto tu bali na maeneo mengine ya kijiji. Hema alijisikia amefanikiwa lengo la kukuza upeo wa madhara ya uchafuzi wa maji na aliridhishwa na ushawishi wa mtazamo wa wanafunzi kwa jamii.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Shughuli ya 2: Jaribio la uchafuzi

Kujikumbusha au kukuza upeo wako kuhusu masuala ya maji soma Nyenzo 2. Jaribu shghuli hii mwenyewe kabla ili uwasaidie vizuri wanafunzi wako

Watake wanafunzi wako kufanya jaribio litakalochukua siku tano, ilivyoelezwa katika Nyenzo 3: Jaribio la mbegu za mahindi

Halafu watake kila mwanafunzi kuandika utabiri wake juu ya kitakachotokea kwa kila mbegu kwa siku tano.

Watake kuangalia maendeleo ya mbegu zote tatu kila siku

Wanafunzi watengeneze dondoo za uchunguzi wao wa kila siku. Unaweza kuhusika kwa kutengeneza dondoo zako mwenyewe.

Siku ya tano, fanya majadiliano ya kina pamoja na wanafunzi kuhusu kama utabiri wao umetokea au haukutopkea. Nini kimetokea kwa kila mbegu?Jadili matokeo ya jaribio kwa kuzingatia uchafuzi. Mnaweza kufikiri jaribio jingine juu ya uchafuzi wa mazingira

## Somo la 3

Wanafunzi wengi wamevutiwa na kile kinachotokea katika mazingira yao na matumizi ya rasilimali kama magazeti au redio vinaweza saidia kuimarisha kipindi chako.

Lengo la shughuli muhimu ni kuhamasisha wanafunzi kufikiri jinsi mabadiliko ya hali ya hewa duniani yanavyoweza kuathiri mazingira ya mahali fulani, na kuwapa wazo la kuongezeka kwa joto kama maelezo yanayoweza kusababisha mabadiliko ya hali ya hewa.katika uchunguzi kifani 3, mwalimu alitumia taarifa za mahali kama sehemu ya kuanzia kufundisha juu ya mzunguko wa maji.

Mara wanafunzi wakiweza kuona uhusiano baina ya matukio unaweza kuanza kupanua ujuzi wao wa kufikiri kwa kina. Ujuzi huo utawasaidia kujenga hisia juu ya kila badiliko katika dunia wanamoishi

## Uchunguzi kifani ya 3: Matumizi ya magazeti katika kufundisha mzunguko wa maji

Kumekuwa na mijadala mingi kuhusu maji katika magazeti wiki lililopita. Matumizi ya maji yamezuiwa. Maji yaingiayo bwawa la Pangani ni kidogo. Kulikuwa na uzalishaji mdogo kaskazini mwa nchi

Muhgare aliona uwezekano wa kujadili masuala ya upatikanaji wa maji na wanafunzi wake. Aliandika swali hili ubaoni. ‘mvua yote huenda wapi ardhi inapokauka? Na halafu aliwataka kila kundi la wanafunzi kuongelea hili kwa dakika kumi. Wakati huo alizungukia makundi na kuhamasisha kila mmoja kutoa mawazo yake

Halfu Muhgare alikusanya wanafunzi kumzunguka na aliwataka kubadilishana mawazo. Wanafunzi kwa pamoja walielewa kuhusu mzunguko wqa maji ( **Rejea Nyenzo 4: Mzunguko wa maji)**

Muhgare alimaliza kwa kuchora mchoro unaoonyesha mzunguko wa maji ubaoni na kuwataka wanafunzi kunakili mchoro huo.

## Shughuli muhimu: Ongezeko la joto

Soma **Nyenzo 5: makala yanayohusu ongezeko la joto kabla ya kipindi**

Gawanya darasa katika makundi madogo na halafu wasomee makala au wape kila kundi nakala ya kusoma pamoja

Waelezee wanafunzi kuhusu mfumo wa barafu ya Kilimanjaro katika miaka kumi iliyopita( Rejea **Nyenzo 6: Barafu ya Kilimanjaro**)

Waamuru kila kundi kutoa bango au mchezo mfupi kujibu maswali yafuatayo

Nini kinasababisha ongezeko la joto?

Ni madhara gani yanaweza kusababishwa na ongezeko la joto? Nini tunaweza kufanya kupunguza ongezeko la joto? Utawaulizaje wanafunzi kutathmini kazi yao?

Unaweza kushirikishana kazi ya wanafunzi juu ya ongezeko la joto pamoja na wanafunzi wengine.

## Nyenzo-rejea ya 1: Kijitabu cha mimea

**Matumizi ya wanafunzi**

| **Utafiti wa mimea** | | |
|---|---|---|
| **Mimea ninayoiona eneo la shule** | **Mmea huu ni wakupandwa?** | **Tunaitumia mmea huu kama ndio tunaitumiaje?** |
| mahindi | Ndio | Chakula |
| mti wa miiba | Hapana | Mpini wa jembe |
| Waridi | Ndio | Hapana |
| mchungwa | Ndio | Chakula |
| Mwembe | Ndio | Chakula |
| mguva | Ndio | Chakula |
| Mpingo | Hapana | Mafuta, |
| | | |
| | | |
| | | |

# Nyenzo-rejea 2: Masuala ya maji

**Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi**



**Uchafuzi wa maji**

Uchafuzi husababiswa na:

- Takataka na mbolea za chumvuchumvi
- Matope na mchanga (mkusanyiko wa mawe ambao huwa katika matabaka)
- Malighafi zitokanazo na viumbe hai kama majani na nyasi zilizo katwa

**Matumizi ya maji**

Matumizi ya maji duniani yameongezeka mara sita zaidi kati ya mwaka

1900 na 1995 zaidi ya mara mbili ya kiwango cha ongezeko la watu-na huendelea kukua kadri kilimo viwanda na matumizi ya nyumbani yaongezekavyo. Kilimo hutumia takribani asilimia 70 ya matumizi yote ya maji duniani. Maji yatahitajika zaidi kadri watu watakavyoongezeka-inakadiriwa kuwa watu wataongezeka kutoka bilioni 6 sasa hadi bilioni8.9 ifikapo mwaka 2050



Tunaohitaji maji sio sisi tu bali kila kiumbe kinachoishi katika dunia hii pamoja nasi-na mfumi-kolojia ambapo viumbe hutegemeana

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Ugonjwa


Zaidi ya watu milioni tano hufa kutokana magonjwa yatokanayo na maji kila mwaka –mara kumi ya idadi ya watu wanaokufa kutokana na vita.

Mabadiliko ya hali ya hewa

Mabadiliko ya hali ya hewa yatakuwa na athari. Baadhi ya maeneo yanaweza kufaidika na ongezeko la mvua, lakini maeneo mengine huathirika kutokana na ongezeko hilo la mvua.Tunatakiwa kufikiri tena

kwa kiwango gani tunahitaji maji kama tunajifunza namna ya kushirikiana maji. Wakati mabwawa na miradi mingine mikubwa ikiwa na umuhimu mkubwa kwa jamii duniani kuna ongezeko utambuzi wa thamani ya kutumia maji tuliyo nayo vizuri kuliko kuvuna maji bila mpangilio. Mamilioni ya watu duniani hutegemea maji ili waishi, na kukosekana kwake hupelekea kifo.

**Mgawanyo wa maji duniani**




## Nyenzo-rejea 3: Jaribio la mbegu za mahindi

**Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi**

Jaribio

- madishi matatu, yenye utambulisho 1, 2, 3
- udongo
- mbegu tatu za mahindi
- maji
- mafuta ya taa

Njia: Siku ya jumatatu, panga madishi matatu na kila moja panda mbegu ya muhindi udongoni

weka maji kwenye dishi la1 na la 2, na mafuta ya taa kwenye dishi la 3. Kwa kila siku ya juma, weka maji kwenye dishi la 1, usiweke chochote kwenye dishi la 2, weka mafuta ya taa kwenye dila 3.

Mategemeo: Unaamini nini kitatokea kwa mbegu kwa siku tano zinazofuata?


**Uchunguzi**

| | | | |
|---|---|---|---|
| siku ya kwanza | 1 | 2 | 3 |
| | | | |
| siku ya pili | | | |
| | | | |
| siku ya tatu | | | |
| | | | |
| siku ya nne | | | |
| | | | |
| siku ya tano | | | |

**Hitimisho:**

# Nyenzo-rejea 4: Mzunguko wa maji

**Taarifa za msingi/ ujuzi wa mada kwa mwalimu**




*Chanzo: Environmental Protection Agency, Website*

# Nyenzo-rejea: 5: Makala inayohusu kuongezeka kwa joto

**Taarifa za musingi/ ujuzi wa mada kwa mwalimu**

**Makala**

Ongezeko la joto linasababisha mabadiliko ya hali ya hewa duniani, au vipindi virefu vya hali ya hewa, ambavyo hutofautiana kutoka eneo moja hadi jingine. Kadili dunia inavyozunguka,joto jipya huzunguka pamoja na dunia, ikichukua mvuke kutoka baharini, huongezeka hapa kutua mahali. Inabadilisha uwiano wa hali ya hewa ambayo viumbe hai hutegemea.

Tutafanya nini ili kupunguza ongezeko la joto? Namna gani tutabadilika ili kuendana na mabadiliko ambayo tayari tunayo? Wakati tukipambana na hili, sura ya dunia tunayoifahamu – pwani, misitu, mashamba na barafu iliyofunika milima vinatoweka.

**Athari za gesi joto**

Athari za gesi joto ni ongezeko la joto ambalo hutokea wakati gesi fulani angani zinapofyonza joto. Gesi hizi huruhusu mwanga lakini kama ukuta wa kioo wa nyumba za kuzalishia mimea hutunza joto lisipotee.

Kwanza,mionzi ya jua hutua kwenye uso wa dunia ambapo hufyonzwa na halafu mionzi hiyo hurudi tena angani kama joto. Angani, Gesi joto hufyonza baadhi ya joto na joto jingine hupotea hewani.Kadili gesijoto zinavyoongezeka angani ndivyo joto hufyonzwa zaidi.

Wanasayansi walijua juu ya athari za gesijoto tangu 1824,na wamekokotoa kuwa dunia ingekuwa baridi sana kama kusingekuwa na anga. Athari za gesijoto ndizo zinazofanya hali ya hewa ya duniani iweze kuishika.Bila hiyo,sura ya dunia ingekuwa na wastani wa kiwango cha 60 oF cha baridi. Binadamu huweza kuongeza kiasi cha gesi joto kwa kutengeneza gesi za kaboni dioksaidi (co2)

Kiwango cha gesi joto kimekuwa kikiongezeka na kupungua katika historia ya dunia, lakini kimekuwa hakibadiliki kwa miaka elfu iliyopita. Wastani wa kiwango cha joto duniani kimekuwa cha kawaida tangu muda mrefu hadi hivi karibuni. Kupitia kuchoma mabaki ya mafuta na utoaji gesi joto, binadamu wanaongeza athari za gesi joto na ongezeko la joto duniani.

Kwa kawaida wanasayansi hutumia neno “mabadiliko ya hali ya hewa” badala ya ongezeko la joto duniani.Hii ni kwa sababu kadili wastani wa joto unavyoongezeka duniani upepo na mikondo ya bahari inaondoa joto kwa njia ambazo zinaweza kusababisha baridi baadhi ya maeneo, joto na kubadili kiwango cha mvua na kiasi cha barafu. Matokeo yake, hali ya hewa hubadilika tofauti katika maeneo tofauti.

**Je mabadiliko ya joto sio ya asili?**

Wastani wa joto duniani na kiwango cha kaboni dioksaidi (moja ya gesi joto) kimepungua kwenye mzunguko kwa mamia ya maelfu ya miaka kulingana na sehemu ilipo dunia na jua vinavyotofautiana. Matokeo yake, theruji inakuja na kupotea.

Hata hivyo, kwa miaka mingi sasa, uzalishaji wa gesi joto angani umewianishwa na gesi joto zilizozinafyonzwa kiasili .Matokeo yake kiwango cha gesi joto na joto vimekuwa sawa(havibadiliki).Usawa huu umeruhusu jamii ya watu kuendelea kuwepo katika hali ya hewa isiyobadilika.

Mara chache,sababu nyingine huchangia kuongezeka au kupungua kwa joto. Kwa mfano milipuko ya volkano hutoa chembechembe ambazo huifanya sura ya dunia kuwa ya baridi kwa muda. Lakini hizi zina madhara yasiokwisha katika miaka machache.

kwa sasa,binadamu wameongeza kiwango cha karbon dioksaidi angani kwa zaidi ya theruthi tangu mapinduzi ya viwanda.Mabadiliko haya makubwa yana historia ya miaka mingi,lakini kwasasa yanatokea zaidi ya mwendo wa miongo mingi.

**Kwanini hili ni tatizo?**

Ongezeko la haraka la gesi joto ni tatizo kwa sababu linabadilisha hali ya hewa kwa haraka kuliko baadhi ya viumbe hai vinavyoweza kubadilika. Pia hali ya hewa mpya na isiyotabirika hutoa changamoto ya pekee kwa maisha.

Kihistoria, hali ya hewa duniani mara nyingi imebadilika, joto limepungua na kuongezeka kama hili tunaloliona leo na baridi kali iliyofunika sehemu kubwa ya Amerika na Ulaya. Utofauti kati ya kiwangi cha joto duniani cha leo na cha wakati wa barafu ni 5 centigradi na hutokea taratibu,kwa miaka mingi kwa sasa, kwa kiwango cha gesi joto kupanda, sehemu zilizobaki na barafu duniani (kama Greenland na Antaktika) nako barafu

imeanza kuyeyuka pia. Maji ya ziada yanaweza kuongeza kina cha bahari.

Hali ya hewa inaweza kubadilika kwa njia isiyotegemewa. Mbali na Kuongezeka kwa kina cha bahari , hali ya hewa inaweza kuwa baridi au joto kuzidi kiwango. Hii ina maana mvua kubwa zaidi za mawe, mvua nyingi zikifuatiwa na vipindi virefu vya ukame(changamoto kwa uzalishaji wa mazao), mabadiliko katika kiwango ambacho mimea na wanyama wanaweza kuishi,na upungufu wa maji ambayo kihistoria yametoka na barafu.

Wanasayansi wameshaona baadhi ya haya mabadiliko yanatokea haraka zaidi kuliko hata ilivyotegemewa.Miaka 11 kati 12 ya joto jingi tangu kumbukumbu zianze kupatikana ilikuwa kati ya mwaka 1995 na 2006.

**Makala ya 2** inangalia madhara ya kuongezeka kwa joto Afrika. Bara la Afrika ni tajiri kwa mfumi-kolojia mbalimbali,unaonzia theruji na barafu ya mlima Kilimanjaro misitu ya tropiki hadi jangwa la sahara.Hata kama lina matumizi madogo ya nguvu kuliko mabara mengine duniani, Afrika linaweza kuwa bara linalodhurika kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa kuliko mengine mengine kwa sababu ya umasikini mkubwa unaozikumba nchi nyingi za Kiafrika na kukosa uwezo wa kubadilika. Dalili za

mabadiliko ya hali ya hewa Afrika zimeshaonekana: mlipuko wa magonjwa na kuyeyuka kwa barafu milimani,kuongezeka kwa joto jangwani na maeneo mengine,kuongezeka kwa kina cha bahari na kuchubuka kwa marijani kandokando ya bahari. Yafuatayo yanaonesha baadhi ya matukio yanayoelekeana

**Cairo, Misri – Agosti yenye jot jingi zaidi katika kumbukumbu**

**1998**. Joto lilifikia41 °C (105.8 °F) Agosti 6, 1998.

**Afrika ya kusini- muongo wa joto jingi na ukame katika kumbukumbu , 1985–1995.** Wastani wa joto uliongezeka kwa kiasi cha

0.56 centigradi ukilinganisha na kalne iliyopita.

**Senegali-ongezeko la kina cha bahari**. ongezeko la kina cha bahari inasababisha kupotea kwa ardhi iliyopo ufukweni Rufisque katika pwani kusini mwa senegali.

**Kenya –katika mlima Kenya kiwango kikubwa cha barafu kinapotea**. Asilimia 92 ya barafu ya lewis imeyeyuka miaka mia moja iliyopita. Bahari- kupata joto kwa maji. Bahari imekuwa ikipata joto linalofikia nyuzi 0.06 centigradi kutoka usawa wa bahari hadi kina cha

3,000m kwa miaka 35-45 iliyopita . zaidi ya nusu ya ongezeko la joto imetokea juu zaidi ya m 300. Kupata joto kwa maji kunatokea katika mabonde yote ya bahari na sehemu zenye kina kirefu kulikoilivyofikiriwa kabla.

**Milima ya Ruwenzori-Uganda –**Kutoweka kwa barafu.Tangu miaka ya

1990 eneo lenye barafu limepungua kwa asilimia 75. katika bara la Afrika joto limeongezeka kwa kiwango cha 0.5 centigradi kwa karne iliyopita, na miaka mitano ya joto katika Afrika imetokea tangu mwaka 1988.

**Kenya-Mlipuko wa ugonjwa wa malaria, majira ya joto, 1997**

Mamia ya watu walikufa kutokana na malaria kwenye miinuko nchini

Kenya ambako watu hawakuwa na uelewa juu ya malaria.

**Tanzania – Malaria huongezeka milimani.**.Kiwango cha juu cha joto la mwaka katika milima ya Usambara kimehusianishwa na kuenea kwa malaria.

**Bahari ya hindi, Ghuba ya Persian, visiwa vya Shelisheli – Kuchubuka kwa mwamba wa marijani**. Inajumuisha Shelisheli; Kenya; Somalia;Madagaska ;Maldives;Indonesia;Sri-lanka; ghuba ya Tailend Visiwa vya Andamani;Malesia;Omani;India na Kambodia.

**Kenya-ukame mkali katika miaka 60, 2001**.Zaidi ya watu millioni nne waliathirika na upungufu mkubwa wa mavuno kudhoofika kwa mifugo na hali mbaya ya usafi.

**Ziwa Chadi-kupotea kwa ziwa.**.Sura ya eneo la ziwa imepungua

kutoka mita za mraba 9,650 (25,000 Kilometa za mraba) ndani ya mwaka

1963 hadi mita za mraba 521 (1,350 kilometa za mraba) kwa sasa. Mafunzo ya sasa yanaashiria upungufu mkubwa wa maji unatokana na muunganiko wa upungufu wa mvua na ongezeko la mahitaji ya maji kwa kilimo cha kumwagilia na mahitaji mengine ya binadamu.

**Afrika kusini –Uchomaji wa fukwe. Januari 2000**

Moja ya miezi ya kumi na mbili kame iliyo katika kumbukumbu, na joto zaidi ya sentigredi 40 ilichoma moto pwani ya magharibi mwa mkoa wa Cape. Kiasi kikubwa cha moto uliochomwa kilichochewa na uwepo wa aina mbalimbali za mimea vamizi, ambayo baadhi hutoa asilimia 300 zaidi ya joto ikichomwa ikilinganishwa na mimea asili.

*Imenukuliwa kutoka: Climate Hot Map, Website*

## Nyenzo 6: Barafu ya mlima Kilimanjaro

**Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi**

Kama baba yake kabla yake, Munyai alifanya kazi kama kiongozi katika mlima Kilimanjaro. Kila mwaka huongoza makundi mawili ya watalii mpaka kileleni. Amekuwa akifanya kazi hii kwa miaka mitano na hakumbuki ni mara ngapi amepanda mlima huo. Leo yuko kileleni, akizungumza na baadhi ya watalii wa Kiswisi kuhusu kupanda mlima na wameshafika kileleni. Mmoja anatoa maelezo ya kushangazwa na ukweli kuwa hakuna barafu juu ya mlima kwa sasa. Mnyai anagundua kuwa miaka miwili tu iliyopita barafu ya mlima Kilimanjaro imepotea na anashangaa kwanini. Anaporudi nyummbani anamwuliza baba yake kama anakumbuka kama kuna wakati kulikuwa hakuna barafu juu ya mlima. Jibu la baba yake ni la wazi-kuwa kulikuwa na barafu muda wote!

**Picha za barafu na theruji juu ya Mlima Kilimanjaro**

Mlima Kilimanjaro umekuwa ukijulikana 'Mlima unaong'ara'. Baadhi ya wanasayansi wanasema kilele cha Mlima Kilimanjaro kinaweza kising'are tena. Kwa mujibu wa profesa Lonnie Thompson wa Chuo Kikuu Ohio, theruji ya Mlima Kilimanjaro inaweza kupotea mwaka 2020. Katika makala yake ya tarehe 18 Oktoba jarida la sayansi, Thompson na waandishi wenzake waligundua kuwa theruji kileleni ambayo iliyokuwepo zaidi ya miaka 11000 iliyopita imepungua kwa asilimia 82% kwa karne iliyopita. Waandishi wametammbua kuwa kupungua kwa kasi kwa theruji kwa siku za karibuni ni kwa kushangaza ukizingatia uwezo wake wa kustahmili mabadiliko mengi ya hali ya hewa., ikijumuisha ukame mkubwa wa miaka 300 ambao uliathiri maisha ya watu walioishi kuzunguka eneo hilo yapata miaka 4000 iliyopita.

Picha zinaonesha mitazamo miwili kuhusu mlima Kilimanjaro, tarehe 17

Februari 1993(juu), na tarehe 21 Februari 2000 (chini). Picha hizi zilipigwa na kipimo cha satilaiti 5 na 7, moja-moja. Madhari yanaonesha uoto mkubwa (wa kijani) kuzunguka mlima, wakati uoto kwa wastani upo mbalimbali hadi urefu wa mita 5,895. rangi ya kahawia sehemu ya juu ya Mlima inaonesha mawe na ardhi tupu, kuonesha mifumo ya maji inayokatizana yatokanayo na mvua na kuyeyuka kwa barafu katika mlima Kilimanjaro.



*Chanzo: NASA Earth Observatory, Website*

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

# Sehemu ya 5: Kuwapeleleza watu wengine na maeneo

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kuwasaidia wanafunzi watambue uhusiano wa kufanana kwa watu tofauti na mahali tofauti?

**Maneno muhimu:** Utafiti, maeneo, mazingira

| Matokeo ya ujifunzaji |
|---|
| Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:<br>• Unatambua tofauti na kufanana katika muktadha/mazingira mbalimbali ya Africa;<br>• Utakuwa umetumia mbinu za kimawasiliano zinazohusu kufananisha jamii na matendo katika mazingira/ muktadha wowote;<br>• Kupanga kazi ya utafiti darasani kwa kutumia nyenzo mbalimbali. |

## Utangulizi

Unapofundisha masomo ya kijamii, muda wote unakutana na maswali ya utofauti na ukawaida/ufanano.

Sehemu hii imeangalia namna unavyoweza kuwasaidia wanafunzi wako kulinganisha maisha na matendo ya kiuchumi katika mazingira mbalimbali. Hii itasaidia kujenga uwezo muhimu wa kififkra katika taaluma ya maarifa ya jamii kwa wanafunzi wako na wewe mwenyewe.

## Somo la 1

Katika shule ya msingi wanafunzi wakubwa wanaweza kufanya kazi kwa wazo kuwa vitu katika makundi mawili tofauti vinaweza kuwa na sifa nyingi zinazovifanya kuwa sawa. Ni sehemu ya majukumu yako kuwasaidia wanafunzi wa umri mdogo kulijua hili.

Katika sehemu hii, unahimizwa kuwajengea wanafunzi wako wazo hili katika mahusiano kati ya ukawaida na utofauti walionao wanadamu. **Uchunguzi kifani 1** na **shughuli 1** vinapendekeza njia za kutumia makundi ya majadiliano kutambua aina tofauti za maisha ya watu katika maeneo mbalimbali, lakini pia kuwakumbusha wanafunzi kuwa watu wote kila mahali wanafanana kwa utu wao.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Uchunguzi kifani ya 1: Kutambua tofauti katika makazi

Bi. Maryogo anafundisha Jiografia katika shule ya kijijini nchini Tanzania. Wakazi wa kijiji hiki ni maskini sana. Bi Maryogo anataka kuwasaidia wanafunzi wake kujua tofauti zilizopo katika jamii, hivyo anawapa kazi zinazowachochea kutafakari kwa undani/kudadisi ili wagundue wenyewe ukweli juu ya dunia wanayoishi.

Leo, amepanga kwa umakini anachoweza kutarajia wanafunzi wake wa miaka 11 wafanye na ameandaa mlolongo wa picha zinazoakisi maisha katika jamii tofauti. (Angalia **nyenzo rejea 1: kuishi katika jamii tofauti).**

Katika majadiliano darasani, Bi Maryogo anatoa maswali yafutayo: Vitu/mambo gani ya maeneo haya yanafana?

Jinsi gani watu wanaoishi sehemu hizi wanafanana?

Kuna tofauti gani?

Kwa nini kuna tofauti hizi?

Wanafunzi wanapopendekeza majibu ya maswali haya, anawahimiza kupanua mawazo yao ili wafikiri kwa undani zaidi. Anaibua hisia zao juu ya wanavyohisi kuishi kijijini kwao **. (Pia angalia nyenzo rejea muhimu: kutumia maswali kuhamasisha kufikiri)**

## Shughuli ya 1: Tuko tofauti, tuko sawa.

Gawanya darasa lako katika makundi ya wanafunzi wanne au zaidi (kama itawezekena kuzalisha nakala chache za **nyenzo rejea 1** : basi makundi yako yatakuwa makubwa).

Lipe kila kundi matukio kuanzia **nyenzo rejea 1 -kusoma shule, kuogelea au kuhemea** –ili wazifanye kazi. Kila kundi liandae orodha ya mfano wa kila hali, na tofauti zilizopo. Tumia ushahidi uliopo kwenye picha tu.

Waambie kila kundi waandike sentensi zinazolinganisha hali hizo za kila mfano.

A: Sokoni bidhaa za chakula zimepangwa kwenye sinia la duara B: Dukani,watu husukuma bidhaa kwenye vigani vya kubebea Wanaweza kuzionyesha sentensi hizi na picha darasani ili waweze

kuona/angalia nini makundi tofauti yanasema juu ya picha.

Ukiangalia kwenye maonyesho yao utagundua namna walivyoelewa mada. Unaweza kutumia hili kupanga hatua inayofuata katika kujifunza kwao.

Kama una wanafunzi wa umri mdogo, unaweza kufanya kama shuguli ya darasa, kwa kutumia picha mbili zinazokinzana na kuwauliza wanafunzi ili kuwasaidia kuelekeza ugunduzu wao.

## Somo la 2

Kuwapa nafasi wanafunzi wako wapate habari juu ya hali tofauti kutawasaidia kuelewa tofauti kati ya jamii. **Uchunguzi kifani 2 na shughuli 2** vinaonyesha njia tofauti za kuwapanga wanafunzi na kutumia maswali kuruhusu fikra juu ya ufanano na tofauti.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kutumia maswali kulinganisha maeneo mbali mbali

Bi. Maryogo ameandaa somo juu ya kugundua tofauti na ufanano kati ya maeneo tofauti ya kienyeji. Ameandaa karatasi yenye maelekezo kati ya maeneo mawili tofauti ( **Angalia nyenzo rejea 2: Kulinganisha Magubike na Gairo)** . Mwanzoni mwa somo, anatoa karatasi na anawaambia wanafunzi wazifanyie kazi kwenye makundi yao.

Anaandika maswali yafutayo ubaoni;

Yapi yanafanana na yapi ni tofauti kati ya haya mazingira mawili (Magubike na Gairo)?

Je, Kuna viwango vya kufanana vya maisha kwa haya mazingira mawili? Wakati makundi haya yanafanya kazi Bi Maryogo anazunguka akisikiliza

mazungumzo yao na kuwaunga mkono kwa kutafakari kwa kina.

Anawauliza maswali kulingana na yale wanayosema wanafunzi ili awasaidie kufikiri, na anazingatia mawazo yao na mitazamo zao.

Bi Maryogo anahakikisha kila wakati kwamba amejipanga vizuri ili aweze kuangalia zaidi maendeleo ya uelewa wa wanafunzi wake.

## Shughuli ya 2: Kulinganisha mazingira mawili tofauti:

Shughuli hii inawapa fursa wanafunzi kutazama mazingira tofauti ya kijamii

Unaweza ktumia **nyenzo rejea 2** au kutengenza mazingira yako tofauti (labda kwa kutumia picha za magazeti) Lipe kila kundi picha mbili tofauti: ( **nyenzo rejea ya muhimu 2: kutumia kazi za makundi darasani kwako)** . Waambie waainishe sifa za kila mazingira kwa kuzingatia mambo kama sifa za kimazingira, shughuli za kiuchumi na kazi ambazo watu hufanya. Wanaweza kutofautisha picha na mahali wanapoishi. Waambie waandike sifa na mawazo muhimu kuhusu kipi ni tofauti na vipi vinafanana.

Weka makundi mawili pamoja na wambie kila kundi kushirikishana mawazo yao.

Liambie kila kundi kueleza walichotafiti darasani.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Somo la 3

Baada ya kutambua tofauti na kufanana kati ya eneo la kijiografia na darasa lako, hatua inayofuata ni kutumia mawazo haya kwa kuwahusisha wanafunzi wako kutafakari njia za kuboresha mazingira yao. **Uchunguzi kifani 3** unaonyesha namna mwalimu alivyotengeneza bustani ya shule kama sehemu ya masomo yake ya Sayansi na Maarifa ya Jamii; **Shughuli muhimu** huwasaidia wanafunzi kuchunguza jinsi mazingira yao yanavyoweza kuboreshwa.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kutengeneza mazingira ya shule

Bi Mgude anafundisha somo la Maarifa ya Jamii kwa wanafunzi wake wa darasa la 4 na la 5 kusini magharibi mwa Tanzania. Amekuwa akilinganisha mazingira ya sehemu mbalimbali akichunguza jinsi yanavyofana pia tofauti zake. Anataka wanafunzi wake watumie habari hizi kutafakari namna wanvyoweza kuboresha mazingira yao shuleni kwa njia endelevu (angalia **Nyenzo rejea 3: Elimu kwa maendeleo endelevu).**

Baada ya majadiliano ya kutosha, wanafunzi wake waliamua kua wangependelea kuandaa maeneo ya kukaa kwenye bustani na pia kupaka rangi kwenye uwanja wa michezo au kutengeneza michezo ya kucheza wakati wa mapumziko. Aliwaruhusu wanafunzi kujadii kwenye makundi yao. Walihitaji kufikiri juu ya:

Pa kuweka viti;

Watavitengeneza kutokana na nini; Kupata ruhusa toka kwa mwalimu mkuu;

Kuwahusisha wazazi na wajumbe wengine katika jamii; Michezo gani wanayopenda;

Wakiwa pamoja awalipanga ratiba ya kazi iliyobandikwa ukutani. Mwalimu

mkuu aliomba kuhudhuria na kusikiliza mawazo yao.

## Shughuli muhimu: Kuboresha mazingira.

Waulize wanafunzi wako wanapenda nini kwenye jamii yao na mazingira yao, kisha viorodheshe ubaoni.

Halafu waambie watafute njia za kuboresha mazingira ya shule yao

Waulize maswali haya mawili ili kuwafanya waanze kuongea Utafanyaje mazingira ya shule yavutie wakati wa michezo? Utamhamasishaje kila mtu ili ajivunie na kulinda shule?

Kila kundi litakapokuwa linatoa mawazo, orodhesha mawili ambayo ni maarufu ubaoni.

Wakati ambao kila kundi limetoa marejesho, pitia kila pendekezo kwa kutoa ufupisho wa kila suala.

Waambie wanafunzi wako (mmoja mmoja au kama kundi) kutengeneza mpango wa chaguo lao la namna ya kuborehsa mazingira, na kuubandika ukutani.

## Nyenzo-rejea ya 1: Kuishi kwenye jamii tofauti

**Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi**

<table>
<tr><th>Mjini</th><th>Kijijini</th></tr>
<tr><td><br>Imerekebishwa kutoka chanzo halisi: Jesuit Missions, Website</td><td><br>Imerekebishwa kutoka chanzo halisi: SOS Childrens Village, Website</td></tr>
<tr><td colspan="2"><br>Imerekebishwa kutoka chanzo halisi: Istafrica, Website</td></tr>
<tr><td><br>Imerekebishwa kutoka chanzo halisi: Zambeef, Website</td><td><br>Imerekebishwa kutoka chanzo halisi: Volunteer New Zealand, Website</td></tr>
</table>

## Nyenzo-rejea 2: Ulinganifu wa Magubike na Gairo

**Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi**

Kijiji cha Mugaboke kinapatikana kilomita 5 kwenye barabara ya Morogoro

– Dodoma katika wilaya ya Kilosa ya Tanzania. Pamoja na kupata mvua ya uhakika na kutosha mwaka mzima, kijiji kimejaa chemchem .Wakazi wa kijiji cha Mugaboke ni wakulima mchanganyiko. Wanazalisha mazao mbalimbali yakiwemo mahindi, viazi mviringo, ndizi na mboga za majani kama vile vitunguu, nyanya ,n.k .Pia wanafuga kuku, mbuzi na mifugo midogo midogo

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Ingawa kimejaliwa rasilimali za asili za kutosha bado wakazi wa Mugaboke wana kiwango cha chini cha maisha. Wanapata bei ndogo kwa mazao yao ya kilimo, kwa vile wafanyabiashara hujihusisha na mkulima mmoja mmoja, badala ya kujihususha na vyama vya ushirika vya wazalishaji ambavyo wananchi walijaribu kuunda kwa kupitia wakala wa wafanyabiashara wadogo wa Agakhan. Kutokana na kutokuwa na uwezo wa kulifikia soko, wanakijiji wanaweza kupata mahitaji ya msingi tu. Hawana uwezo wa kuzalisha rasilimali za kifedha ili kupambana na majukumu mengine ya kijamii kama vile vifaa vya kiafya, shule, maji ya bomba, nyumba za kisasa, umeme n.k

Gairo ni kituo cha kibiashara kwenye barabra kuu ya Morogoro - Dodoma. Kwa sababu ya kuwa kwenye njia ya usafiri ya kibiashara, wakazi wake kihistoria wameweza kujenga mawasiliano na miji mikubwa kupitia madereva wa malori. Pia wanajenga mtandao miongoni mwa madereva wa malori makubwa na wasafirishaji wengine, kunakowawezesha kusafirisha bidhaa zao kwa bei ndogo. Wakazi wengi wa Gairo ni wafanyabiashara. Wananunua mazao ya kilimo pamoja na kuku, mbuzi kutoka kwenye vijiji jirani kwa bei ndogo, na kuviuza kwa bei ya juu kwenye miji mikubwa kama vile Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam. Matokeo yake, wakazi wa Gairo wanaishi maisha ya kiwango cha juu ukilinganisha na watu wa vijiji vinavyowazunguka. Gairo ina huduma za kijamii kama vile zahanati, shule, umeme na maji ya bomba.

## Nyenzo-rejea 3: Elimu kwa maendeleo Endelevu (EME)

**Taarifa za msingi/ ujuzi wa mada kwa mwalimu**

**Elimu kwa maendeleo endelevu ni nini?**

‘Elimu kwa maendeleo endelevu inawezesha watu kujenga ufahamu, taratibu za maisha/maadili na ujuzi wa kushiriki kwenye maamuzi juu ya njia za kufanya mambo, mmoja mmoja au kwa pamoja, kitaifa na kimataifa, kuinua ubora wa maisha ya sasa bila kuharibu sayari kwa ajili ya siku zijazo?

**(Kongamano la Elimu kwa Maendeleo Endelevu, 14 Septemba 1998).**

Maendeleo endelevu ni sehemu muhimu ya uraia itakayowawezesha wanafunzi waweze:

- Kufahamu kwamba pamoja na tofauti za kimaumbile, kivifaa na kiutamaduni kuna mengi yanayotuunganisha na dunia.
- Kufikiri kwa makini na kuhoji kutokuwepo kwa haki na usawa;
- Kuainisha, kuheshimu na kuthamini upana na mawazo anuwai;
- Kujenga uhusika wa uwajibikaji kwenye masuala yanayohusu mazingira na maendeleo endelevu;
- Kuwa tayari kwa matendo yao kuifanya dunia iwe mahali endelevu na penye usawa.
- Kuwajibika kwa matendo yao.

Vyote, uraia na elimu ya maendeleo endelevu vinatoa fursa kubwa kwa namna nzuri ya kujifunza inayomlenga mwanafunzi ambayo mwanafunzi anapata hisia za kuwajibika kama raia wa dunia nzima. Mbinu hii ya kujifunza inajumuisha masomo yanoyochanganua sehemu mbali mbali za dunia na masuala yahusuyo mazingira. Kuchambua jamii zao na jamii nyingine za mbali kutawasaidia wanafunzi kupanua fikra zao kuhusu jinsi jamii na tamaduni tofauti zinavyokuwa; na jinsi tatizo linavyoweza kutatuliwa kwa njia nyingi tofauti; pia kupata mawazo mapya ya kupima na kujaribu. Elimu kwa maendeleo endelevu (EME) pia inaibua njia za kujitegemea zaidi. Hii inamaanisha kuwa unaweza kutumia vizuri rasilimali zinazokuzunguka lakini sio kuzitumia na kuzimaliza. Kufikiri njia za kurudishia au kupanda kutahakikisha uendelevu. Inamaanisha kutumia kile unachohitaji tu.

Rasilimali za kawaida si kwamba haziishi bali zina kikomo labda tujaribu kushirikiana na kuzitumia kwa busara na kuzirudishashia tunazotumia pale inapowezekana.

*Imerekebishwa kutoka chanzo halisi: BBC World, Website*

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

TESSA

Teacher Education in Sub-Saharan Africa

www.tessafrica.net

Rasilimali za Msingi

# Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa

## **Namba ya moduli 2** Utafiti wa Kihistoria

**Sehemu ya 1** Utafiti wa historia ya familia

**Sehemu ya 2** Kutafiti namna tulivyoishi zamani

**Sehemu ya 3** Kutumia njia tofauti za ushahidi katika historia

**Sehemu ya 4** Ufahamu wa Chati ya kalenda ya matukio

**Sehemu ya 5** Kutumia kazi za sanaa kujifunza mambo ya kale

KISWAHILI

*TESSA (Teacher Education in Sub-Saharan Africa) inalenga kuboresha utekelezaji darasani wa walimu wa msingi na walimu wa sayansi wa sekondari barani Afrika kupitia matoleo ya Rasilimali Huria za Elimu (OERs) ili kuunga mkono walimu kuunda njia zinazowalenga wanafunzi na kuwashirikisha. OER ya TESSA huwapa walimu kitabu cha kurejea pamoja na vitabu vya shule. Zinatoa shughuli kwa walimu kujaribu madarasani pamoja na wanafunzi wao, pamoja na masomo ya utafiti inayoonyesha jinsi walimu wengine wamefunza mada hiyo, na rasilimali husishi za kuwaunga mkono walimu katika kukuza mipango ya masomo yao na ufahamu wa somo.*

OER ya TESSA imeandikwa kwa ushirikiano wa waandishi wafrika pamoja na wa kimataifa *ili kushughulikia mtalaa na muktadha. Zinapatikana kwa matumizi ya mtandaoni na chapa (*http://www.tessafrica.net*). OER Msingi zinapatikana katika matoleona lugha kadhaa (Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu na Kiswahili). Mara ya kwanza, OER ilitolewa kwa Kiingereza na kupatikana Afrika nzima. OER hizi zimebadilishwa na washirika wa TESSA ili kufaa Ghana, Nijeria, Zambia, Rwanda, Uganda, Kenya, Tanzania na Afrika Kusini, na kutafsiriwa na washirika nchini Sudani (Kiarabu), togo (Kifaransa) na Tanzania (Kiswahili) OER ya Sayansi ya Sekondari zinapatikana kwa Kiingereza na zimebadilishwa ili kufaa Zambia, Kenya, Uganda na Tanzania. Tunakaribisha maoni kutoka kwa wale wanaosoma na kutumia rasilimali hizi. Leseni ya uundaji wa ubunifu huwawezesha watumiaji kuchukua na kujanibisha OER zaidi ili kutimiza mahitaji na muktadha wa kindani.*

*TESSA inaongozwa na Open University, Uingereza, na inafadhiliwa kwa sasa na ruzuku za ufadhili kutoka kwa Wakfu wa Allan and Nesta Ferguson, Wakfu wa William and Flora Hewlett na Open University Alumni. Orodha kamili ya wafadhili inapatikana kwenye tovuti ya TESSA (*http://www.tessafrica.net*).*

*Pamoja na rasilimali kuu za mafundisho za kuunga mkono mafunzo katika masomo maalum, ni chaguo za rasilimali za ziada ikiwa ni pamoja na sauti, rasilimali kuu ambazo zinafafanua utendakazi, vitabu na zana maalum.*

**TESSA Programme**
**The Open University**
**Walton Hall**
**Milton Keynes, MK7 6AA**
**United Kingdom**

**tessa@open.ac.uk**

Copyright © 2017 The Open University
Except for third party materials and otherwise stated, this content is made available under a Creative Commons Attribution-Share Alike 4.0 licence: http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0/. Every effort has been made to contact copyright holders. We will be pleased to include any necessary acknowledgement at the first opportunity.

***TESSA_SwPA_SCI_M2 August 2017***

*This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Share Alike 4.0 License*

# Contents


Sehemu ya 1: Utafiti wa historia ya familia 5
Somo la 1 5
Somo la 2 7
Somo la 3 8
Nyenzo-rejea ya 1: Jedwali la mahusiano/ukoo 10
Nyenzo-rejea 2: Jedwali jingine la ukoo 10
Nyenzo-rejea 3: Kalenda ya matukio yangu 11
Sehemu ya 2: Kutafiti namna tulivyoishi zamani 12
Somo la 1 12
Somo la 2 14
Somo la 3 15
Nyenzo-rejea ya 1: Historia simulizi 16
Nyenzo-rejea ya 2: Maswali yanayoweza kutumika kwenye mahojiano 17
Nyenzo-rejea ya 3: Uhuru wa Tanzania 18
Sehemu ya 3: Kutumia njia tofauti za ushahidi katika historia 20
Somo la 1 20
Somo la 2 22
Somo la 3 23
Nyenzo-rejea ya 1: Zimbabwe kuu 24
Nyenzo-rejea ya 2: Ramani ya picha ya Zimbabwe kuu 25
Nyenzo-rejea ya 3: Ufahamu juu ya ufugaji ngo’mbe 26
Nyenzo-rejea ya 4: Ng’ombe na utamaduni wa maisha ya Wamasai 26
Nyenzo-rejea ya 5: Umuhimu wa ng’ombe-zamani na sasa 27
Sehemu ya 4: Ufahamu wa Chati ya kalenda ya matukio 28
Somo la 1 28
Somo la 2 30
Somo la 3 31
Nyenzo-rejea ya 1: Zimbabwe kuu 32
Nyenzo 2: Jedwali la Kalenda ya matukio ya Kiafrika 33
Nyenzo-rejea ya 3: Matukio muhimu kuelekea uhuru 34


Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Sehemu ya 5: Kutumia kazi za sanaa kujifunza mambo ya kale 40
Somo la 1 40
Somo la 2 42
Somo la 3 43
Nyenzo-rejea ya 1: Matumizi ya kazi za sanaa darasani 44
Nyenzo-rejea ya 2: Sanaa zangu 47

# Sehemu ya 1: Utafiti wa historia ya familia

**Swali Lengwa muhimu:** Namna gani unaweza kupanga shughuli vikundi vidogo vidogo darasani kukuza ufanyaji kazi pamoja na kujenga kujiamini?

**Maneno muhimu:** familia: historia: kujiamini: utafiti: kundi dogo la kazi: majadiliano.

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- umepanga kazi zako kusaidia wanafunza kujielewa wenyewe na uhusiano wao na familia nyingine;
- umetumia makundi madogo ya majadiliano kujenga kujiamini wanafunzi wakiwa wanatafiti historia za familia zao.

## Utangulizi

Ufundishaji mzuri huanza kwa kuwahamasisha wanafunzi kutafiti mambo ambayo wanayafahamu.Kihistoria, hii ina maana kutumia maisha yao na ya familia zao kama chanzo cha utafiti. Ujuzi uliotumika kutafiti historia ya familia, unaweza kutumika kutafiti masuala mapana zaidi ya kihistoria.

Sisi wote tuna historia,iliyoanza mara baada ya kuzaliwa.Hii inajumuisha uzoefu wetu na watu wote tunaohusiana nao.

Katika sehemu hii,unaanza kutafiti hali za familia za wanafunzi wako, kazi na majukumu yao katika famlilia zao. Utaangalia pia kwa upana familia kubwazenye misingi ya kiukoo. Kadili unavyotafiti sehemu hii unatakiwa kuwa makini na uzoefu tofauti wa familia au miundo mingine ambayo wanafunzi wako wanaiishi.

## Somo la 1

Uanapotafiti familia ni muhimu kujua kwanza uelewa wa wanafunzi juu ya maana familia na kuwaonesha mipangilio tofauti ya familia. Kujua utofauti huu kunawasaidia wanafunzi kujisikia vizuri wanapotambua namna ambavyo familia zinaweza kutofautiana. **Uchunguzi kifani 1** na **shunguli 1** tunangali njia mbali mbali za kufanya hili.

Katika **Uchunguzi kifani**,mwalimu huwahamasisha wanafunzi kufanya kazi katika makundi madogo (rejea **nyenzo muhimu: Utumiaji wa kazi za makundi katika darasa lako**) na kukumbuka sheria walizokubaliana kufuata kwenye majadiliano ya vikundi.

## Uchunguzi kifani ya 1: Kutumia kundi dogo kutafiti familia yangu

Bwana Nguzo, mwalimu wa Maarifa ya Jamii katika shule ya msingi Muhimu Tanzania alitaka wanafunzi wake wa darasa la tatu kujifunza kuhusu familia na kazi za familia mbalimbali.

Aliunda makundi ya wanafunzi wasiozidi sita. Aliwaweka wanafunzi pamoja ambao sio kawaida yao kufanya kazi pamoja.

Katika makundi wanafunzi walijibu maswali yafuatayo,ambayo ambayo mwalimu aliaandika ubaoni:

Jina lako nani?

Baba na mama yako ni nani? Taja majina yao

Babu na bibi yako ni nani? Taja majina yao

Una dada na kaka wangapi? Taja majina yao. Ni wakubwa au wadogo kuliko wewe?

Una binamu wangapi? Taja majina yao

Wakati wa majadiliano,Bwana Nguzo alikwenda kila kundi kuahakikisha kuwa wanafunzi wote walipewa nafasi ya kutoa mawazo. Baaada ya dakika

10 hadi 15,aliyataka makundi kushirikishana na darasa nini wametafiti kuhusu familia mbalimbali. Nini mfanano kati ya familia hizo? Nini totauti?(kwa wanafunzi wadogo au wasiojiamini huwauliza maswali zaidi, mfano: Nani alikuwa na kaka wengi?)

Pia aliyataka makundi kuzingatia swali hili.

Nini kinamfanya mtu awe dada ,kaka shangazi yako,n.k?

Baada ya dakika 10,mwanafunzi mmoja kutoka kila kundi huwasilisha majibu ya maswali la 6 darasani. Nguzo huandaa jedwali kubwa la mahusiano kusaidia kuongoza mjadala (Angalia Nyenzo rejea 1 jedwali la uhusiano )

Bwana Nguzo na wanafunzi wanajua kuwa ingawa kuna maneno katika lugha zao yanayoelezea kuhusu binamu, baba mdogo/mkubwa na mama mdogo/mkubwa, mahusiano haya kwa kawaida hujulikana kama, kaka au dada, baba na mama. Kunautofauti kati ya kaka wa baba na kaka wa mama pia dada wa mama na dada wa baba. Mfano: Kaka wa mama ni mjomba lakini kaka wa baba ni baba mdogo/mkubwa; dada wa baba ni Shangazi lakini dada wa mama ni mama mdogo/mkubwa. Mwalimu Nguzo anagundua kwamba kufundisha wanafunzi kuhusu uhusiano wa kifamilia unaweza kuwachanganya wanafunzi wadogo.

## Shughuli ya 1: Mimi ni nani?

Kabla ya kipindi, andaa jedwali la mahusiano (angalia **Nyenzo rejea 1** )

Watake wanafunzi kufanya kazi katika makundi ya watatu au wane. Mwanafunzi mmoja ajitolee kuorodhesha watu wote anaowafahamu katika familia yake na kujaza habari zao kwenye jedwali la mahusiano (unaweza kumchagua mwanafunzi wewe mwenyewe)

Wanafunzi wanaweza kuhitaji kuchora picha za ndugu zao kwenye jedwali

Shirikishana majedwali haya na darasa lote

Jadili utofauti katika familia na sisitiza jinsi utofauti huo ulivyo mzuri

Mwishoni mwa kipindi, onesha jedwali la uhusiano kwenye ukuta wa darasa

## Somo la 2

Tunapo jifunza mambo ya kale, ni muhimu kusaidia wanafunzi kuelewa kupita kwa wakati na jinsi vitu vinavyobadilika kutoka kizazi hadi kizazi.

Kubuni njia ambazo wanafunzi wanazitumia kujifunza historia za familia zao kunawasaidia kuhusianisha matukio pamoja na kuyaweka kwenye mtiririko mzuri. **Nyenzo rejea 2: jedwali jingine la uhusiano** linaonesha ukoo ambao utawasaidia wanafunzi kuona uhusiano kati ya wanafamilia mfano binamu yao ni mtoto wa dada au kaka wa mama au baba yao,

## Uchunguzi kifani ya 2: Historia za familia

Juma Bhalo anapanga kufundisha wanafunzi wa darasa la tano kuhusu uhusiano wa kifamilia kwa kipindi fulani

Anakakata vipande kadhaa vya picha kutoka kwenye magazeti ya watu wa nyakati tofauti, wakifanya shughuli tofaut,:i mfano harusi, siku ya bonanza la shule, na kuandika namba nyuma ya kila picha. Aliwaambia wanafunzi wake kuwa picha zinawakilisha matukio tofauti kwa maisha ya mtu mmoja na kuwataka wanafunzi katika makundi ya watu sita kupanga picha kulingana na umri wake. Anawapa dakikia 15 kujadili mpangilio wao.

Halafu anawataka kila kundi kutoa mrejesho. Anawataka kueleza kwa nini walichagua mpangilio fulani na kuandika dondoo za picha zilizo wasaidia kupanga matukio. Wanajadiliana matukio muhimu yaliyoonyeshwa kwenye picha na Mwalimu Juma anawaambia wametengeneza kalenda ya matukio ya maisha.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Shughuli ya 2: Wanafunzi watengeneze kalenda zao za matukio

**Nyenzo rejea 3: Kalenda yangu** inaweza kuwa mwanzo kwa darasa kutengeneza kalenda yao ya matukio.

Kwanza, jadili umuhimu wa kujijua asili yako na wanafamilia wengine

Elezea maana ya kalenda ya matukio

Onyesha mfano kwa kutengeneza kalenda ya matukio yako mwenyewe (sio lazima utumie maisha yako halisi-unaweza ukatumia uhalisia wa maisha ya mtu fulani unaye mfahamu). Kuonyesha mfano ni njia muafaka ya kuwasaidia wanafunzi

kujifunza ujuzi mpya. Chora kalenda hii ubaoni waone na zungumzia nini unafanya au uwe umeiandaa kwenye karatasi kubwa. Kumbuka kutumia vipimo sahihi- mwaka uwakilishe na umbali fulani. (wanafunzi wako wanapotengeneza kalenda zao, watumie sentimeta za mraba 5 au umbali wa mkono kama hawana rula.

Watake wanafunzi kuandika vitu muhimu wanavyokummbuka kuhusu maisha yao. Pia wape muda wa kuwauliza wazazi/walezi kuhusu walipotembea kwa mara ya kwanza n.k.

Watake kunakiri taarifa yoyote wanayohitaji kuiweka katika kalenda ya matukio

Wasaidie wakati wanatengeneza kalenda zao. Unaweza kuwahamasisha kuandika matukio makubwa ambayo yamewatokea, na katika rangi tofauti.( au katika mabano chini ya mstari) matukio makubwa ambayo yalitokea katika familia zao( mfano dada mkubwa kwenda chuo, baba kununua shamba n.k)

Onyesha kalenda zao darasani

Wanafunzi wanaomaliza mapema wanaweza kuombwa kufikiri na kuchora kalenda ya muda ujao. Nini yatakuwa matukio makubwa wakati wana umri wa miaka 20,25,40 n.k?

## Somo la 3

Kusaidia wanafunzi kukuza ufahamu wao wa mambo ya zamani na sasa kunachukua muda, na inahusisha kuwapa kazi mbalimbali ambapo wanatakiwa kuona, kuuliza maswali na kufanya maamuzi kuhusu kile wanacho chunguza.

Wanawezaje kukuza ujuzi kuwasaidia kufikiri kuhusu namna vitu vinavyobadilika kulingana na muda? **Uchunguzi kifani 3** na shughuli muhimu unatumia mazingira ya kawaida kupanua ufahamu wa wanafunzi wako kuhusu muda unaopita na vitu vinavyobadilika.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kutembelea mzee wa mahali

Mbwana Kato, Bibi Sime na Dada Benda waliandaa pamoja mafunzo ya jamii. Hawakufundisha wote mada moja kwa wakati mmoja, lakini iliwasaidia kushirikishana mawazo.

Wote walisoma **Nyenzo muhimu: matumizi ya mazingira ya jamii/ mahali kama nyenzo.** Walipanga kwenda pamoja na wanafunzi kutembelea wazee katika jamii kuongea nao kuhusu namna kijiji kilivyobadilika tangu walipokuwa watoto. Waliamua kugawa darasa katika makundi na kila kundi lingeandaa maswali ya kumuuliza mzee. Kila kundi lingeuliza maswali kwenye eneo tofauti kama michezo waliyocheza, chakula walicho kula,nyumba walizoishi n.k.

## Shughuli muhimu: Matumizi ya vyanzo mbalimbali kuchunguza maisha ya zamani

Wape wanafunzi nafasi ya kutoa mawazo yao. Watake kufikiria jinsi wanavyoweza kuchunguza namna maisha yalivyobadilika katika familia zao, kijijini au katika jamii kwa kipindi fulani. Wangetumia nyenzo gani kuchunguza hilo?

Wanaweza kuwa na mawazo kama: kutumia uchunguzi na kumbukumbu zao kufikiri kuhusu nini kimebadilika katika maisha yao; kuuliza wazazi wao; kuzungumza na wazee wengine; kuongea na watu wenye mamlaka ( kama wafalme); kuangalia ramani za zamani; kutumia makumbusho (kama yapo); kusoma vitabu vinavyohusu eneo husika n.k.

Watake wanafunzi kukusanya hadithi kutoka kwenye familia zao kuhusu namna maisha yalivyobadilika kwa vizazi vichache vilivyopita, namna maisha ya kila siku yalivyokuwa. Zipi ni hadithi za zamani za familia zao? Je familia inachapisho lolote? Picha, barua.n.k zinazovyoonesha maisha yalikuwaje?


Wanafunzi washirikishane hadithi zao kwa kila mmoja darasani na tumia hadithi zao kama msingi wa mawasilisho –hii itajumuisha picha zinazoonyesha maisha yalivvokuwa,kazi zilizofanyika kwa maisha ya zamani maandishi yanayohusu hadithi za familia na nyaraka nyingine.na hadithi za kufikirika mfano: elezea siku moja katika maisha ya bibi yako wakati akiwa kijana.

# Nyenzo-rejea ya 1: Jedwali la mahusiano/ukoo

**Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi**


Jedwali la ukoo linaonyesha kila mtu anavyohusiana na wengine na wanafamilia au jamii. Tamaduni tofauti zina namna tofauti za kuelezea uhusiano wao.

Lifuatalo ni jedwali la mahusiano ya ukoo kwa Tanzania.




# Nyenzo-rejea 2: Jedwali jingine la ukoo

**Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi**



# Nyenzo-rejea 3: Kalenda ya matukio yangu

## Nyenzo za mwalimu kwa kuandaa au kubadili kwa matumizi ya wanafunzi

| Tarehe | 1988 | 1989 | 1990 | 1991 | 1992 | 1993 | 1994 | 1995 | 1996 | 1997 | 1998 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Matukio | Kuzaliwa | Hatua ya kwanza | Maneno ya kwanza | Kumbukumbu ya mwanzo | Kuzaliwa kwa dada | | Kuanza shule | Alienda zahanati kwa matibabu | | Kuzaliwa kwa kaka | |
| Mwaka | 0 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

# Sehemu ya 2: Kutafiti namna tulivyoishi zamani

**Swali Lengwa muhimu:** Je, namna gani unaweza kukuza ujuzi wa kufikiri katika historia kwa wanafunzi?

**Maneno muhimu:** ushahidi: historia: ujuzi wa kufikiri: mahojiano: maswali,:uchunguzi

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- Umetumia mapokeo na nyaraka,kukuza ujuzi wa kufikiri wa wanafunzi wako katika historia;
- Umepanga na kufanya shughuli zinazo saidia wanafunzi kukusanya na kutumia ushahidi wa mapokeo kutafiti kuhusu matukio ya yaliyopita.

## Utangulizi

Tunaposoma historia kama sehemu ya mafunzo ya jamii, tunaweka msisitizo katika vyanzo vya ushahidi vinavyoweza kutufundisha mambo ya kale.

Kuna njia kuu mbili za kupata ushahidi wa kale-kutafuta na kuchanganua nyaraka ambazo huweka kumbukumbu ya kile kilichotokea na kutumia mapokeo. Mapokeo ni makusanyo ya hadithi za watu kuhusu tukio fulani.

Katika sehemu hii, utahamasisha wanafunzi wako kutafiti nyaraka na kufanya mahojiano kwa lengo la kujenga uelewa wa kule walikotoka. Ni muhimu kuhamasisha wanafunzi kuuliza maswali na kusikiliza mawazo ya wenzao; hivyo wanakuza ujuzi katika kupembua ushahidi na kupata picha halisi.

## Somo la 1

Kufundisha historia sio tu kunahusisha ukweli juu ya matukio ya kihistoria bali pia maendeleo ya ujuzi wa wanafunzi katika nyanja ya historia. Kama mwalimu, unatakiwa kuwapa wanafunzi wako nafasi ya kukuza na kufanyia mazoezi ujuzi huu. Aina ya matukio unayotafiti na wanafunzi wako yatategemea umri wao. Kwa watoto wadogo, utatoa mwongozo zaidi katika kuwasaidia kutafuta na kuelewa nini kilitokea.

Katika sehemu hii, wanafunzi watafanya mahojiano pamoja na waliowazidi umri katika familia zao au yeyote katika jamii. Lengo la mahojiano ni kutafuta namna wanavyotofautiana kimaisha, ukilinganisha na watu wa kale. Kwa kuwaonyesha wanafunzi namna ya kufanya mahojiano, unaweza saidia kukuza ujuzi muhimu-kuwa tayari kuona thamani ya historia simulizi na kuwa tayari kusikiliza. (**Rejea nyenzo 1: Historia simulizi**; kufahamu zaidi juu ya nyenzo hii muhimu)

**Uchunguzi kifani 1** unaonesha namna mwalimu mmoja alivyowaelekeza wanafunzi wake wazo la kutumia historia simulizi kutafiti juu ya mambo ya kale. Soma hii na wanafunzi wako kabla ya kujaribu **shughuli 1**.

## Uchunguzi kifani ya 1: Historia simulizi za familia

Kila mtu anahistoria yake. Bibi Eunice Shikongo, mwalimu wa darasa la tano katika shule ya Sheetheni nje ya Windhoek Namibia, hutaka wanafunzi wake kutafiti historia za familia zao kwa kumhoji mmoja wa wanafamilia.

Kwanza, hujadili maana ya ushahidi wa mapokeo kwa kuwahamasisha wanafunzi kushirikishana vitu walivyojifunza kutoka kwa wazazi wao. Huwauliza: Je, kile mlichojifunza kimeandikwa? Wengi wanakubali kuwa vitu walivyojifunza kwa njia hii havijaandikwa, lakini wameyapata kwa njia ya mdomo. Bibi Shikongo kisha huelezea kwamba, kwa kufanya mahojiano, wanafunzi watakusanya ushahidi wa mapokeo kuhusu zamani ilivyokuwa na watajua jinsi chanzo hiki kinavyoweza kuwa muhimu kuelezea mambo ya kale.

Huwasaidia kukusanya maswali muhimu watakayotumia kuwahoji wanafamilia zao (Angalia Nyenzo rejea 2: maswali yanayoweza kutumika katika mahojiano ). Halafu wanafunzi huongeza maswali yao kabla yakufanya mahojiano majumbani kwao.

Siku inayofuata, wanashirikishana matokeo ya utafiti na wanafunzi wenzao. Bibi Shikongo uandika muhtasari wa utafiti wao kwenye ubao kwa kichwa cha habari 'Kale'. halafu, huwataka kujibu maswali yaleyale kuhusu maisha yao, na kuandika muhtasari wa maelezo yao chini ya kichwa cha habari cha habari, 'Sasa'.

Huwataka kufikiri kuhusu namna maisha yao yanavyotofautiana na ya ndugu zao wa zamani. Halafu huwataka wanafunzi wawili wawili, kulinganisha Kale' na 'Sasa'

Wanafunzi wa umri mdogo huandika sentensi mbili/tatu kwa kutumia maneno ya ubaoni. Wanafunzi wakubwa huandika aya fupi.

## Shughuli ya 1: Mahojiano ya ana kwa ana kuhusu utoto

Kwanza panga wanafunzi wawili wawili. Halafu, waambie wafikirie baadhi ya maswali wanayoweza kuuliza watu wazima kuhusu utoto wao. Wape wanafunzi muda wa kufikiri juu ya maswali yao na waambie muda watakaotumia katika zoezi

hili-yaweza kuwa siku mbili au tatu. Kama una wanafunzi wa umri mdogo, mnaweza kufanya pamoja kutengeneza maswali matatu au manne ambayo watakumbuka na kuweza kuuliza nyumbani.

Wakisha uliza maswali nyumbani, watake wanafunzi kushirikishana mawazo na wenzao.

Halafu, watake kila kundi la wanafunzi wawili kuungana na kundi lingine ili kushirikishana kile walichokipata.

Sasa waulize kila kundi la wanafunzi wanne kumalizia jedwali kuonyesha jinsi maisha yanavyoweza kubadilika.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

| Mtu wa makamo/zamani | mimi |
|---|---|
| Ningeenda sokoni kwa punda | Naenda sokoni kwa basi. |
| | |
| | |

Jadili na darasa lote namna maisha yalivyobadilika tangu wazazi wao na/au babu au watu wengine wa zamani walipokuwa watoto.

Uliza maswali yanayo wahamasisha kufikiri kwa nini mabadiliko haya yametokea. (**Nyenzo muhimu: matumizi ya maswali kusaidia kufikiri** inaweza kusaidia kufikiri aina gani ya maswali unahitaji kuuliza kuwahamasisha wanafunzi. Unaweza kuandika haya kabla ya kipindi kukukumbusha katika hatua hii.)

Tengeneza orodha ya mabadiliko ubaoni

## Somo la 2

Kama ulivyoweza kutumia historia simulizi kujua maisha ya kale, unaweza pia pamoja na wanafunzi wako kutumia kumbukumbu zilizoandikwa

Katika sehemu hii, tunaangalia namna jozi tofauti za kumbkumbu zinavyoweza kusaidia kujenga uelewa wao wa mambo ya kale. Katika **shughuli 2** na **shughuli muhimu**, wanafunzi hutafiti kumbukumbu zilizoandikwa juu ya mambo ya kale na kufanya mahojiano ya ana kwa ana na wanajamii. Namna unavyoweza kutunga na kukusanya pamoja nyenzo ni sehemu ya jukumu lako. Ushauri unavyoweza kufanya kazi hii umetolewa.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kutumia nyaraka kutafiti matukio yaliyopita

Bwana Murungi ni mwalimu wa darasa la 6 katika Shule ya msingi Mkiwa, sehemu ya Marangu,

Tanzania. Siku ya kuhadhimisha uhuru wa Tanzania inakaribia na anataka wanafunzi wake kufikiri kuhusu historia ya Tanzania.

Alipeleka darasa lake maktaba ambako walisoma kuhusu matukio. Magazeti mawili, *The Daily News na The Express*, yamekwisha kuchapisha kuhusu uhuru na huwasomea wanafunzi sehemu ya machapisho kuamsha ari ya kutaka kujua. Vitinyi hivi vina historia ya maisha ya baadhi ya watu husika. Aligawa darasa lake katika makundi na kuwataka kila kundi kuchukua mmoja kati ya watu hawa na kujifunza habari zake,halafu kuandika historia ya yule mtu katika bango, kwa maonyesho katika ukumbi wa shule. Bango lazima lijumuishe namna walivyojihusisha na nini kimewatokea.

Wanafunzi wa Bwana Mrungi kisha walipanga kuonyesha matokeo ya utafiti wao kwa shule nzima. Mabango yao yalibandikwa kuzunguka ukumbi na baadhi ya wanafunzi walisimulia kwenye mkusanyiko wa shule nzima.

**Nyenzo rejea 3: Uhuru wa Tanzania** inatoa taarifa za msingi

## Shughuli ya 2: Kujifunza tarehe muhimu katika historia

Shughuli hii inategemea kutembelea sehemu za makumbusho, yaani makumbusho ya kitaifa ya Dares Salaam, lakini unaweza kutumia sehemu nyingine. (kama haiwezekani kutembelea makumbusho, unaweza kukusanya pamoja baadhi ya machapisho kwenye magazeti, picha na vitabu kusaidia wanafunzi wako kujitafutia wenyewe kuhusu tukio.

Chagua tukio fulani la kihistoria unalotaka wanafunzi wako walitafiti wakati wa kutembelea makumbusho (au darasani kama una nyenzo husika), mfano, harakati za ukombozi/uhuru. Ni muhimu kuzingatia ufahamu wa wanafunzi wako juu ya tukio fulani, hasahasa kama wanatembelea makumbusho yanayoonyesha matukio ya miaka mingi iliyopita.

Gawanya wanafunzi kwenye makundi, ukiwapa kila kikundi mada tofauti ya kuzingatia juu ya tukio la kihistoria

Jadili aina ya maswali wanayoweza kuhitaji kutafutia majibu wakati wakisoma na kuangalia maonyesho (kama ni kwenye makumbusho) au nyenzo (kama ni shuleni).

Darasani, watake wanafunzi kwenye makundi yao kuandika juu ya utafiti wao katika mabango makubwa. Yaweke mabango darasani au ukumbini kwa wote kuona.

## Somo la 3

Sehemu hii inalenga kupanua mawazo yako namna ya kusaidia wanafunzi kutumia historia simulizi kama nyenzo ya kujifunzia juu ya mambo ya kale. Utawahamasisha kufikiri kiundani juu ya ukweli na uhalisia wa ushahidi huu, na kulinganisha ushahidi wa mapokeo ya matukio ya kihistoria pamoja na ushahidi wa maandishi kwa tukio hilohilo. Kutafiti ufanano na utofauti katika aina mbili za ushahidi kunatoa nafasi nzuri kwa wanafunzi kujifunza.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kukusanya ushahidi wa mapokeo

Bi Paka Ngowa hufundisha historia darasa la Sita kwenye shule ndogo nje kidogo ya Dares Salaam, Tanzania. Familia nyingi katika eneo hilo zilihusika kwenye matukio yaliyopelekea kupatikana kwa uhuru wa Tanzania. Bi Ngowa amewaarika shuleni wageni wawili walioshiriki katika harakati za kupata uhuru ili kuelezea juu ya uzoefu wao. (angalia

nyenzo rejea muhimu: kutumia jamii/mazingira husik a kama nyenzo zitakazo kusaidia kuandaa na kupanga ujio huo) Watakuja kwa siku mfululizo kwa vile hawajuani na wana mitazamo tofauti juu ya uhuru wa Tanzania.

Bi ngowa huwatahadharisha wanafunzi kwamba watu hawa wawili kwa sasa ni wazee sana, na kumbukumbu zao sio nzuri muda wote. Kabla ya wageni kufika, wanafunzi huandaa baadhi ya maswali muhimu wanayotaka kuuliza kwa wazee hao. Kwa siku mbili, wageni hufika na kusimulia hadithi zao. Wanapoondoka, Bi Ngowa na wanafunzi hujadili ufanano na tofauti kati ya hadithi mbili. Pia hujadili sababu zilizopelekea kutofautiana.

Mwalimu huorodhesha dondoo muhimu zilizojitokeza kwenye hadithi zao. Pia huelezea kwamba ingawa historia simulizi inaweza kufanya wanafunzi waelewe vizuri uhuru wa Tanzania, lakini mara nyingine wasimuliaji hawawezi kuwa sahihi na hadithi za watu tofauti huweza kutofautiana. Bi Ngowa anaamini kuwa wanafunzi wake wamejifunza kipindi muhimu katika matumizi na matatizo ya historia simulizi.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Shughuli muhimu: Kulinganisha mahojiano na nyaraka zilizoandikwa

Pamoja na wanafunzi wako, taja tukio muhimu la kihistoria (kama mapigano ya kikabila, au uasi) yaliyotokea. Kama unaweza, tafuta nyaraka zilizoandika juu ya hilo.

Katika kuandaa shughuli hii, unahitaji kujua (kama mwalimu) kuhusu kile jamii yako inachofahamu juu ya uasi au tukio husika. Kumbukumbu hizi ni hadithi simulizi iliyorithiwa kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Watambue baadhi ya watu muhimu ambao wanafunzi wako wanaweza kuzungumza nao nyumbani au wanaweza kuja shuleni.

Peleka wanafunzi wako nje kwenye makundi kwa mahojiano/usaili na wazee hawa. Watake wanafunzi kuorodhesha dondoo muhimu kumi zilizotolewa na kila mhojiwa/msailiwa (Hakikisha wanafunzi wanakwenda kimakundi tu na wako salama muda wote.)

Mkirudi darasani, watake wanafunzi kuelezea matokeo muhimu ya utafiti.

Watake kila kundi kubuni chati/bango la tukio husika, ikijumuisha matukio muhimu na kutumia baadhi ya maelezo ya wageni kutoa hisia ya kile kilichokuwepo.

Onyesha hii darasani.

Jadili pamoja na wanafunzi wako kama wanafikiri wanaushahidi wa kutosha juu ya nini kilitokea kutoka kwa watu walio zungumza nao. Kama hakuna, namna gani wanaweza kutafiti zaidi?

## Nyenzo-rejea ya 1: Historia simulizi

**Taarifa za msingi/welewa wa somo wa mwalimu utangulizi**

Wote tunahadithi za kusimulia, hadithi kuhusu maisha yetu na matukio muhimu yaliyotokea. Tunatoa uzoefu wetu na kuunganisha kumbukumbu zetu kufanya ziwe hadithi. Hadithi hizi zinaweza kuturuhusu kujenga picha halisi juu ya nini kilitokea kama zitaunganishwa na kumbukumbu za watu wengine katika tukio moja.

Jamii yako itakuwa chanzo muhimu kwa utafiti wa nini kilitokea kwa tukio husika au nini kinahisiwa kuwepo pale miaka 20 iliyopita. Wanafunzi wako wanaweza kutafiti vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Wanigeria au vita vya Biafra au matukio mengine.

**Nini maana ya historia simulizi?**

Historia simulizi siyo uwongo au uvumi lakini ni historia ya kweli ya watu wanaozungumziwa kutokana na mitazamo yao kadili wanavyoikumbuka. Inahusu mpangilio mzuri wa ukusanyaji wa hadithi juu ya uzoefu wa

watu. Kumbukumbu hizi za kila siku zina umuhimu kihistoria. Zinatusaidia kuelewa maisha jinsi yalivyo. Kama hatukusanyi na kuzitunza kumbukumbu hizo, siku moja zitapotea moja kwa moja.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Hadithi zako na hadithi za watu wanaokuzunguka ni za pekee na zinaweza kukupa taarifa muhimu.

Kwa sababu tunaishi kwa miaka kadhaa tunaweza kuwa na kumbukumbu za kipindi tu cha maisha. Hii

hufanya wanahistoria wawe na wasiwasi kwamba wanaweza kupoteza kumbukumbu muhimu na mitazamo juu ya matukio. Kukusanya hadithi hizi husaidia wanafunzi wako kukuza hisia za kujitambua wao wenyewe na namna gani wanajiweka katika hadithi ya mazingira yao.

**Namna gani unakusanya hadithi za watu?**

Unapokuwa umeamua ni tukio au shughuli gani unataka kuichunguza, unahitaji kutafuta watu waliohusika na kuwaomba kama wapo tayari kukusimulia hadithi zao.

Wasiliana nao kupanga muda na waambie nini unataka kuzungumzia na nini utafanya.

Unahitaji kunukuu wanachokisema. Unaweza kufanya hivyo kwa kuandika kwa mkono au ikiwezekana kwa kuchukua mkanda wa video au kurekodi sauti.

Baada ya kukusanya habari au ushahidi wao, ni muhimu kulinganisha na kutofautisha mitazamo ya watu tofauti kwenye tukio hilohilo, ili kuweza kugundua ukweli kutoka tafsiri za watu mbalimbali walizonazo juu ya tukio hilo. Unaweza kuwaomba wanafunzi wako katika makundi kufanya mahojiano na watu mbalinbali na halafu kuandika ufupisho wa utafiti wao ili kushirikishana au kushirikiana na wanafunzi wengine. Kitabu kinaweza kutengenezwa kuhusu utafiti wa wanafunzi juu ya tukio Fulani.

*Imenukuliwa kutoka Do History, Website*

## Nyenzo-rejea ya 2: Maswali yanayoweza kutumika kwenye mahojiano

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**

Chini, ni baadhi ya maswali ya kutumia na wageni kutafiti juu ya matukio yaliyopita au namna walivyofanya vitu wakati uliopita. Maeneo unayoweza kutafiti yanajumuisha:

- kuzalisha chakula
- mavazi ya kale
- tiba za asili
- kujenga nyumba
- Elimu

Jozi hizi tatu za masawali ya mwanzo yatakusaidia kuwapa wanafunzi msaada wa kufikiri juu ya maswali yao.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

**1. matukio ya kihistoria.**

- Matukio gani ya kihistoria yalitokea wakati wa udogo wako?
- Ulivaa nini wakati unaenda kwenye sherehe au harusi?
- Nitukio gani unalikumbuka zaidi?
- Unakumbuka nini juu ya hilo?
- Nini kilitokea? Nisimulie ilivyokuwa.
- Nani mwingine alikuwa na wewe?
- Naweza kuongea nao juu ya hadithi hii?

**2. Michezo**

- Ni michezo gani ulicheza wakati wa utoto wako?
- Namna gani ulicheza michezo hiyo?
- Nani alikufundisha kucheza michezo hiyo?
- Lini ulicheza michezo hiyo?
- Ulichezea wapi michezo hiyo?
- Ni shughuli gani nyingine ulizifurahia?

**3. Kuzalisha chakula**

- Mboga na matunda gani ulizalisha?
- Namna gani ulizalisha?
- Ulizalishia wapi?
- Ulitumia zana gani?
- Mboga ziligharimu kiasi gani wakati huo?
- Ulinunua wapi? Mboga gani ulinunua?
- Chakula gani kingine ulikula?
- Je unaendelea kula chakula hicho?

## Nyenzo-rejea ya 3: Uhuru wa Tanzania

**Taarifa za msingi/welewa wa somo wa mwalimu utangulizi**

Tanganyika ilipata uhuru kamili tarehe 9 Desemba 1961 baada ya Nyerere kuwa Waziri Mkuu mapema mwaka huo. Hatukumwaga damu. Huu ulikuwa mfano mzuri wa kile kinachofanywa na umoja na mshikamano na pia ulikuwa mwanzo mzuri kwa taifa. Uhuru wa Zanzibar haukuja kirahisi, ingawa walikuwa chini ya Waingereza, Waarabu walitawala kikamilifu na wao pia walihitaji uhuru. Ukijumuisha kutokubaliana kati ya Waasia,Waafrika na Waarabu wenyewe, utakuwa huna njia nyingine zaidi ya mapinduzi-na ndicho hicho kilichotokea. Baada ya miaka miwili ya kukosa utulivu-na katika jitihada za kuongeza mchakato wa kujitawala- PAFM( Pan African Freedom Movement) kwa Africka Mashariki, Kati na Afrika Kusini viliunganisha vyama vya upinzani na mwaka 1963 mwezi wa Sita, uhuru ulipatikana.

Uhuru kamili wa Zanzibar kutoka kwa Waingereza ulitolewa tarehe 10

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Desemba 1963. kulifuata kutoridhika, na Januari 1964 baada ya vurugu na vita vya wenywewe, Sultani na serikali yake walifukuzwa. Msukumo mkubwa wa mapinduzi ulitoka chama muhimu cha UMMA, chini ya uongozi wa Abdul Rahman Mohammed,kwa kushirikiana na John Okello wa Kenya. Tarehe 11 Januari 1964 walitwaa Zanzibar Mjini na kutangaza serikali mpya ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tarehe 26 Aprili 1964 Zanzibar, Pemba,na Tanganyika ziliungana kufanya Jamhuri ya muungano wa Tanzania. Kama sehemu ya katiba, serikali ya mapinduzi ya Zanzibar ingebaki na uhuru na Raisi wake angekuwa Makamu wa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tanzania ilipopata uhuru wake, ilikuwa masikini na nchi ya mwisho kimaendeleo kwa Afrika Mashariki. Nyerere alikuwa na wasiwasi kuwa wale waliokuwa madarakani wangejitajirisha wenyewe kwa gharama za watu masikini waishio vijijini na kuzuia hilo, alifanya Tanzania iwe na mfumo wa chama kimoja na siasa ya ujamaa. Hili halikuwafurahisha viongozi wa Magharibi. Nyerere alizungumzia upinzani dhidi ya utawala uliojitangazia uhuru Rhodesia, alipata upinzani kutoka kwa Waingereza ambao walikata misaada yote kwa Tanzania. Msaada wa Nyerere kwa wapigania uhuru wa Afrika Kusini, Msumbiji na Angola pia uliiongezea Tanzania maadui hasahasa alipowaruhusu ANC na FRELIMO kufanya shughuli zao Tanzania.

Tanzania pia ilivamiwa na Idi Amin – kiongozi wa Uganda maarufu kwa utawala wake wa mauaji- wakati Nyerere alipowahifadhi baadhi ya Waganda pamoja na Milton Obote na Yoweri Mseveni. Amin alivamia kaskazini magharibi mwa Tanzania Oktoba 1978 na kulilipua Bukoba na Musoma. Mwaka 1979, Nyerere aliweka pamoja jeshi dogo la Tanzania na kujibu kwa kuvamia Uganda na kumwondoa Amin madarakani. Moja kwa moja kitendo hicho kililaaniwa na viongozi wengine wa Afrika-mbali kwamba Amin alikuwa mchokozi. Pia vita hiyo ilishusha uchumi wa Tanzania kwa vile hakukuwa na fidia-iwe kutoka Magharibi au sehemu nyingine ya Afrika.

Wakati huohuo, Zanzibar, mambo yalikuwa hayajatulia. Zanzibar hawakukubali kuungana na Tanganyika matokeo vurugu ziliendelea. Abeid Karume, raisi wa kwanza wa Zanzibar aliuwawa mwaka 1972 na nafasi yake ilichukuliwa na Abdu Jumbe. Miaka michache baadae katika harakati kutuliza vurugu kutokana na kuungana kwa Tanzania bara na Zanzibar, Nyerere aliamuru kuundwa nchi ya chama kimoja kilichoitwa Chama Cha Mapinduzi (CCM). Muungano uliridhiwa Aprili 1977 na ingawa leo kuna chaguzi za vyama vingi, CCM imebaki chama chenye nguvu katika siasa za Tanzania.

*Imetolewa kutoka Absolute Tanzania, Website*

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

# Sehemu ya 3: Kutumia njia tofauti za ushahidi katika historia

**Swali Lengwa muhimu:** Kwa jinsi gani unaweza kutumia 'ramani ya mawazo' na ziara za mafunzo kukuza ujuzi wa kihistoria.

**Maneno muhimu:** ujuzi wa kihistoria; Mawazo; ziara za mafunzo; utafiti, historia; ramani.

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- umetumia ramani ya picha kusaidia wanafunzi kuona umuhimu wa mazingira asili katika makazi ya watu (rejea pia moduli 1, sehemu ya 2);
- Umetumia utafiti wa kundi dogo,ikijumuisha ziara maalumu,kukuza uelewa wa wanafunzi juu ya jamii za kale za Kiafrika.

## Utangulizi

Mbali na kuangalia ushahidi wa mapokeo na maandishi wanafunzi wanaweza pia kujifunza kuhusu mambo ya kale kutoka vyanzo vingine kwa mfani ramani.

Katika sehemu hii,utaunda vipindi na shughuli zitakazo wasaidia wanafunzi kuelewa sababu zilizopelekea kujitokeza kwa falme shupavu za kiafrika siku hizo.Hii inakuwezesha kujua undani wa aina za ushahidi na nyenzo unazoweza kutumia.

Inajumuisha

Kutumia ramani na nyaraka nyingine kuchunguza sababu katika mazingira halisi zilizopelekea kuwepo kwa aina Fulani ya makazi na falme.

Kutafiti umuhimu wa shughuli za ufugaji na kilimo katika kubadilisha maisha ya kiafrika na utamaduni.

Kuwapa mwanga wanafunzi kwa vitu halisi vilivyobakia katika mazingira yanayowazunguka ambavyo vitawasaidia kuchunguza namna kale ilivyokuwa.

## Somo la 1

Kwa kuangalia mazingira ya kawaida na muundo wa nchi inawezekana kufiria sababu zilizofanya jamii kukaa mahali Fulani.

Zimbabwe kuu ni mfano mzuri. Kama mwalimu wa mafunzo ya jamii nimuhimu kuelewa kifani kama hiki, ambacho kinakupa ujuzi wa kuhusianisha mawazo haya na falme tofauti za Kiafrika pamoja na mazingira yako halisi. Kutumia ziara za mafunzo kama ziara kwenye eneo fulani huwezesha kujionea wenyewe kwanini sehemu moja ilichaguliwa kwa makazi na kwanini baadhi ya maendeleo yamedumu kwa muda mrefu kuliko mengine.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Makazi mengi yapo pale kwa sababu mazingira yana baadhi ya mahitaji muhimu kama vile maji au miti, na/au eneo linatoa ulinzi kutoka vitu fulani au dhidi ya maadui. Vijiji na miji mara nyingi hupatikana jirani na mito au misitu ambayo hutoa maji na miti ya ujenzi na kuni. Kwa kuangalia kwa ukaribu mazingira ya shule yako au nyumbani kwa wanafunzi, utawasaidia kuelewa jinsi makazi yalivyoanzishwa.

Ramani za zamani zitaonyesha jinsi eneo lilivyobadilika muda hadi muda (hii inaweza kuwa mwendelezo wa shughuli za matembezi kutoka **moduli 2, Sehemu 1**).

## Uchunguzi kifani ya 1: Kuchunguza maeneo ya utamaduni.

Sekai Chiwamdamira hufundisha darasa la sita katika shule ya msingi Musvingo Zimbabwe. Shule yake iko karibu na eneo la utamaduni la Zimbabwe kuu. Anafahamu kuwa wanafunzi wake wengi pindi waendapo shuleni hupita karibu na eneo hili maarufu lililozungukwa na kuta za mawe. Lakini haelewi kama wanajua kwa nini lipo pale. Sekai hutaka kuwasaidia wanafunzi kutambua kwamba ardhi na rasilimali zake za asili zilichangia katika uamuzi wa watu kuishi katika Zimbabwe Kuu.

Alianza kipindi kwa kuelezea jinsi Zimbabwe kuu ilivyokuwa na nguvu katika falme za kiafrika ambayo ilikuwepo miaka ya 1300-1450 ( **rejea nyenzo 1: Zimbabwe kuu** ). Huwataka wanafunzi kufikiria kwa nini watawala wa falme hii walichagua kuishi katika miinuko ya Zimbabwe kuliko eneo lingine katika Afrika. Ramani ni nyenzo yake muhimu kwa majadiliano haya ( **rejea nyenzo 2: ramani ya picha ya Zimbabwe kuu**). Huonesha uwepo wa dhahabu pembe za ndovu, mbungo, uwepo wa maji na njia za kibiashara kwenye ramani: huwataka wanafunzi wake kupendekeza namna kila moja ilivyochochea watu kujenga makazi hapo yalipo. Kadili wanafunzi wanavyotoa mapendekezo yao, Sekai huchora picha ya mawazo ubaoni

Sekai ameridhishwa na kiwango cha kufikiri na majadiliano kilichoonyeshwa.

## Shughuli ya 1: Kutumia ramani kupata taarifa kuhusu Zimbabwe kuu

Kabla ya kipindi, nakiri ramani na maswali kutoka **nyenzo ya 2**

kwenye ubao au andaa nakala kwa kila kikundi.

Kwanza, elezea kile kinachowakilishwa na ufunguo ubaoni. Halafu, gawanya darasa katika makundi na kitake kila kikundi kupambanua ufunguo kuhusiana na ramani ya Zimbabwe kuu. Kubali kila kitu kinachowakilishwa na ufunguo.

Uliza wanafunzi wako kwanini wanafikiri waliishi hapa kwanza. Unaweza kutumia maswali kutoka **nyenzo ya 2** kama msaada kuanza majadiliano.

Kadili unavyofanya, zunguka zunguka katika makundi kutoa msaada pale unapohitajika kwa kuuliza maswali yanayowaongoza.

Baada ya dakika 15, kitake kila kikundi kuorodhesha mawazo yao

Baada ya hapo, watake kupanga mawazo yao kulingana na umuhimu wake.

Andika mawazo yao ubaoni

Mwisho, waambie wanafunzi kupigia kura sababu tatu wanazofikiri ni muhimu.

Kwa watoto wadogo, unaweza kuangalia katika vitu katika mazingira yao na watake wafikiri kwanini binadamu walishi hapa.

## Somo la 2

Zamani, ng'ombe walitazamwa kama rasilimali muhimu, na wakulima wengi na jamii bado hutazama ng'ombe katika mtazamo huu.

**Lengo la shughuli ya 2 ni kwa wanafunzi kuchunguza** umuhimu wa ng'ombe katika jamii za Kiafrika kwa kutumia jamii husika kama chanzo cha taarifa. Hapo wanafunzi watagundua kiasi gani jamii za wakulima zimebadilika.

**Uchunguzi kifani 2 na shughuli 2** , tumia akili na mwongozo kusaidia wanafunzi juu ya shughuli hii kadili wanavyoshirikiana katika makundi.

## Uchunguzi kifani ya 2: Shughuli za kilimo Arusha

Kuna wakulima wengi wanaoishi Arusha na wengi wa wanafunzi mashuleni ni watoto wa wakulima.Wema pamoja na wanaunzi wake wanataka kuchunguza umuhimu wa ng'ombe katika maisha na utamaduni wa wakulima wa zamani walioishi Tanzania.

Wema huanza kipindi chake kwa kuelezea jukumu muhimu la ng'ombe katika jamii za Kiafrika siku hizo. Huchora ramani ubaoni ambayo husisitiza umuhimu wa ng'ombe na namna ng'ombe walivyotumika. ( **Nyenzo rejea muhimu: Kutumia picha ya mawazo na majadiliano** na

**Nyenzo 3: ufahamu kuhusu ufugaji ng'ombe** kukusaidia kuwauliza maswali wanafunzi). Wanafunzi wajadili mawazo hayo

Katika kipindi kijacho, mtu mzima na wanafunzi katika makundi watakwenda kuwauliza maswali wakulima. Wema amewasiliana nao kujua ambaye yupo tayari kuongea na wanafunzi. wanafunzi walikuwa na maswali rahisi mawili ya kuwauliza wakulima

Kwanini ng'ombe ni muhimu kwako? Nini matumizi ya ng'ombe?

Darasani, wanafunzi hushirikishana utafiti wao na Wema huorodhesha majibu yao ubaoni. Wanajadiliana juu ya kile kilichobadilika kulingana na wakati.

## Shughuli ya 2: Kilimo cha zamani na sasa.

Kabla ya kipindi, soma nyenzo 4: Ng’ombe katika maisha ya kitamaduni-Wamasai.

Elezea kwa wanafunzi umuhimu wa ng’ombe kwa watu wanaoishi Tanzania

Wakiwa katika makundi , watake kuorodhesha sababu zilizopelekea wafuge ngombe

Kwa kazi ya nyumbani, waombe kutafiti kutoka kwa wazee wa jamii zao namna ufugaji ulivyobadilika.

Katika kipindi kinachofuata, waombe wanafunzi kunakiri na halafu kujaza mwongozo katika Nyenzo 5: Umuhimu wa ng’ombe –zamani na sasa kudondoa mawazo yao.

Shirikishana na wanafunzi wote majibu ya kila kundi na weka mwongozo ukutani kwa siku kadhaa ili wanafunzi waweze kujikumbusha.

## Somo la 3

Njia mojawapo ya kujua jinsi jamii ya kale ilivyoishi ni kuchunguza majengo, kazi za sanaa, sanamu na alama za muda mrefu zinazopatikana sehemu fulani.

Katika sehemu hii, wanafunzi waende ziara kwenye maeneo ya kihistoria. Kama hili haliwezekani kwa darasa lako, inawezekana kufanya jambo linalofanana na hilo darasani kwa kutumia nyaraka mbalimbali, picha na kazi za sanaa. Wanafunzi wanaweza kuelewa jinsi ya kutafiti hili na kujaza baadhi ya nafasi wenyewe kuhusiana na nini kilitokea.

## Uchunguzi kifani ya 3: Uandaaji wa ziara ya mafunzo

Jasmin ameshafanya uchunguzi na wanafunzi wake wa darasa la tano kuwa huenda mwanzo wa binadamu ni Afrika Mashariki. Sasa anawataka kufikiri jinsi tunavyojua juu ya hili, kwa vile shule yake ipo jirani na makummbusho ya Olduvai Gorge yaliyo Ngorongoro, huandaa ziara ya mafunzo. Hutaka wanafunzi kuchunguza kazi za sanaa na picha, na kufikiri jinsi wanahistoria walivyotumia taarifa kuongeza uelewa wetu juu ya mabadiliko ya mwanadamu.

Ziarani, wanafunzi wachukue dondoo za taarifa kwenye chati na picha. Pia wanaelezea na kuchora baadhi ya kazi za sanaa na alama ambazo zipo Olduvai Gorge.

Shuleni, hujadili vitu vyote walivyoona na kusikia na kuviorodhesha ubaoni. Jasmine huwaomba kupanga tafiti zao chini ya vichwa tofauti vya habari juu ya aina za majengo waliyoona. Halafu wanafunzi hujadili wanachofikiri kuhusu matumizi ya majengo, kwa kuzingatia mwonekano wake na kazi za sanaa na sanamu zilizomo. Jasmin husaidia kujaza nafasi kwa kuelezea maana ya baadhi ya kazi za sanaa na sanamu. Mawazo hutolewa na wanafunzi wengine wanaalikwa kuona kazi yao.

**Rejea Nyenzo muhimu: matumizi ya mazingira ya asili/jamii husika** kama nyenzo muhimu

## Shughuli muhimu: Kutafiti historia ya mahali

Kabla hujaanza shughuli hii, kusanya taarifa za kutosha kadili unavyoweza kuhusu jamii ya mahali kama ilivyokuwa. Unaweza kuwa na machapisho ya magazeti, dondoo za mazungumzo na wazee katika jamii hiyo, majina ya watu waliotayari kuongea na wanafunzi wako.

Panga wanafunzi kwenye makundi. Elezea kuwa watatafiti kuhusu historia ya kijiji kwa kutumia nyenzo mbalimbali. Kila kundi litashughulika na kipengele kimojawapo, kwa mfano duka, kanisa au shule.

Angalia nyenzo ulizonazo, kabla hujaenda kuongea na watu. Wape wanafunzi muda wakuandaa maswali na halafu wapangie

siku ya kwenda kuuliza maswali kuhusu kipengele chao.

Warudipo shuleni, kila kundi liamue namna ya kuwasilisha utafiti wao darasani.

Shirikishana utafiti

Unaweza kutoa kitabu cha kazi zao kuhusu historia ya eneo husika.

## Nyenzo-rejea ya 1: Zimbabwe kuu

**Taarifa za msingi/welewa wa somo wa mwalimu utangulizi**

Zimbabwe kuu au nyumba ya mawe, ni jina lililotolewa kwa mamia ya ngome za mawe zilizozunguka kilomita za mraba 500 ndani ya Zimbabwe ya sasa, ambayo imeitwa kutokana na ngome hizo.



Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Ngome zinaweza kugawanywa katika makundi matatu tofauti yanajulikana kama Mwinuko Changamano, Bonde Changamano na eneo maarufu lililozungushiwa ukuta. Kiasi cha majengo 300 yapo katika eneo hili lililiozungushiwa ukuta. Aina za majengo ya mawe yanayopatikana katika eneo hili yanaonyesha hali ya uzalendo. Majengo mazuri zaidi yalikuwa kwa ajili ya wafalme na yalijengwa mbali na mji. Inaaminika kuwa ilifanywa hivyo kukwepa ugonjwa wa malale (ugonjwa wa kusinzia).


Mifano michache iliyopo inaonyesha kuwa Zimbabwe kuu pia ilikuwa kituo cha kibiashara, kazi za sanaa zinaonyesha kuwa mji uliunganishwa kibiashara na China. Sarafu kutoka Arabia, shanga na vitu vingine visivyo vya asili vimepatikana katika ardhi ya Zimbabwe.

Hakuna anayejua kwanini eneo hili hatimaye liliachwa. Labda ilisababishwa na ukame, magonjwa au inaweza kuwa kuanguka kwa biashara ya dhahabu iliyowalazimu watu walioishi Zimbabwe kuu kwenda sehemu nyingine. Ngome za Zimbabwe kuu ni shemu zilizochukuliwa na UNESCO tangu 1986.

*Imenukuliwa kutoka: Zimbabwe Wikipedia, Website*

## Nyenzo-rejea ya 2: Ramani ya picha ya Zimbabwe kuu

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**




Tafuta Zimbabwe kuu

1. Tafuta miinuko ya Zimbabwe. Unafikiri ni kwanini waanzilishi wa Zimbabwe kuu waliamua kuanzisha makazi juu ya miinuko?
2. Rasilimali gani za asili zilipatikana hapo na eneo linalozunguka Zimbabwe kuu?
3. Kwanini rasilimali hizi zilikuwa muhimu?
4. Ni sababu zipi nyingine za kimazingira zilizochangia katika uamuzi wa kuweka makazi juu ya miinuko?

*Chanzo: dyer, c., nisbet, j., friedman, m., johannesson, b., jacobs, m., roberts, b. & seleti, y. (2005). looking into the past: source-based history for grade 10. cape town: maskew miller longman. isbn 0 636 06045 4.*

## Nyenzo-rejea ya 3: Ufahamu juu ya ufugaji ngo'mbe

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**




## Nyenzo-rejea ya 4: Ng'ombe na utamaduni wa maisha ya Wamasai

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**

Maisha ya kabila la wamasai waishio Kenya na Tanzania yanahusu ng'ombe wao ambao ni chanzo kikuu cha chakula na uchumi wao. Wanaamini kuwa Mungu aliwapa ng'ombe wakuchunga na majukumu ya kijamii na hadhi yao inapatikana na mahusiano yao na ng'ombe.



Provided by: Drew Conroy

Madaraja ya Wamasai hutegemea kiasi cha ng’ombe ilichonacho familia, hivyo ng’ombe ni mara chache huchinjwa; huachwa wazaliane kama ishara ya utajiri na huuzwa au kununuliwa kulipa deni. Mara nyingine askari wa kimasai huandaliwa kimakundi kwa lengo la kuiba au kunyang’anya ng’ombe.

Mazingira yao ya kuchungia ngombe yanaanzia katikati ya Kenya hadi katikati ya Tanzania. Vijana wakiume wanahusika kuchunga ng’ombe na kawaida huishi kwenye kambi ndogondogo, wakihama mara kwa mara kutafuta maji na malisho mazuri. Kwa vile wanahamahama, Wamasai hujenga nyumba za muda kwa kinyesi cha ng’mbe na matope. Mchanganyiko huu hukauka haraka na jua na ni mgumu kama saruji na hautoi harufu. Nyumba hujengwa kwa mduara; usiku ng’ombe wote huwekwa katikati ili kuwaepusha na wanyama wakali.

Maziwa ya ng’ombe pamoja na damu ni chakula cha kila siku kwa wamasai ambao hawali matunda wala nafaka. Mara moja kwa mwezi damu huchukuliwa kwa wanyama hai kwa kuchoma mkuki shingoni.

Damu hii huchanganywa na maziwa kwenye kibuyu kilichooshwa kwa mkojo kuzuia yasiharibike.

*Imenukuliwa kutoka: University of Iowa, Website*

## Nyenzo-rejea ya 5: Umuhimu wa ng’ombe-zamani na sasa

**Kwa matumizi ya wanafunzi**

| **Umuhimu wa ng’ombe zamani** | **Umuhimu wa ng’ombe sasa** |
|---|---|
| Ng’ombe walikuwa muhimu kwa: | Ng’ombe ni muhimu kwa: |
| | |
| | |
| | |
| | |

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

# Sehemu ya 4: Ufahamu wa Chati ya kalenda ya matukio

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kutumia kalenda ya matukio ya kihistoria na nyenzo nyingine kukuza ufahamu wa chanzo na matokeo?

**Maneno muhimu:** Chati ya wakati na matukio, mabadiliko ya kihistoria; mpangilio wa matukio ya kihistoria; historia; vyanzo vya kihistoria; mdahalo

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- umetumia kalenda ya matukio kuonyesha mabadiliko ya kihistoria kipindi hadi kipindi;
- umewasaidia wanafunzi kutambua matukio muhimu katika mchakato fulani wa kihistoria;
- umewahamasisha wanafunzi kuiangalia historia sio kama mtiririko wa tarehe za kujifunza lakini ni mchakato wa kutafiti;
- Umetumia nyenzo mbalimbali kusaidia wanafunzi kujifunza kwamba tukio moja linaweza kuwa ni matokeo ya sababu nyingi.

## Utangulizi

Unapokuza ufahamu wa muda uliopita na unaoendelea kupita, ni muhimu kuwa na uwezo wa kupanga matukio katika mpangilio fulani kulingana na yalivyokuwa yanatokea.

Mara nyingi wanafunzi huhangaikia kujua dhana ya muda. Katika sehemu hii kitu cha kwanza utawasaidia wanafunzi wako kugawanya muda katika vipindi ambavyo ni rahisi kuelewa; mara wakiweza kufanya hili, kufikiri kuhusu mtiririko wa matukio na kwa nini ni muhimu. (kwa wanafunzi wadogo hili linaweza kurahisishwa kwa utawasaidia namna ya kupanga kazi fulani wanazozifanya, ukiwaelekeza kwenye shughuli ngumu kadili ufahamu wao unavyoongezeka). Utawasaidia wanafunzi wako kutambua matukio muhimu katika kipindi fulani. Hili litawaongoza wanafunzi wadogo na wakubwa kwenye uchambuzi wa chanzo na matokeo yake, na kujua kuwa kuna sababu zaidi ya moja katika tukio fulani.

## Somo la 1

Kutafiti kipindi fulani cha kihistoria, na kujaribu kupanga matukio kwa mtirirko kadili yalivyotokea kutasaidia wanafunzi kuanza kuona uhusiano kati ya matukio na baadhi ya sababu za matukio. Kujua chanzo cha mabadiliko katika nchi na jamii zetu, inaweza kutusaidia kuishi maisha bora.

Kusudio la sehemu hii ni kutafuta namna matumizi ya kalenda ya matukio ya kihistoria yanavyoweza kuwa ni njia muhimu katika kugawanya vipindi ili kujua ni kipindi gani tunahusika nacho. Hili ni muhimu hasa pale tunapofundisha historia kwa sababu ni lazima wanafunzi kujua mabadiliko kutegemeana na muda.

Wanafunzi wanahitaji kusaidiwa kuchambua na kupanga matukio kutoka utotoni. Kadili wanavyokua na kuishi wanaweza kurejea shughuli kama hizi kwa kutumia mchanganyiko zaidi wa matukio.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

(**Sehemu ya 1** katika moduli hii imetumia kalenda ya matukio kutafiti historia ya familia. Inafaa kuangalia sehemu hiyo kama bado hujapitia, hasa kama unafanya kazi na wanafunzi wenye umri mdogo)

## Uchunguzi kifani ya 1: Mpangilio wa matukio

Tetha Rugenza, ambaye hufundisha historia katika shule ndogo Rwanda, anataka kuwaonyesha wanafunzi wa darasala 4 jinsi ya kugawanya muda katika vipindi vidogo vidogo. Ili kufanya hili, huandaa kipindi ambapo wanafunzi na yeye mwenyewe hujifunza namna ya kutengeneza kalenda ya matukio na kuigawanya katika vipindi.

Rugenza huamua kutumia mfano wa Rwanda. Huchora kalenda ya matukio ya historia ya Rwanda ubaoni. Kuwasaidia wanafunzi kuelewa dhana ya vipindi, hugawanya historia ya Rwanda katika vipindi vya kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na wakati wa uhuru.

Huandika orodha ya matukio muhimu pamoja na tarehe yalipotokea kwenye vipande tofauti vya karatasi na kuweka mezani. Kila tukio, analowaelezea wanafunzi lipo katika kipindi fulani. Huwataka wanafunzi wake kupanga matukio kulingana na vipindi yalipotokea.

Huanza na tukio moja na huruhusu mwanafunzi kuchukua tukio la pili na kubandika sehemu husika kwenye kalenda ya matukio. Wanafunzi wengine huhakikisha kama tukio limewekwa katika sehemu sahihi. Kupitia majadiliano, huwasaidia wanafunzi kama hawana uhakika na mahali tukio linapotakiwa kuwekwa. Huwataka wanafunzi kufikiri kama kuna matukio mengine ya kitaifa yanayoweza kuwekwa kwenye kalenda ya matukio nayo pia huyapanga katika mtiririko unaofaa.

## Shughuli ya 1: Uchoraji wa kalenda ya matukio

Waambie wanafunzi kuwa wanatakiwa kutengeneza kalenda ya matukio ya shule kwa pamoja.

Anza kipindi kwa kuwataka wanafunzi wako kuandika matukio muhimu yaliyotokea shuleni katika mwaka husika.

Watake wanafunzi kutoa tarehe ya kila tukio kama wanaweza au watafute tarehe hizo.

Watake wanafunzi kupanga matukio haya kutoka mwanzo hadi mwisho wa mwaka wa shule.

Wasaidie wanafunzi kufanya uamuzi kuhusu ukubwa wa kalenda za matulio wanaoutaka na kutengezeza kipimo inavyotakiwa.

Watake wanafunzi kuonyesha mwezi kwa usahihi kulingana na vipimo walivyochagua na kuandika tarehe za matukio kushoto mwa kalenda- matukio ya miaka ya zamani yaanzie chini nay a tarehe za karibuni yawe juu.

Katika upande wa kulia wa kalenda ya matukio, watake wanafunzi waandike maelezo mafupi ya tukio husika dhidi ya kila tarehe.

Weka wazi hiyo kalenda ili wote waione. (kama huna nyenzo za kutosha kwa kila mwanafunzi kufanya peke yake, basi kazi hii inaweza kufanywa katika makundi ya wanafunzi wasiozidi watano.) Darasa zima wajadili kama kuna matukio ya shule yaliyoweza kutokea

wakati wowote katika mwaka. Je kuna yale yanayotokea katika kipindi fulani? Kwa nini? (kwa mfano, kwa nini mitihani ya kumaliza mwaka haiwezi kufanywa mwanzoni mwa muhula?

Zamani, ng'ombe walitazamwa kama rasilimali muhimu, na wakulima wengi na jamii bado hutazama ng'ombe katika mtazamo huu.

## Somo la 2

**Lengo la shughuli ya 2 ni kwa wanafunzi kuchunguza** umuhimu wa ng'ombe katika jamii za Kiafrika kwa kutumia jamii husika kama chanzo cha taarifa. Hapo wanafunzi watagundua kiasi gani jamii za wakulima zimebadilika.

**Uchunguzi kifani 2 na shughuli 2**, tumia akili na mwongozo kusaidia wanafunzi juu ya shughuli hii kadili wanavyoshirikiana katika makundi.

## Uchunguzi kifani ya 2: Shughuli za kilimo Arusha

Kuna wakulima wengi wanaoishi Arusha na wengi wa wanafunzi mashuleni ni watoto wa wakulima.Wema pamoja na wanaunzi wake wanataka kuchunguza umuhimu wa ng'ombe katika maisha na utamaduni wa wakulima wa zamani walioishi Tanzania.

Wema huanza kipindi chake kwa kuelezea jukumu muhimu la ng'ombe katika jamii za Kiafrika siku hizo. Huchora ramani ubaoni ambayo husisitiza umuhimu wa ng'ombe na namna ng'ombe walivyotumika. ( **Nyenzo rejea muhimu: Kutumia picha ya mawazo na majadiliano** na

**Nyenzo 3: ufahamu kuhusu ufugaji ng'ombe** kukusaidia kuwauliza maswali wanafunzi). Wanafunzi wajadili mawazo hayo

Katika kipindi kijacho, mtu mzima na wanafunzi katika makundi watakwenda kuwauliza maswali wakulima. Wema amewasiliana nao kujua ambaye yupo tayari kuongea na wanafunzi.

Wanafunzi walikuwa na maswali rahisi mawili ya kuwauliza wakulima

Kwanini ng'ombe ni muhimu kwako? Nini matumizi ya ng'ombe?

Darasani, wanafunzi hushirikishana utafiti wao na Wema huorodhesha majibu yao ubaoni. Wanajadiliana juu ya kile kilichobadilika kulingana na wakati.

## Shughuli ya 2: Kilimo cha zamani na sasa.

Kabla ya kipindi, soma nyenzo 4: Ng'ombe katika maisha ya kitamaduni-Wamasai.

Elezea kwa wanafunzi umuhimu wa ng'ombe kwa watu wanaoishi Tanzania

Wakiwa katika makundi , watake kuorodhesha sababu zilizopelekea wafuge ngombe

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Kwa kazi ya nyumbani, waombe kutafiti kutoka kwa wazee wa jamii zao namna ufugaji ulivyobadilika.

Katika kipindi kinachofuata, waombe wanafunzi kunakiri na halafu kujaza mwongozo katika Nyenzo 5: Umuhimu wa ng'ombe –zamani na sasa kudondoa mawazo yao.

Shirikishana na wanafunzi wote majibu ya kila kundi na weka mwongozo ukutani kwa siku kadhaa ili wanafunzi waweze kujikumbusha.

## Somo la 3

Njia mojawapo ya kujua jinsi jamii ya kale ilivyoishi ni kuchunguza majengo, kazi za sanaa, sanamu na alama za muda mrefu zinazopatikana sehemu fulani.

Katika sehemu hii, wanafunzi waende ziara kwenye maeneo ya kihistoria. Kama hili haliwezekani kwa darasa lako, inawezekana kufanya jambo linalofanana na hilo darasani kwa kutumia nyaraka mbalimbali, picha na kazi za sanaa. Wanafunzi wanaweza kuelewa jinsi ya kutafiti hili na kujaza baadhi ya nafasi wenyewe kuhusiana na nini kilitokea.

## Uchunguzi kifani ya 3: Uandaaji wa ziara ya mafunzo

Jasmin ameshafanya uchunguzi na wanafunzi wake wa darasa la tano kuwa huenda mwanzo wa binadamu ni Afrika Mashariki. Sasa anawataka kufikiri jinsi tunavyojua juu ya hili, kwa vile shule yake ipo jirani na makummbusho ya Olduvai Gorge yaliyo Ngorongoro, huandaa ziara ya mafunzo. Hutaka wanafunzi kuchunguza kazi za sanaa na picha, na kufikiri jinsi wanahistoria walivyotumia taarifa kuongeza uelewa wetu juu ya mabadiliko ya mwanadamu.

Ziarani, wanafunzi wachukue dondoo za taarifa kwenye chati na picha. Pia wanaelezea na kuchora baadhi ya kazi za sanaa na alama ambazo zipo Olduvai Gorge.

Shuleni, hujadili vitu vyote walivyoona na kusikia na kuviorodhesha ubaoni. Jasmine huwaomba kupanga tafiti zao chini ya vichwa tofauti vya habari juu ya aina za majengo waliyoona. Halafu wanafunzi hujadili wanachofikiri kuhusu matumizi ya majengo, kwa kuzingatia mwonekano wake na kazi za sanaa na sanamu zilizomo. Jasmin husaidia kujaza nafasi kwa kuelezea maana ya baadhi ya kazi za sanaa na sanamu. Mawazo hutolewa na wanafunzi wengine wanaalikwa kuona kazi yao.

**Rejea Nyenzo muhimu: matumizi ya mazingira ya asili/jamii husika** kama nyenzo muhimu

## Shughuli muhimu: Kutafiti historia ya mahali

Kabla hujaanza shughuli hii, kusanya taarifa za kutosha kadili unavyoweza kuhusu jamii ya mahali kama ilivyokuwa. Unaweza kuwa na machapisho ya magazeti, dondoo za mazungumzo na wazee katika jamii hiyo, majina ya watu waliotayari kuongea na wanafunzi wako.

Panga wanafunzi kwenye makundi. Elezea kuwa watatafiti kuhusu historia ya kijiji kwa kutumia nyenzo mbalimbali. Kila kundi litashughulika na kipengele kimojawapo, kwa mfano duka, kanisa au shule.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Angalia nyenzo ulizonazo, kabla hujaenda kuongea na watu.

Wape wanafunzi muda wakuandaa maswali na halafu wapangie siku ya kwenda kuuliza maswali kuhusu kipengele chao.

Warudipo shuleni, kila kundi liamue namna ya kuwasilisha utafiti wao darasani.

Shirikishana utafiti

Unaweza kutoa kitabu cha kazi zao kuhusu historia ya eneo husika.

## Nyenzo-rejea ya 1: Zimbabwe kuu

**Taarifa za msingi/welewa wa somo wa mwalimu utangulizi**

Zimbabwe kuu au nyumba ya mawe, ni jina lililotolewa kwa mamia ya ngome za mawe zilizozunguka kilomita za mraba 500 ndani ya Zimbabwe ya sasa, ambayo imeitwa kutokana na ngome hizo.



Ngome zinaweza kugawanywa katika makundi matatu tofauti yanajulikana kama Mwinuko Changamano, Bonde Changamano na eneo maarufu lililozungushiwa ukuta. Kiasi cha majengo 300 yapo katika eneo hili lililiozungushiwa ukuta. Aina za majengo ya mawe yanayopatikana katika eneo hili yanaonyesha hali ya uzalendo. Majengo mazuri zaidi yalikuwa kwa ajili ya wafalme na yalijengwa mbali na mji. Inaaminika kuwa ilifanywa hivyo kukwepa ugonjwa wa malale (ugonjwa wa kusinzia). Mifano michache iliyopo inaonyesha kuwa Zimbabwe kuu pia ilikuwa kituo cha kibiashara, kazi za sanaa zinaonyesha kuwa mji uliunganishwa kibiashara na China. Sarafu kutoka Arabia, shanga na vitu vingine visivyo vya asili vimepatikana katika ardhi ya Zimbabwe.

Hakuna anayejua kwanini eneo hili hatimaye liliachwa. Labda ilisababishwa na ukame, magonjwa au inaweza kuwa kuanguka kwa biashara ya dhahabu iliyowalazimu watu walioishi Zimbabwe kuu kwenda sehemu nyingine.

Ngome za Zimbabwe kuu ni shemu zilizochukuliwa na UNESCO tangu 1986.

*Imenukuliwa kutoka: Zimbabwe Wikipedia, Website*

## Nyenzo 2: Jedwali la Kalenda ya matukio ya Kiafrika

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Nigeria | | | | | Uhuru (63) | | | | | | | | | | |
| Tarehe | 1940 | 1945 | 1950 | 1955 | 1960 | 1965 | 1970 | 1975 | 1980 | 1985 | 1990 | 1995 | 2000 | 2005 | 2010 |
| Ghana | | | | uhuru (57) | | | | | | | | | | | |
| Tarehe | 1940 | 1945 | 1950 | 1955 | 1960 | 1965 | 1970 | 1975 | 1980 | 1985 | 1990 | 1995 | 2000 | 2005 | 2010 |
| | | | | uhuru | | | | | | | | | | | |
| Sudan | | | | (57) | | | | | | | | | | | |
| Tarehe | 1940 | 1945 | 1950 | 1955 | 1960 | 1965 | 1970 | 1975 | 1980 | 1985 | 1990 | 1995 | 2000 | 2005 | 2010 |
| Kenya | | | | | uhuru (63) | | | | | | | | | | |
| Tarehe | 1940 | 1945 | 1950 | 1955 | 1960 | 1965 | 1970 | 1975 | 1980 | 1985 | 1990 | 1995 | 2000 | 2005 | 2010 |
| Rwanda | | | | | | | | | | | | | | | |
| Tarehe | 1940 | 1945 | 1950 | 1955 | 1960 | 1965 | 1970 | 1975 | 1980 | 1985 | 1990 | 1995 | 2000 | 2005 | 2010 |
| Afrika Kusini | | | | | | | | | | | | | | | |
| Tarehe | 1940 | 1945 | 1950 | 1955 | 1960 | 1965 | 1970 | 1975 | 1980 | 1985 | 1990 | 1995 | 2000 | 2005 | 2010 |
| Matukio ya Dunia | | | | | | | | | | | | | | | |
| Tarehe | 1940 | 1945 | 1950 | 1955 | 1960 | 1965 | 1970 | 1975 | 1980 | 1985 | 1990 | 1995 | 2000 | 2005 | 2010 |

# Nyenzo-rejea ya 3: Matukio muhimu kuelekea uhuru

**Taarifa za msingi/welewa wa somo wa mwalimu utangulizi**

| | |
|---|---|
| 1957 | Ghana inakuwa nchi ya kwanza ya Afrika kupata uhuru chini ya Kwame Nkrumah kupitia mikutano kama ile ya Ghandi, migomo, kuwalazimisha Waingereza kutoa uhuru |
| 1958 | Chinua Achebe(Nigeria): Things Fall Apart, kilicho andikwa kwa ‘Kingereza cha Kiafrika’ kinachunguzia madhara ya utamaduni wa Magharibi kwa tamaduni za asili. |
| 1958 | Mkutano wa mataifa yote ya Afrika: suluhisho la ubepari na ukolini, Accra, 5-13 Desemba 1958 |
| 1954–1962 | Makoloni ya Kifaransa (mataifa ya Kiafrika yanayo zungumza Kifaransa) yanakataa kuendelea kutawaliwa hata kama wanatambua kuwa uchumi na tamaduni zao bado zinategemea Ufaransa-isipokuwa Algeria iliyokua na walowezi wapatao millioni 1. Vita vya kikabila nchini Algeria viliendelea hadi ulipopatikana uhuru mwaka 1962, miaka sita baadae baadaye Moroko na Tunisia kupata uhuru. |
| 1958 | Makaburu wenye asili ya Kidachi walipata uhuru kutoka kwa Waingereza Afrika Kusini. |
| 1964 | Nelson Mandela, katika hukumu ya uhaini na viongozi wenzake wa ANC mbele ya Mahakama Kuu ya Pretoria, anatoa hotuba kali kabla hajafungwa kwa muda wa miaka 25 katika gereza lililo kisiwani Robben. |
| 1960–1961 | Zaire (koloni la zamani la Ubelgiji) linapata uhuru kutoka kwa Wabelgiji mwaka 1960. Halafu katika mji wa Elisabethville( sasa Lubumbashi ), kiongozi mzalendo Patrice Lumumba aliuwawa mwaka 1961, na kanali Joseph Desere Mobuto (30) ambaye alikuja kuwa raisi. (Bill Berkeley, ‘Zaire: An African Horror Story’, The Atlantic Monthly, August 1993; rpt. Atlantic Online) |
| 1962 | Algeria inapata uhuru kutoka kwa Wafaransa, zaidi ya walowezi 900,000 wanaihama nchi mpya. |
| 1963 | Kenya inatangaza uhuru kutoka kwa Waingereza |
| 1963 | Mkataba wa umoja wa nchi huru za Afrika, 25 Mei 1963 |
| Mid-60s | Nchi nyingi za Afrika zinapata uhuru na kipindi cha ukoloni kinaisha. Vile vile utawala wa uchumi na utamaduni wa magharibi na uchu wa mali na madaraka vinaongeza matatizo yanayozikumba nchi huru za Kiafrika. |
| 1965 | Rodesia: kutangazwa kwa utawala wa watu wachache |
| 1966 | Bechuanaland inapata uhuru na kuwa Botswana |
| 1970s | Wareno wanapoteza makoloni ya Afrika, pamoja na Angola na Msumbiji |

| | |
|---|---|
| 1976 | Cheikh Anta Diop( Senegal , 1923-1986), moja wa wanataaluma wa Afrika wa karne ya 20, anatoa kitabu, Afrika chanzo cha Ustaarabu kuondoa uvumi (kuhusu historia ya Afrika) tulio jifunza na kusahihisha kwa kizazi kijacho. |
| 1980 | Zimbabwe ( zamani Rodesia ya Kusini inapata uhuru kutoka kwa walowezi wa kizungu baada ya miaka kadhaa ya uadui |
| 1970s–1980s | Watawala wachache wa Kizungu Afrika Kusini wanasisitiza kuendeleza ubaguzi na mfumo usio na usawa wa ubaguzi wa rangi kupelekea vurugu, uadui, migomo na mauaji kutawala. |
| 1986 | Mnigeria mwandishi wa tamthilia za fasihi Wole Soyinka anatuzwa zawadi ya Nobel 1986. |
| 1988 | Mmisri mwandishi wa hadithi na hadithi fupi Nahfouz anatuzwa zawadi ya Nobel 1988, mwandishi wa kwanza kushinda akiwa Kiarabu ndiyo lugha yake ya asili(ya kwanza) |
| 1994<br><br>1996 | Wahutu waliua Watusi wapatao 1,000,000, huku wakiogopa serikali ya Kitusi kulipa kisasi zaidi ya wahutu millioni 1 walihama Rwanda kwa mkupuo na kuvuta hisia dunia nzima.<br><br>Wakimizi wa Kihutu kama 500,000 walirudi Rwanda kutoka Zaire kuepuka vita nchini zaire |
| 2001 | Baada ya miaka 38 ya uwepo,OAU (http:// oau.oua.org) inageuzwa kuwa Umoja wa Afrika (AU) |

## Kalenda-Nchi za Afrika katika mpangilio wao wa kupata uhuru

| Nchi | Jina la ukoloni | wakoloni | Tarehe ya uhuru | Mkuu wa kwanza wa nchi |
|---|---|---|---|---|
| Ethiopia | Ufalme wa Aksum | | Karne ya kwanza kabla ya Yaesu | Menelik I |
| Liberia | Jumuia ya madola ya Liberia | utawala wa jamii ya kiamerika | 26 Julai 1847 | Joseph Jenkins Roberts |
| Libya | Libya | Italia | 24 Desemba 1951 | Idris |
| misri | misri | Uingereza | 1922/1936/1953 | n/a |
| Sudani | sudani | Uingereza | Januari 1956 | Ismail al-Azhari |
| Tunisia | Tunisia | Ufaransa | 20, machi 1956 | Muhammad VIII al-Amin |
| Moroko | Moroko | Ufaransa | 7 Aprili 1956 | Mohammed V |
| Ghana | Gold Coast | Uingereza | 6machi 1957 | Kwame Nkrumah |
| Guinea | French West Africa | Ufaransa | 2 Oktoba 1958 | Sékou Touré |
| Cameroon | Cameroun | Ufaransa, Uingereza | 1 Januari 1960 | Ahmadou Ahidjo |
| Togo | ufaransa Togoland | Ufaransa | 27 Aprili 1960 | Sylvanus Olympio |
| Mali | French West Africa | Ufaransa | 20 Juni 1960 | Modibo Keita |
| Senegal | French West Africa | France | 20 June 1960 | Léopold Senghor |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Madagascar | Malagasy Protectorate | France | 26 June 1960 | Philibert Tsiranana |
| Nchi | Jina la ukoloni | wakoloni | Tarehe ya uhuru | Mkuu wa kwanza wa nchi |
| DR Congo | Belgian Congo | Belgium | 30 June 1960 | Patrice Lumumba |
| Somalia | Italian Somaliland, British Somaliland | Italy, Britain | 1 July 1960 | Aden Abdullah Osman Daar |
| Benin | French West Africa | France | 1 August 1960 | Hubert Maga |
| Niger | French West Africa | France | 3 August 1960 | Hamani Diori |
| Burkina Faso | French West Africa | France | 5 August 1960 | Maurice Yaméogo |
| Côte d'Ivoire | Côte d'Ivoire | France | 7 August 1960 | Félix Houphouët-Boigny |
| Chad | French Equatorial Africa | France | 11 August 1960 | François Tombalbaye |
| Central African Republic | French Equatorial Africa | France | 13 August 1960 | David Dacko |
| Congo | French Equatorial Africa | France | 15 August 1960 | Fulbert Youlou |
| Gabon | French Equatorial Africa | France | 17 August 1960 | Léon M'ba |

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Nigeria | Nigeria | Britain | 1 October 1960 | Nnamdi Azikiwe |
| Mauritania | French West Africa | France | 28 November 1960 | Moktar Ould Daddah |
| Sierra Leone | Sierra Leone | Britain | 27 April 1961 | Milton Margai |
| Tanzania | Tanganyika | Britain | 9 December 1961 | Julius Nyerere |
| Nchi | Jina la ukoloni | wakoloni | Tarehe ya uhuru | Mkuu wa kwanza wa nchi |
| Rwanda | Ruanda-Urundi | Belgium | 1 July 1962 | Grégoire Kayibanda |
| Burundi | Ruanda-Urundi | Belgium | 1 July 1962 | Mwambutsa IV |
| Algeria | Algeria | France | 3 July 1962 | Ahmed Ben Bella |
| Uganda | British East Africa | Britain | 9 October 1962 | Milton Obote |
| Kenya | British East Africa | Britain | 12 December 1963 | Jomo Kenyatta |
| Malawi | Nyasaland | Britain | 6 July 1964 | Hastings Kamuzu Banda |
| Zambia | Northern Rhodesia | Britain | 24 October 1964 | Kenneth Kaunda |
| Gambia | Gambia | Britain | 18 February 1965 | Dawda Kairaba Jawara |
| Botswana | Bechuanaland | Britain | 30 September 1966 | Seretse Khama |
| Lesotho | Basutoland | Britain | 4 October 1966 | Leabua Jonathan |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Mauritius | | Britain | 12 March 1968 | |
| Swaziland | Swaziland | Britain | 6 September 1968 | Sobhuza II |
| Equatorial Guinea | Spanish Guinea | Spain | 12 October 1968 | Francisco Macías Nguema |
| Guinea-Bissau | Portuguese Guinea | Portugal | 24 September 1973 | Luis Cabral |
| Mozambique | Portuguese East Africa | Portugal | 25 June 1975 | Samora Machel |
| Cape Verde | | Portugal | 5 July 1975 | |
| Comoros | | France | 6 July 1975 | |
| Nchi | Jina la ukoloni | wakoloni | Tarehe ya uhuru | Mkuu wa kwanza wa nchi |
| São Tomé and Príncipe | | Portugal | 12 July 1975 | |
| Angola | Angola | Portugal | 11 November 1975 | Agostinho Neto |
| Seychelles | | Britain | 29 June 1976 | |
| Djibouti | French Somaliland | France | 27 June 1977 | Hassan Gouled Aptidon |
| Zimbabwe | Southern Rhodesia | Britain | 18 April 1980 | Robert Mugabe |
| Namibia | South West Africa | South Africa | 21 March 1990 | Sam Nujoma |
| Eritrea | Eritrea | Ethiopia | 24 May 1993 | Isaias Afewerki |
| South Africa | South Africa | South Africa (apartheid) | 27 April 1994 | Nelson Mandela |
| Sahrawi Republic 1 | Spanish Sahara | Spain | 27 February 1976 | El-Ouali Mustapha Sayed |

*Imenukuliwa kutoka: Decolonization of Africa, Wikipedia, Website*

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

# Sehemu ya 5: Kutumia kazi za sanaa kujifunza mambo ya kale

**Swali Lengwa muhimu:** unawezaje kutumia kazi za sanaa na ushahidi mwingine kutafita historia ya mahali fulani na ya kitaifa?

**Maneno muhimu:** kazi za sanaa; ushahidi; kazi za makundi; historia ya mahali; mazingira; kuuliza

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- umetumia kazi za sanaa kusaidia wanafunzi kuibua maswali juu ya mambo ya kale na kuifahamu historia yao;
- umeandaa vipindi vinavyowafanya wanafunzi kujitambua wao kwa kufikiri na kujihusianisha na historia ya taifa lao;
- Umetumia wataalamu wa ndani na mazingira ya mahali hapo katika kipindi chako kuamsha hamasa ya wanafunzi ya kutaka kujua historia yao.

## Utangulizi

Kujifahamu wewe ni nani na kujitambua kunaimarishwa kama una uelewa mpana juu ya utambulisho wako na unaweza kuona nafasi yako katika maisha kwa ujumla. Kujifunza kilichotokea zamani kunaweza kuchangia hili. Kupitia kazi za sehemu hii,utawahamasisha wanafunzi wako kufikiria jinsi walivyosehemu ya historia hiyo. Kwa kutumia kazi za makundi, kualika wageni darasani na kazi za mikono, kuchunguza kazi za sanaa kutawafanya wanafunzi kushirikishana mawazo na kukuza ujuzi wao katika historia.

## Somo la 1

Kutumia kazi za sanaa au kuangalia picha zao ni njia yakuwafanya wawe wasikivu kwa dhana halisi ya historia na tafsiri yake. Kitu kinachoweza kukusaidia katika kazi hii ni kukusanya nyenzo kama zilivyo na kadili unavyoweza. Daima inawezekana kutafuta vyombo vya zamani na kazi za sanaa kutoka nyumbani na sokoni.

Sehemu hii itakusaidia kupanga shughuli kwa wanafunzi wako kufikiri jinsi vitu tunavyotumia katika maisha yetu ya kila siku vilivyobadilika. Kwa mfano, vitu tunavyotumia kupikia sasa na tulivyotumia zamani tunaweza kupata picha namna gani watu waliishi. Tunaweza kulinganisha vyombo na kutokana na ulinganisho huo, kubuni juu ya maisha yalivyokuwa zamani kwa kutumia kazi za sanaa kama hizo. Hili litawahamasisha wanafunzi kujitafakari nafasi yao katika jamii yao na historia yake.

## Uchunguzi kifani ya 1: Uchunguzi wa vitu

Bwana Ndomba, mwalimu wa darasa la 5 mjini Mbinga, Tanzania ameamua kutumia kazi za sanaa zilizotumika kwa kilimo katika somo lake kuamusha udadisi wa wanafunzi na kuwahamasisha kufikiri kihistoria.

Hupanga darasa katika makundi, na kuwapa kila kundi kazi halisi za sanaa au picha mojawapo. Huwataka kuangalia picha au vitu kwa undani na kuandika kadili wanavyoweza juu ya vitu au picha hizo. Wanafunzi wake hufanya vizuri,kwa kuwa hupenda majadiliano, na inaeleweka kwa Ndomba kuwa wanavutiwa na wanafurahia kudadisi juu ya kazi za sanaa. (**rejea Nyenzo muhimu: utumiaji wa kazi za makundi darasani** )

Baada ya dakika chache, hulitaka kila kundi kubadilishana picha au kazi za sanaa zao na kundi jingine na kufanya tena zoezi lile. Wanapo maliza huamuru makundi mawili kuungana na kushirikishana mawazo yao juu ya picha na kazi za sanaa. Wanafikiri nini juu ya kazi hizo za sanaa?

Zimetengenezwa kwa kutumia nini? Zimetengenezwaje? Wanakubaliana kuandika dondoo tano kwa kila kazi ya sanaa, na kila kundi hushughulika na picha au kazi moja ya sanaa.

Bwana Ndomba huweka kazi za sanaa mezani na dondoo zake tano na kuweka mahali wazi kwa siku kadhaa ili wote waone.

Mwishoni mwa juma, hutaka kila kundi kuandika kwenye upande mmoja wa karatasi juu ya kile walicho na uhakika nacho, na kwa upande mwingine wa karatasi waandike vitu ambavyo hawana uhakika navyo pamoja na maswali yoyote wanayoweza kuwa nayo. Kwake, sio muhimu wakubaliane juu ya kitu, lakini anataka majadiliano yaliyochangamka juu ya yanayodhaniwa kuwa ni matumizi yake na umri wa kitu hicho.

## Shughuli ya 1: Kuwa mtaalamu wa historia wa kutumia kazi za sanaa

**Rejea nyenzo 1** : kutumia kazi za sanaa darasani kabla ya kuanza kipindi.

Waamuru wanafunzi kuleta vitu vyovyote vya kitamaduni walivyonavyo majumbani. Waambie unataka kitu kilicho cha zamani kadili inavyo wezekana, labda kilichotumiwa na babu zao au nyuma yao. Lakini wasisitize kuvitunza kwa uangalifu visiharibiwe. Kuwe na meza tayari kwa kuviweka pindi wanafunzi watakapoleta siku ya pili.

Waeleze wanafunzi wako kuwa watakuwa wataalamu wa kuunganisha pamoja ushahidi na taarifa nyingi iwezekanavyo kuhusu vitu vyao.

Watake katika jozi waangalie kazi za sanaa zote na kuziita majina na kuorodhesha katika daftari zao. Kwa kuangalia na kushika, watake kuandika wanachofikiri kimetumika kuzitengeneza, jinsi kilivyotengenezwa na matumizi yake. Unaweza kuwapa karatasi kwa matumizi hayo.

Angalia kazi za sanaa kama darasa kwa zamu na jadili mawazo juu ya sanaa hizo. Kubaliana na wazo lililotolewa na wengi na mtake aliyeleta hicho kitu aeleze anajua nini juu yake. Au wapeleke nyumbani na baadhi ya maswali ya kuuliza na kuleta majibu kwa lengo la kushirikishana na wengine siku inayofuata.

## Somo la 2

Moja ya malengo ya kufundisha historia kwa wanafunzi wako ni kuwawezesha kujielewa na kujigundua na kuelewa utambulisho wa jamii zao. Kama mwalimu wa mafunzo ya jamii, hata kama wa shule za msingi unatakiwa kutafuta njia zinazovutia za kuwasaidia wanafunzi kujua ya kale na historia yao. Kwa kuzingatia namna utamaduni wao, shughuli za kila siku na vitu vitumikavyo vilivyobadilika husaidia kujenga utambulisho huu.

## Uchunguzi kifani ya 2: Mafunzo ya mavazi ya asili

Bibi Ndonga amewaalika wazee wawili kutoka katika jamii kuja darasani wakiwa na mavazi yao ya asili na kuzungumza kuhusu nini kimebadilika kwenye mavazi ya asili tangu utoto wao.

Kabla ya ziara, Bibi Ndonga husoma **Nyenzo muhimu: matumizi ya jamii/mazingira ya mahali kama nyenzo muhimu; na** pamoja na wanafunzi wake, huandaa ziara hiyo. Mara wakikubaliana kuhusu muda na tarehe, wanafunzi huandaa maswali ya kuwauliza wageni juu ya kile kilichobadilika kulingana na wakati.

Siku ya ziara, darasa linapangwa na baadhi kwenda kuwakaribisha wageni. Darasa limesisimuka lakini lina aibuaibu kwa wageni. Hata hivyo, wageni wamefurahishwa kuja na kuongea. Pia na kwamba kila mmoja alitulia na kukawa na mjadala mzito juu ya mavazi waliyovaa na umuhimu wa kila kipande cha nguo hizo. Pia wageni walileta baadhi ya mavazi ya asili waliyotumia wazazi wao ili watoto wayaone.

Baada ya wageni kuondoka, Bibi Ndonga anawauliza wanafunzi kuhusu kitu kipya walichojifunza na anashangazwa na kuridhishwa kwa namna wanavyo kumbuka na kulipenda tukio hilo.

## Shughuli ya 2: Uchunguzi wa utaalam/ujuzi wa asili

Shughuli hii inalenga kuweka mwongozo, kama mwalimu, unaweza kutumia kufanyia mjadala darasani kuhusu dhana yoyote ya mafunzo ya jamii au historia. Kwa maana hiyo, tunaangalia kazi za sanaa na matumizi yake ya asili.

Waandalie wanafunzi wako ziara ya kumtembelea fundi asilia au waalike shule kuongea na wanafunzi kuhusu ufundi wao wa sasa na namna ulivyokuwa siku za nyuma.

Kabla ya ziara utahitaji kupanga tarehe na muda na nini unataka kuongelea, ili wageni wajiandae nini cha kuleta.

Halafu, pamoja na wanafunzi wako amua ni vitu gani wanataka kuvijua na maswali gani wanataka kuuliza kuhusu kazi za sanaa ambazo wageni wanaweza kuwaonyesha au kuviona wakati wa ziara yao. Inawezekana wageni wakafanya maonesho mbele ya darasa.

Siku ya ziara, waambie wanafunzi wafurahie ziara na kuwaheshimu wakubwa.

Katika kipindi kinachofuata, jadili matokeo ya utafiti na watake wanafunzi katika makundi ya watu wanne kuchagua kitu kimoja kukichora na kuandika wanachokiweza kuhusiana nacho kutokana na kumbukumbu na dondoo walizochukua.(rejea nyenzo muhimu : Matumizi ya kazi za makundi darasani.)

Watake wanafunzi kuweka kazi zao ukutani ili wote wazione na kusoma

Unaweza kuandaa kipindi cha ufundi pamoja na wageni ili wanafunzi waweze kufanya kwa vitendo.

## Somo la 3

Daima, historia inaweka usawa kati mawazo au maoni ya watu binafsi dhidi ushahidi halisia. Unapojifunza kazi za sanaa badala ya ushahidi simulizi na maandishi uwiano uleule hujitokeza. Kuna vitu halisi ambavyo vinaweza kuongelewa kwa mfano chungu yaani umbo lake, kimetengenezwa kwa kutumia nini, n.k. kitu kama matumizi yake inaweza kuwa ni udadisi tu kuzingatia matumizi yake kwa sasa. Kwa kuangalia chungu kwa umakini unapochunguza michoro ya zamani na upigwaji wa rangi na kuzungumza na wengine tunaweza kujenga picha fulani kuhusu matumizi ya chungu siku za nyuma.

Sehemu hii inatafiti njia za kusaidia wanafunzi kudadisi fikira na uelewa wao kuhusu kazi za sanaa.

## Uchunguzi kifani ya 3: Tafsiri ya matukio ya kihistoria kwa kutumia herufi zikiwa kama kazi za sanaa.

Bibi Marwa kutoka Shinyanga huamua kutumia kitabu cha herufi juu ya namna watoto wanavyokumbuka uasi wa Soweto mwaka 1976. Amepanga kutumia kitabu cha *Mbwa Wawili na Uhuru* kama kitabu cha kiada kwa ajili ya kipindi. Anachukua baadhi ya barua fupi kuhusu uzoefu wa watoto kuhusu uasi huo. Baada ya kujifunza hili kwa uangalifu, Bibi Marwa anatambua kuwa barua zile zilikuwa ni maoni ya watu binafsi na alifikiri kuwa ni vizuri kulinganisha maoni hayo na ushahidi halisi wa kihistoria wakati wa kipindi. Kwa hiyo Bibi Marwa alikusanya na kupanga nyaraka na vitabu vya historia vinavyochunguza migogoro ya Kitongoijo cha Soweto katika miaka ya 1970. Alitengeneza majumuisho ya mawazo muhimu ya kutumia darasani.

Kwanza, aliwataka kila kundi kusoma barua zilizochaguliwa na watoto ndani ya kitabu cha *Mbwa Wawili na uhuru* na kuwataka kuangalia jedwali la matukio muhimu na mawazo yaliyowasilishwa na wanahistoria. Je, wanaona ufanano au utofauti katika maelezo ya tukio moja? Wanajadili kama maoni binafsi katika kitabu yanashadidiwa na ushahidi halisi wa kihistoria uliowekwa na wanahistoria.

Wanakubaliana kuwa zote zinawiana kitabu ni mtazamo wa watoto na unaweza kutofautiana kutokana na imani zao, lakini jedwali linabakia kuwa na ukweli.

Mwishoni, Bibi Marwa hutoa majumuisho ya utofauti kati ya ushahidi wa maoni binafsi na ushahidi halisi katika kujifunza ya kale.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Shughuli muhimu: Maonyesho ya baadhi ya historia yetu

Watake wanafunzi wako kuleta vitu vya zamani walivyo navyo majumbani-kama mavazi ya asili, vyombo vya kupikia, kazi za miti, vinyago, shanga, vyungu n.k

Kumbuka kwamba kwa wanafunzi wako vitu vya miaka ya 20 au

30 tu vitaonekana kama vya zamani sana. Sehemu muhimu ya zoezi hili ni kwa wao kukusanya ushahidi juu ya kazi za sanaa na kwa kuangalia vitu vingi vya zamani, kukuza baadhi ya mawazo ya jinsi maisha ya zamani yalivyokuwa. Kama unaweza hakikisha kuwa umekusanya baadhi ya vitu ili uweze kuonyesha kwa wale ambao hawana uwezo wa kuleta chochote.

Watake wanafunzi wako katika jozi kutengeneza ukurasa ( **rejea nyenzo 2: kazi zangu za kisanaa** ) kuonyesha pamoja na kazi za sanaa.

maonesho yakiwa tayari, waalike wanafunzi wengine kutembelea maonesho yako. Unaweza kuwaalika hata wazazi na jamii inayowazunguka kuja kuona maonesho. Unaweza kupata mawazo mengine kutoka kwa waalikwa kuhusu baadhi ya kazi zako za sanaa.

## Nyenzo-rejea ya 1: Matumizi ya kazi za sanaa darasani

**Taarifa za msingi/welewa wa somo wa mwalimu utangulizi**

Nafasi ya kushika kazi halisi za sanaa ni uzoefu pekee. Kwa sababu ambazo hakuna mwenye uhakika nazo, kitendo cha kushika kitu ambacho dhahiri kina historia na hadithi yake, huhamasisha kila mmoja. Bila shaka wanafunzi watakuwa wadadisi juu ya kazi za sanaa na hii itapelekea kuwa na mjadala mzuri.

Kushika kazi ya sanaa huwafanya wanafunzi kutumia hisia zao kukuza udadisi na ujuzi wa kutatua matatizo, kuimarisha uelewa wao wa wakati ule na kuwajali watu wa kale.

**Nini lengo la kipindi cha kazi za sanaa?**

Vipindi vya kazi za sanaa vinaweza kutumika kwa:

- kuwapa motisha wanafunzi mwanzoni mwa mada;
- kuwavutia na kuvuta usikivu wa wanafunzi
- kupanua ufahamu wao juu ya mada wanayojifunza
- kuwapelekea kujifunza kiundani na kwa mapana zaidi
- Kusimama kama daraja kati ya baadhi ya masomo tofauti na vitu vinavyozungumziwa
- Kupembua ukuaji wa ufahamu wa wanafunzi mwishoni mwa kipindi. Maswali gani niulize wakati wa kipindi cha kazi za sanaa?

Aina ya maswali unayouliza yatategemea ni kazi gani ya sanaa unatumia. Maswali ya hapa chini yatakusaidia kupata majibu ya kazi za sanaa.

**Maswali kuhusu tabia za wazi za kitu**

- Inaonekanaje? Hisia, harufu na sauti yake?
- Ni kikubwa kiasi gani?
- Kina umbo gani?
- kina rangi gani?
- Kina uzito gani?
- Je kina alama yoyote inayotuonyesha namna kilivyotengenezwa, kilivyo tumiwa au kutunzwa?
- Kimetengenezwa kwa kutumia nini?
- Ni cha kawaida au chakipekee?
- Ni kizima au sehemu ya kitu chote?
- Je kipo katika hali nzuri au kimechakaa?
- Je, kimebadilishwa kimeigwa, kimerekebishwa au kimegeuzwa?

**Maswali kuhusu ubunifu na matengenezo ya kitu**

- Kimetengenezwa kwa vifaa gani?
- Kwanini vifaa hivyo vilichaguliwa?
- Je vifaa tofauti vingetumika?
- Kinavutia kukiangalia?
- Kinaweza kuwa kilitengenezwa lini na wapi?
- kilitengenezwa kwa mkono au kwa mashine?
- Nani anaweza kuwa alitengeneza?
- Kimetengenezwa katika kipande kimoja au vipande tofauti?
- Kinaweza kuvunjwa vipande vipande?
- Kimeunganishwaje?
- Kinawezaje kufanya kazi?
- Kimerembwa au kawaida?
- Kuna alama zozote/taswira kwenye kitu?
- Hivi vinatuambia nini kuhusu watu waliokitengeneza au wanaokimiliki na wakati tunapojifunza?

**Maswali kuhusu umuhimu na thamani ya kitu**

- Kifaa hicho kilileta utofauti gani katika maisha ya watu?
- Kilikuwa na umuhimu gani: watu waliokitengeneza au waliokimiliki; watu wa leo?
- Kinatuambia nini kuhusu watu waliokimiliki?
- Kimetengenezwa kwa wingi, mara chache au kwa upekee?
- Ni muhimu kiuchumi/kihistoria/kiutamaduni?
- Ni kwa namna gani ni muhimu leo?

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

**Maswali kuhusu kazi ya kifaa**

- Ni nini?
- Kwa nini kilitengenezwa?
- Jinsi gani kinaweza kuwa kilitengenezwa?
- Nani anadhaniwa kukitumia?
- Ujuzi gani ulihitajika kukitumia?
- Kingeweza kutumiwaje?
- Wapi kinadhaniwa kutumiwa?
- Je kinadhaniwa kutumiwa na vitu vingine?
- Matumizi yake yamebadilika?

**Kufundisha kwa kutumia vitu-baadhi ya mbinu**

Baadhi ya mbinu zilizoelezewa hapo chini zinaweza kutumiwa na wanafunzi wakati wa kusoma nyaraka, machapisho na rangi. kichokoo kinachoonekana

Vitu vinaweza kutumika kuanzisha majadiliano mwanzoni mwa kipindi. Vitu hivyohivyo vinaweza kutumika kurejea walichojifunza wanafunzi na kuona kama moja ya mawazo na ufahamu wao umebadilika kutokana na kipindi hicho.

utafiti wa kihistoria

Uchaguzi wa vitu unaweza kutumika na wanafunzi kwa mazoezi ya utafiti kihistoria-kupata taarifa kutoka vyanzo. Wape muda wanafunzi kuona vitu kwa umakini kabla ya kutafiti baadhi ya maswali yafuatayo:

- Kimetengenezwa kwa kutumia nini?
- Vifaa au mbinu gani zilihitajika kukitengeneza?
- Nani anadhaniwa kukitengeneza?
- Je kulihitajika ujuzi wa kipekee kukitengeneza?
- Kimerembwa? Namna gani?
- Nani anadhaniwa kukitumia?
- Kilikuwa ni kwa matumizi gani?
- Je kilifanya kazi au kilitumika kwa njia nyingine?
- Kinauzito au ukubwa kiasi gani?
- Ni cha muhimu au kitu adimu?

**Kulinganisha na kuvihusianisha vitu**

Tumia vitu viwili au taswira kwa pamoja na watake wanafunzi kulinganisha, kutafiti ufanano na utofauti kati ya vitu na taswira. Tumia makundi ya vitu na ongelea uhusiano kati yao.

Uwakilishi na ufasiri

Baadhi ya kazi ya sanaa zinaweza kuonyesha ushahidi wa mtazamo fulani. Nani alitengeneza kitu hicho na kwa malengo gani? Ni kitu halisi au propaganda tu? Kinatupa habari yote? Kinatuambia nini?

**Shughuli nyingine zitumiazo vitu ni**

**Shughuli za utabiri**-waonyeshe wanafunzi kifaa na watake kufikiria kipindi gani cha kihistoria kinahusiana na kifaa hicho.

**Uchunguzi kifani**-wanafunzi wanaweza kutumia kitu kimoja au vingi kujenga uchunguzi kifani, kwa mfano maisha ya Afrika Mashariki kabla ya kuja Waarabu.

**Makundi-**wanafunzi wanaweza kukusanya vitu katika jozi zinazokuwa na vitu fulani vinavyofanana (kama vifaa fulani, nchi vinakotoka, namna vilivyotumika). Wanafunzi wanaweza kufikiria namna ya kutengeneza makumbusho kwa kuweka vitu katika makundi na kwa namna tofauti.

Uandishi wa kichwa cha habari-wanafunzi wanaweza kuandika vichwa vyao vya habari au alama za maonyesho, au kutoka mtazamo wa kisasa au kama walikuwa wanandika kwa muda huohuo wakati kitu kinatengenezwa.

Hisia zenye ufahamu-wanafunzi wanaweza kuorodhesha sifa zinazoelezea namna wanavyojisikia kuhusu kitu, wakionyesha ufahamu na kuguswa juu ya vitu husika.

Majibu ya ubunifu-wanafunzi wanaweza kuitikia vitu kupitia ubunifu, tamthilia au sanaa za maonyesho.

**Ni masomo gani yanaweza kusaidiwa na matumizi ya kazi za sanaa?**

kujifunza kutokana na vitu ni msaada kwa somo katika mitaala mbalimbali

- Historia: ufahamu wa mtiririko, hisia na ujuzi wa msingi
- Sayansi: tabia za vitu, uchunguzi, kulinganisha, mchanganuo, na ujuzi wa kudadisi.
- Kingereza: kuuliza na kujibu maswali, nyenzo za muktadha.
- Tamthilia: nyenzo chokoo, kujenga hisia
- Sanaa na ubunifu: nyenzo chokoo, nyenzo za muktadha

## Nyenzo-rejea ya 2: Sanaa zangu

**Matumizi ya wanafunzi**

Jina la mwanafunzi

Kazi ya sanaa yangu

Sanna hii imeundwa kutokana na

Sanaa hii ilitumika kwa

Hivi ndivyo sanaa hii ilivyotumika

Hivi ndivyo sanaa ya zamani inavyodhaniwa kuwa

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

TESSA

Teacher Education in Sub-Saharan Africa

www.tessafrica.net

Rasilimali za Msingi

# Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa

## **Namba ya moduli 3** Kuangalia sanaa

**Sehemu ya 1** Kuchunguza Kazi za Sanaa zionekanazo

**Sehemu ya 2** Kuandaa Shughuli za Sanaa kwa Vitendo-

**Sehemu ya 3** Kutumia ngoma kujifunza

**Sehemu ya 4** Kutumia muziki darasani

**Sehemu ya 5** Sanaa ya kuhadithia hadithi

**KISWAHILI**

*TESSA (Teacher Education in Sub-Saharan Africa) inalenga kuboresha utekelezaji darasani wa walimu wa msingi na walimu wa sayansi wa sekondari barani Afrika kupitia matoleo ya Rasilimali Huria za Elimu (OERs) ili kuunga mkono walimu kuunda njia zinazowalenga wanafunzi na kuwashirikisha. OER ya TESSA huwapa walimu kitabu cha kurejea pamoja na vitabu vya shule. Zinatoa shughuli kwa walimu kujaribu madarasani pamoja na wanafunzi wao, pamoja na masomo ya utafiti inayoonyesha jinsi walimu wengine wamefunza mada hiyo, na rasilimali husishi za kuwaunga mkono walimu katika kukuza mipango ya masomo yao na ufahamu wa somo.*

OER ya TESSA imeandikwa kwa ushirikiano wa waandishi wafrika pamoja na wa kimataifa *ili kushughulikia mtalaa na muktadha. Zinapatikana kwa matumizi ya mtandaoni na chapa (*http://www.tessafrica.net*). OER Msingi zinapatikana katika matoleona lugha kadhaa (Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu na Kiswahili). Mara ya kwanza, OER ilitolewa kwa Kiingereza na kupatikana Afrika nzima. OER hizi zimebadilishwa na washirika wa TESSA ili kufaa Ghana, Nijeria, Zambia, Rwanda, Uganda, Kenya, Tanzania na Afrika Kusini, na kutafsiriwa na washirika nchini Sudani (Kiarabu), togo (Kifaransa) na Tanzania (Kiswahili) OER ya Sayansi ya Sekondari zinapatikana kwa Kiingereza na zimebadilishwa ili kufaa Zambia, Kenya, Uganda na Tanzania. Tunakaribisha maoni kutoka kwa wale wanaosoma na kutumia rasilimali hizi. Leseni ya uundaji wa ubunifu huwawezesha watumiaji kuchukua na kujanibisha OER zaidi ili kutimiza mahitaji na muktadha wa kindani.*

*TESSA inaongozwa na Open University, Uingereza, na inafadhiliwa kwa sasa na ruzuku za ufadhili kutoka kwa Wakfu wa Allan and Nesta Ferguson, Wakfu wa William and Flora Hewlett na Open University Alumni. Orodha kamili ya wafadhili inapatikana kwenye tovuti ya TESSA (*http://www.tessafrica.net*).*

*Pamoja na rasilimali kuu za mafundisho za kuunga mkono mafunzo katika masomo maalum, ni chaguo za rasilimali za ziada ikiwa ni pamoja na sauti, rasilimali kuu ambazo zinafafanua utendakazi, vitabu na zana maalum.*

**TESSA Programme**
**The Open University**
**Walton Hall**
**Milton Keynes, MK7 6AA**
**United Kingdom**

**tessa@open.ac.uk**

Copyright © 2017 The Open University
Except for third party materials and otherwise stated, this content is made available under a Creative Commons Attribution-Share Alike 4.0 licence: http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0/. Every effort has been made to contact copyright holders. We will be pleased to include any necessary acknowledgement at the first opportunity.

***TESSA_SwPA_SCI_M3 August 2017***

*This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Share Alike 4.0 License*

# Contents

Sehemu ya 1: Kuchunguza Kazi za Sanaa zionekanazo 5
Somo la 1 5
Somo la 2 7
Somo la 3 8
Nyenzo-rejea ya 1: Kazi ya nyumbani ya kuorodhesha kazi za ughushi za mahali hapo 10
Nyenzo-rejea ya 2: Kazi ya nyumbani ya kuorodhesha kazi za ughushi za mahali hapo 11
Nyenzo-rejea ya 3: Kinyago cha kiafrika 12
Nyenzo-rejea ya 4: Andalio la somo kuhusu vinyago vya Afrika ya Mashariki 13
Sehemu ya 2: Kuandaa Shughuli za Sanaa kwa Vitendo 15
Somo la 1 15
Somo la 2 17
Somo la 3 18
Nyenzo-rejea ya 1: Maswali ya utafiti juu ya vifaa vya jadi na kazi zake 19
Nyenzo rejea 2: Tathimini ya mawasilisho ya utafiti 20
Nyenzo rejea 3: Kutengenza vyungu 21
Sehemu ya 3: Kutumia ngoma kujifunza 24
Somo la 1 24
Somo la 2 26
Somo la 3 27
Nyenzo-rejea ya 1: Hadithi za ngoma ya Venda 29
Nyenzo-rejea ya 2: Mila za kienyeji: Mbinu za kuchezangoma katika Tanzania 30
Nyenzo rejea 3: Kuboresha ngoma zetu 31
Nyenzo rejea 4: Kutafakari juu ya ngoma 32
Sehemu ya 4: Kutumia muziki darasani 33
Somo la 1 33
Somo la 2: Kufanya kazi katika vikundi ili kutunga ushairi wa wasifu yaani utenzi 35
Somo la 3 36
Nyenzo-rejea ya 1: Kugundua sauti 37
Nyenzo-rejea ya 2: Kutengeneza zana 38
Nyenzo rejea 3: Kusikiliza sauti katika maisha ya kila siku 40
Nyenzo rejea 4: Kusifu uimbaji 41
Nyenzo rejea 5: Nyimbo za kusifu za mwanafunzi 42
Nyenzo rejea 6: Kutengeneza muziki 43

Sehemu ya 5: Sanaa ya kuhadithia hadithi 47
Somo la 1 47
Somo la 2 49
Somo la 3 50
Nyenzo-rejea ya 1: Sauti ya kiwavi 52
Nyenzo-rejea ya 2: Hadithi na hekaya kutoka Afrika 53
Nyenzo-rejea ya 3: Picha za hadithi 54
Nyenzo rejea 4 : Kutumia picha kama kichokoo cha kuandika hadithi 55

# Sehemu ya 1: Kuchunguza Kazi za Sanaa zionekanazo

**Swali Lengwa muhimu:** Unachunguzaje sanaa za maonyesho na wanafunzi wako?

**Maneno muhimu:** sanaa; vinyago; maonyesho; ughushi; ujuzi wa kufikiria; ufundi

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- Umejijengea ujuzi wa kuendesha shughuli za darasani na majadiliano yanayohusu eneo la sanaa zinazoonekana;
- Umejenga uelewa wa wanafunzi juu ya sanaa zinazoonekana ambazo zinatengenezwa na kutumika katika jamii;
- Umefanya kazi ya sanaa kwa vitendo na wanafunzi wako.

## Utangulizi

Baadhi ya sehemu zinazofurahisha sana katika urithi wa jamii ni sanaa zake na ufundi wa jadi. Jinsi hivi vitu vya mapambo na vya kila siku, vinavyotengenezwa na kupambwa, na muziki na michezo inayotolewa, vinatoa mwelekeo wa thamani halisi na mahitaji ya jamii.

Sehemu hii itakuonyesha jinsi ya kuwahusisha wanafunzi wako na kazi za sanaa zionekanazo zinazowazunguka na jinsi ya kutumia hizi sanaa kuamsha ubunifu darasani kwako.Kazi yako ni kuwasaidia wanfunzia kuelewa kuwa kazi za sanaa hufanya mazingira yavutie. Vilevile,utahitaji kujenga uelewa kuwa sanaa ni njia ya mawasiliano na ni njia ya kueneza utamaduni.

## Somo la 1

Uchunguzi wa sanaa na ughushi na jinsi vinavyotengenezwa unaweza kutoa mwanga kwa wanafunzi juu ya utamaduni wao na historia ya jamii. Pia, inakupa wewe, mwalimu, nafasi ya kubuni vizuri masomo kwa vitendo, kwa sababu kuna vitu vingi sana vya kusisimua na kazi za sanaa ambazo zinaweza kuletwa darasani kuamsha utashi, pamoja na kutoa mawazo kwa kazi za sanaa za wanafunzi.

Alama ambazo zinapatikana kwenye sanaa, mara nying zinahusiana na uadilifu na dini za jamii husika. Kwahiyo, ni muhinu kuwahimiza wanafunzi wako kuipenda sanaa-kuhifadhi urithi wao wa utamaduni na wasaidie waimaanishe katika mazingira yao. Hii ndiyo sababu tunawafundisha wanafunzi kuhusu sanaa.

## Uchunguzi kifani ya 1: Kufikiria juu ya ughushi wa mahali hapo

Siku moja kabla ya somo la kwanza juu ya sanaa za asili, Bi. Kabalimu, kutoka mkoa wa Tanga Tanzania, aliwaambia wanafunzi wake watengeneze orodha ya ughushi unaotengenezwa katika jamii yao,iwe zamani au sasa. Walikuwa waongee na wazazi wao au majirani ili kupata hizi habari. Ili kuwafanya waanze kufikiria, aliwaonyesha baadhi ya mifano

ya ughushi, kama vile kikapu cha kusukwa kizuri cha Kimakonde na shanga za kuvaa shingoni za Kimasai.

Siku iliyofuata, wanafunzi waliteta orodha-Bi. Kabalimu alipitia kila moja na kuirudisha (angalia **Nyenzo rejea ya muhimu 1: Kazi ya nyumbani ya kuorodhesha ughushi wa mahali hapo** ). Alianza somo kwa kuwaambia wanafunzi wataje majina ya ughushi waliyojifunza, ambayo aliyaandika ubaoni. Yalikuwemo majina ya uchongaji, upakaji rangi na

michoro mbalimbali, silaha, vifaa vya nyumbani na vishirikishi. Bi. Kabalimu aliligawa darasa katika makundi madogo (angalia **Nyenzo rejea ya muhimu: Kutumia makundi darasani kwako** ) na kulipa kila kundi majina ya vitu viwili vya sanaa na maswali yafuatayo:

Elezea matumizi ya hivyo vitu.

Ni ujuzi gani unahitajika kutengeneza vitu hivyo? Ujuzi huu unafahamika kwa watu wengi?

Jinsi gani vitu hivi vinaweza kutunzwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya vizazi vijavyo?

Baada ya dakika 15, kila kundi liliwasilisha majibu yake kwa darasa zima. Bi. Kabalimu alitengeneza muhtasari kwenye makaratasi makubwa, na kwa kufanya hivyo, alijumuisha mawazo ya wanafunzi katika vipengele mbalimbali. Alitambua kuwa ilikuwa ni muhimu kuyajumuisha mawazo kulingana na jinsi yalivyopangwa.

Hizi karatasi zilibandikwa kwenye ubao wa matangazo wa darasa na kuachwa kwa muda wa juma moja ili wanafunzi wajifunze. Sio tu kwamba wanafunzi walikuwa wanajifunza kuhusu ughushi kwenye jamii yao, pia walikuwa wanapewa nafasi ya kujenga uwezo wa kufikiri.

## Shughuli ya 1: Kuchangia mazwazo na kutengeneza sanaa za jadi na ughushi

Unaweza kuangalia katika mchoro Nyenzo rejea muhimu 2: makundi ya kuandaa aina za kazi za mikono na ughushi kukusaidia kupangilia somo hili

Kwenye majadiliano darasani, waambie wanafunzi wafikirie juu ya vitu vya sanaa asilia na ughushi wanavyovifahamu. Anza kwa kutoa mifano.

Jinsi wanafunzi wanavyotoa mawazo, yaandike ubaoni katika vipengele mbalimbali (angalia Nyenzo rejea muhimu 2).

Chunguza kila kifaa kilichosemwa kuwa ni sanaa ya uchongaji na liambie darasa lijadili ujuzi unaotakiwa ili kutengeneza hivyo vifaa, ni vipi na wapi vilitengenezwa, na ni jinsi gani vinasafishwa na kuhifadhiwa.

Fanya hivyo na kwa vipengele vingine, kwa vitu vingi kadri muda utakavyoruhusu.

Maliza somo kwa kuwaambia wanafunzi juu ya kipindi kingine cha sanaa, ambapo watachora picha au kutengeneza baadhi ya vitu. Tafuta sehemu ambapo vitu hivi vitaweza kuonyeshwa kulingana na vipengele vyake. Baadae vinaweza kuwa ni sehemu ya maonyesho ya shule.

# Somo la 2

Vinyago vya jadi vya Kiafrika vilifikiriwa kuwa ni vitu vya muhimu sana kwa sababu vilifanya kazi muhimu ya mizimu katika imani za Kiafrika. Kusudi la kwanza la kutengeneza vinyago vya Kiafrika lilikuwa ni kwa ajili ya sherehe maalumu au shughuli muhimu za kijamii. Si kama Ulaya Magharibi amabako vinyago vilichukuliwa kama njia ya "kuuwakisha" mzimu, vinyago vya Kiafrika vilieleweka kuwa pale ambako mzimu "uliumbwa".

Kwa maneno mengine, pale ambapo mtu anavaa kinyago, pamoja na vazi ambalo limefunika kuanzia kichwani hadi miguuni, mtu huyo kwa kweli "anakuwa" ni mfano wa mzimu amabao umekusudiwa kuwakilishwa, ukipewa uhai kwa kupitia ishara, sauti, shughuli mbalimbali na hata hali yao ya kupagawa.

Katika **Uchunguzi kifani 2**, mwalimu hutumia kazi za vikundi kuwawezesha wanafunzi wake kufikiri na kuwaruhusu kubadilishana mawazo juu ya madhumuni ya vinyago tofauti. Katika shughuli **2**, wanafunzi wako watatengeneza vinyago vyao wenyewe, wakiwa wametafakari maswali kama yale yaliyoulizwa kwenye uchunguzi kifani.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kuchunguza alama na maana kwenye vinyago vya jadi vya Kiafrika

Bi. Sungi ni mwalimu wa sanaa katika shule ya Ihanja, mkoa wa Singida. Ameamua kufanya uchunguzi wa vinyago vya jadi vya Kiafrika akiwa na mitazamo mitatu akilini mwake:

Kuangalia juu ya uzoefu na matumizi ya kazi za sanaa Afrika nzima. Kuchunguza jinsi alama zilizo kwenye kazi ya sanaa zinavyopeleka maana halisi katika mtazamo wa kiutamaduni.

Kuwasaidia wanafunzi wake kutengeneza vinyago vyao wenyewe. Anapanga kutumia kama vipindi viwili vinavyofuatana vya somo la sanaa ili kufikia malengo yake.

Bi. Sungi anaanza kwa kuwaonyesha wanafunzi wake vitabu vya picha na majarida yaliyo na picha za vinyago vya jadi kutoka eneo lote la Afrika, kusini mwa jangwa la sahara. (Angalia **Nyenzo rejea muhimu 3: Kinyago cha Afrika** kwa mfano.)

Analiambia darasa, likiwa katika makundi, kuchunguza baadhi ya vitabu kwa pamoja na kupata matumizi ya kawaida ya vinyago katika maisha ya kijamii kwenye mazingira tofauti ya kiutamaduni. Kila kundi linaandaa orodha ya matambiko na kazi za kiutamaduni za vinyago vya Kiafrika.

Kwa kutumia **Nyenzo rejea muhimu 4: Andalio la somo la vinyago vya Afrika ya Mashariki** , Bi. Sungi anaendelea kuonyesha vinyago maalumu kutoka Afrika Mashariki, ambavyo ni vya mitindo mingi sana ikiendana na matambiko na ishara ya uwezo. Anakazia kwenye alama muhimu za vinyago. Baadaye anawapa wanafunzi wake muda wa kutengeneza vinyago vyao wenyewe.

## Shughuli ya 2: Kutengeneza vinyago vinavyowakilisha hisia na ujumbe wa jamii

Kabla ya somo, kusanya pamoja vitabu vya picha na majarida yenye vinyago vya Kiafrika kutoka sehemu mbalimbali na, ikiwezekana, baadhi ya mifano ya vinyago halisi vya mahali hapo.

Waambie wanafunzi waziangalie nyenzo rejea muhimu ulizozikusanya kupata mwelekeo wa vinyago vyao wenyewe.

Wanavyopangilia vinyago vyao, wanafunzi wanahitaji kufikiria ni ujumbe gani wanataka vinyago vyao vibebe. Wakumbushe kuwa wanatakiwa kufikiria juu ya:

Alama za usoni; alama wanazoweza kutumia; jinsi ya kuteka hisia; rangi.

Waambie wapangilie vinyago vyao katika vipande vidogo vya karatasi/kadi kwanza, kabla ya kutengeneza picha kubwa au mfano wa vinyago kutokana na kadi hizo hizo.

Itabidi uwape vipindi vya sanaa kadhaa kwa ajili ya kazi hii. Onyesha vinyago vyilivyokamilika ili wote waone na alika madarasa mengine yaje yaone.

## Somo la 3

Kutengeneza ughushi wao wenyewe ni muhimu kwa wanafunzi wako na watataka kushirikisha mafanikio yao kwa watu wengine. Katika sehemu hii, tunashauri kuwe na maonyesho shuleni ya ughushi na vitu vingine ambavyo vimetengenezwa na wanafunzi kama njia ya kuendeleza na kuhifadhi fahari ya wanafunzi wako katika urithi wao wa utamaduni. Ughushi kutoka kwenye jamii ya hapo ambao hauwezi kubebeka au haupatikani unaweza kuonyeshwa kwa kutumia picha zilizokatwa kutoka magazetini na vyanzo vingine.

**Uchunguzi kifani 3** unaonyesha jinsi darasa moja, likifanya kazi kwa makundi, lilivyojihusisha kwenye hatua zote za maonyesho, kutoka

kwenye kuyaandaa hadi kuongea na wageni. Kwenye **Shughuli muhimu**, wanafunzi wako wataandaa onyesho ambalo wageni watatembelea bila wenyeji, hivyo kazi ya kuweka alama zinazojieleza na za kuvutia ni muhimu sana.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kuonyesha ughushi shuleni siku isiyo ya masomo

Siku ambazo si za masomo za shule ya msingi ya Ilemela kwa kawaida hufanyika kuelekea mwishoni mwa mwaka wa shule. Bwana Koku, amabaye ni mwalimu wa sanaa wa wanafunzi wa drasa la nne, aliiambia kamati ya maandalizi ya siku hiyo kuweka sehemu kwenye chumba cha maonyesho ili darasa lake lionyeshe ughushi waliotengeneza darasani au waliokusanya kutoka vyanzo mbalimbali katika jamii. Ombi lake lilikubalika.

Katika kipindi cha maandalizi, Bwana Koku aliliongoza darasa lake kuandaa maonyesho. Aliwagawa wanafunzi katika makundi manne. Kundi la kwanza lilitakiwa kukusanya na kuweka utambulisho kwenye michoro yote, picha na vitu ambavyo vilitambulika kama vifaa vya nyumbani. Kundi la pili lilipewa kazi kwa upande wa vifaa vya muziki, kundi la tatu lilipewa kazi kwenye sehemu ya usonara na kundi la nne lilipewa upande wa uchongaji.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Shughuli zote hizo zilichukua vipindi viwili. Katika kipindi cha tatu, kulikuwa na kuelezea makusanyo hayo darasani kama ambavyo mtu angeweza kuelezea kwa wageni. Siku ilipowadia, darasa lilionyesha vitu vikiwa vimepangwa katika makundi manne, na wanafunzi wanne wakitoa maelezo kwa wazazi na wanajamii wengine waliotembelea meza ya maonyesho ya darasa.

Mwisho wa siku, meza ya ughushi ilizawadiwa kikombe cha kuwa meza bora kwenye chumba cha maonyesho.

## Shughuli muhimu: Kuandaa maonyesho ya ughushi

Waambie wanafunzi wako walete darasani michoro, ughushi, vinyago, vyungu na vikapu iwe kutoka nyumbani au walivyotengeneza wakati wa vipindi vya sanaa.

Andaa kadi tano. Kwa kila kadi, andika moja ya maneno yafuatayo: wachoraji, wachongaji, wafinyanzi, mafundi seremala, wasusi. Ligawe darasa lako katika makundi matano na toa kadi moja kwa kila kundi.

Waambie kila kundi wachague vitu walivyoleta vinavyoendana na majina ya kadi zao na waviweke sehemu tofauti.

Baada ya hapo, yaambie makundi yalinganishe vitu. Majadiliano yatakayoendelea hapa ni muhimu kujenga uwezo wa wanafunzi wa kutofautisha na uwezo wa kufikiri; na pia yatasaidia kutambua mambo ya msingi wanayotaka kuyajumuisha kwenye utambulisho wa vitu.

Waambie kila kundi liandike jina na utambulisho wenye maelezo kwa kila kitu kwenye kundi lao.

Waambie kila kundi, wapange vitu vyao kwa ajili ya watu kuangalia, wakati wanafunzi wengine wakijifanya kuwa ni wageni. Waambie “wageni” watoe maoni yao ni jinsi gani makundi yangeweza kuboresha utambulisho wao.

Andaa labels za mwisho na lipe darasa lako muda wa kuandaa maonyesho.

Andaa orodha ya wanafunzi watakaojifanya wamekuja kutembelea maonyesho. Hii inaweza kufanyika muda wa mapumziko au muda wa chakula cha mchana tu.

Baada ya maonyesho,jadili na wanafunzi wako juu ya walichopata kutokana na uzoefu kwa misingi ya uelewa wa ughushi na kujihusisha kwao kwenye tukio kama hilo.

# Nyenzo-rejea ya 1: Kazi ya nyumbani ya kuorodhesha kazi za ughushi za mahali hapo


**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**


**Jabali 6B, 02.10.2005, Majina ya Ughushi**

| | |
|---|---|
| Ngoma | √ |
| Gitaa | Hili ni gitaa ulilotengeneza? |
| Kijiko cha mti | √ |
| Chupa | Fikiria tene. Hii chupa kweli ilitengenezwa katika jamii yako? |
| Chungu cha udongo | √<br>**Vizuri sana** |
| Mchoro wa tingatinga | Hii ni nini? |
| Gari la kuchezea watoto | Moja ya hiki kifaa kinatengenezwa kijijini kwako? |
| mkeka uliosukwa kwa mikono | √ |
| | Umfanya vizuri Jabali. Hapa umekusanya orodha nzuri ya ughushi. Hakikisha unaelewa ni zipi zinatengenezwa katika jamii yako. |

# Nyenzo-rejea ya 2: Kazi ya nyumbani ya kuorodhesha kazi za ughushi za mahali hapo


**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**



## Nyenzo-rejea ya 3: Kinyago cha kiafrika

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**



*Chanzo halisi: Cable, M. The African Kings. New York: Select Books*

# Nyenzo-rejea ya 4: Andalio la somo kuhusu vinyago vya Afrika ya Mashariki

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**



*Chanzo halisi: Masks of the World, Website*

Kwa jumla kuna aina tatu za vinyago; vya usoni, vya kichwani (ambavyo kama jina linavyooyesha vinavaliwa kichwani), na vya mwilini, ambavyo hufunika sehemu kubwa ya mwili wa mchezaji na vinategemewa kubadili mwonekano wake kutoka kwa watu wanaomfahamu. Vinyago vya mwilini wakati mwingine hufunika mwili tu na huvaliwa pamoja na vya usoni au vya kichwani.

Vinyago vyote huwakilisha mizimu au wazee waliokufa,na vilikuwa vikitumika sana kwenye sherehe za jando kama muonesho wa mwendelezo, hofu na uadilifu. Vilevile vilitumika kwenye ngoma na matukio ya sikukuu, kwa mfano sharehe za mavuno.

Vinyago vya kichwani (mapiko; umoja lipiko) vinafahamika sana kwa mfanano wake. Vingi vina nywele halisi za mwanadamu zilizonyolewa vizuri, nyuso nzuri na midomo ya wazi isiyokuwa na meno, masikio makubwa au vizibo vya mdomo. Vinatumika katika mchezo wa mapiko na michezo mingine. Japo kuwa vichwa vya wanaume na wanawake wote vinaweza kutumika, ni mara chache sana kuona vichwa vya wanawake. Mchezaji hupumua na kuona kupitia tundu dogo lililoko mdomoni.

Mapiko si jina linapewa kwa vinyago (kwa kawaida vya kichwani) tu, bali pia ni jina la ngoma, jina la nguvu inayotisha, na vilevile ni jina la moja kati ya hatua za unyago wa wanaume, wakati mhusika anapoingizwa kwenye siri za Mapiko. Vinyago vyenyewe vimetengenezwa katika sehemu ya siri porini inayojulikana kama Mpolo, ambayo wanawake wanakatazwa kupafikia. Pale vinapokuwa havitumiki, vinyago huwekwa

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Mpolo, na kijadi vilichomwa moto vilipovunjika au kubadilishwa na vingine vipya.

**Matokeo**

Wanafunzi watajenga tathmini mbalimbali za vinyago na watatengeneza vinyago;+

**Vifaa**

karatasi ya kuchorea

kadi

penseli

udongo

karatasi katika rangi anuwai

kalamu za rangi

rangi ya bango

shanga, magamba n.k

mkasi

gundi

1. Kusanya baadhi ya picha za vinyago za kuwaonyesha wanafunzi wako.
2. Jadili taswira za vinyago na uashiria wake.
3. Waambie wanafunzi watengeneze mchoro wa mwanzo wa kinyago.
4. Wafuatishie michoro kwenye kadi halafu wachore vinyago vyao. Waambie wanafunzi kuwa wanaweza kubadili baadhi ya vitu kwenye nyuso za vinyago vyao. Mfuatisho ni mwongozo tu wa mahali pa kuweka macho na mdomo endapo wangependa kuvivaa vinyago vyao.
5. Paka vinyago rangi na viache vikauke.
6. Toa vinyago na andaa vitu ambavyo vitaambatana navyo kama nywele na mkanda wa kukishikilia kichwani.
7. Wape wanafunzi muda wa kupamba vinyago vyao.

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

# Sehemu ya 2: Kuandaa Shughuli za Sanaa kwa Vitendo

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kuwasaidia wanafunzi kuuliza maswali kuhusu na kutengeneza sanaa ya mahali hapo?

**Maneno muhimu:** ustadi; utafiti; mawasilisho; vitendo; utamaduni

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- Umepata ni nini wanafunzi tayari wanajua juu ya ufundi wa mahali hapo;
- Umewapanga wanafunzi wako katika makundi madogo kufanya shughuli za kiutafiti;
- Umeandaa shughuli za vitendo ili kuwasaidia wanafunzi watengeneze na kutathimini vifaa vyao vya ufundi.

## Utangulizi

Wanafunzi wengi tayari watakuwa na uelewa juu ya ufundi wa mahali hapo na baadhi yao wanaweza wakawa na ujuzi mkubwa wa kutengeneza baadhi ya hivyo vifaa. Wigo wa ufundi mahali hapo unaweza kujumuisha vitu kama utungaji shanga, ufinyanzi, uchongaji, uchoraji na uhunzi.

Ni muhimu kutambua wanafunzi wanachokifahamu kwanza, na kutumia huo ufahamu kama msingi wa kupangilia shughuli kuzunguka ufundi wa mahali hapo. Katika sehemu hii, utawahimiza wanafunzi kuchangia mawazo na kujenga uelewa wao juu ya thamani na matumizi ya huu ufundi wa jadi. Njia mojawapo muhimu ni kuwaruhusu wanafunzi kutengeneze zana zao wenyewe; hii hutoa nafasi kwao kupangilia na kutathimini kazi zao.

## Somo la 1

Ufundi wa jadi wa jamii utakuwa na maana zaidi kwa wanafunzi wako kama utawahusisha katika kufanya baadhi ya hizi kazi za ufundi. Sehemu hii inaibua kile wanafunzi wako wanachoelewa juu ya ufundi wa mahali hapo pamoja na watu wanaotengeneza zana hizo katika mazingira ya vitendo. Inakupa wewe nafasi ya kujenga ujuzi wa kuuliza maswali, na inakuonyesha njia ya kuwasaidia wanafunzi wako kuuliza maswali yao wenyewe.

Uchoraji ni njia moja ambayo jamii nyingi zinaweza kurekodi matukuio ambayo yametokea. Vilevile ni njia ambayo hutumia kufikiria sana, hivyo ni nzuri kwa wanafunzi kuelezea mawazo na hisia zao.

**Uchunguzi Kifani 1** unaelezea jinsi mwalimu mmoja alivyowahimiza wanafunzi wake kupaka rangi na kuchora. Katika Shughuli **1**, unatumia majadiliano ya vikundi vidogo kuibua nini wanafunzi wanaelewa juu ya ufundi wa mahali hapo, matumizi yake na jinsi zinavyotengezwa. Hii inaweza kuwa ni hatua ya mwanzo ya kufanya utafiti zaidi juu ya ufundi katika shughuli itakayofuata.

## Uchunguzi kifani ya 1: Kuangalia michoro

Bi Moyosola kutoka kusini-magharibi mwa Nigeria alikuwa anafundisha upakaji rangi. Alitaka kulihimiza darasa lake kupaka rangi na kuchora. Aliamua kuanza kwa kuwaambia wanafunzi wake watazame baadhi ya picha zilizochorwa na wachoraji wa kisasa wa Nigeria kutoka katika eneo lao.

Alikuwa na nakala moja kwa kila picha aliyoaibandika ubaoni. Aliwaambia wanafunzi watazame hizo picha na waseme ni kitu gani walikipenda na kipi hawakukipenda. Aliwauliza kama mmoja kati yao aliwahi kupaka rangi au kuchora, na kama ndivyo, alipaka rangi au kuchora nini na lini. Wengi hawakuweza kuwa na karatasi na kalamu, lakini walisema huchora picha mchangani nje ya nyumba wanazoishi. Walisikitika kwa kuwa picha hizi hazikuweza kudumu.

Bi Moyosola aliwaambia wanafunzi wake wafikirie kitu ambacho wangependa kupaka rangi au kuchora. Aliwapa karatasi na penseli, na kuruhusu vipindi viwili vya sanaa wavitumie kwa kuchora na kupaka rangi. Wengi walichora picha zao wenyewe na wengine walifuatishia zile picha za kisasa za Nigeria.

Bi Moyosola alizionyesha hizi picha ili kila mmoja achangie mawazo.

## Shughuli ya 1: Kuuliza maswali juu ya ufundi wa mahali hapo

Kusanya baadhi ya mifano ya ufundi wa mahali hapo. Ungeweza kutumia mifano hiyo hiyo kwa makundi yako yote, au mfano tofauti kwa kila kundi.

Pangilia darsa lako katika makundi madogo ya wanafunzi wanne/watano.

Waambie kila kundi wajadili kitu wanachofahamu katika ufundi wa aina moja. Waambie waanze kwa kujibu maswali yafuatayo (yaandike maswali haya ubaoni).

Ni kitu gani? Kinatumikaje?

Kilitumikaje siku za nyuma? Kinatengenezwaje?

Wape wanafunzi dakika 10–15 kujadili haya maswali na kufikiria swali moja zaidi la kuuliza kuhusu ufundi. Ungeweza kuwaambia wanafunzi wakubwa wachore na kuandika mawazo yao kwenye mchoro.

Halafu, waulize baadhi ya majibu yao. Unaweza kukuta kuwa hawakujibu maswali yote, hivyo waeleze kuwa wataenda kufanya utafiti ili kukusanya habari zaidi katika **Shughuli 2**.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Somo la 2

Kuujadili ufundi wa mahali hapo au silaha za asili au mavazi inahamasisha sana kwa wanafunzi walio wengi kwa kuwa wanaweza kuona uhalisia wa vitu hivi katika maisha yao.Wanafunzi wanapovutiwa, inakuwa pia ni rahisi kwako kusimamia tabia zao. Kwenye Uchunguzi **kifani 2**, kuvutiwa huku kunasababishwa na mgeni. Unamfahamu mtu yeyote ambaye ana muda wa kutembelea darasa lako? Umewauliza wanafunzi kama kuna mtu yeyote wanamfahamu?

Vilevile kama unatumia zaidi njia shirikishi kama vile, kuwagawa wanafunzi wawili wawili au katika makundi, wanafunzi wanaweza kuelewa zaidi kwa kufanya kazi pamoja. Katika **Shughuli 2**, wanafunzi wanafanya kazi wawili wawili kutafuta majibu ya maswali yao wenyewe. Hii nayo pia inawapa motisha sana wanafunzi.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kuangalia historia ya zana asilia za kilimo

Bwana Msane aliwataka wanafunzi wake kutafuta habari zaidi kuhusu zana za asili zinazotumika kwa kilimo. Aliamua kuwapa nafasi ya kuangalia picha na ughushi, na kuandika juu ya walichokiona. Lakini kwanza,alilishangaza darasa lake. Alikuwa amemuomba mwanajamii mmoja ambaye alikuwa na mkusanyiko wa zana za asili kuzileta baadhi yake darasani.

Wanafunzi waliufurahia huo ugeni na waliweza kukusanya habari nyingi kuhusu zana za asili na kuongezea katika utafiti wao. Koleo la zamani ambalo lilikuwa la babu yake na mgeni liliwasisimua sana wanafunzi hasa kwa sababu ya umri wake mkubwa.

Baada ya ugeni, Bwana Msane aliligawa darasa lake katika makundi madogo na kuwapa kila kundi picha –baadhi ya makundi yalichangia picha moja kwa kuwa hakuwa na picha nyingine za kuwapa.Aliwaeleza kuwa walitakiwa kuzijadili hizo picha na baadae kuandika habari fupi kuhusu kila zana ya kwenye picha ilivyokuwa ikitumika.

Alieleza kuwa wangeweza kutumia karatasi ya maswali na kufikiria juu ya kitu gani cha kuandikia (angalia **Nyenzo rejea ya muhimu 1: maswali ya utafiti kuhusu zana za asili** ). Wanafunzi walitumia muhtasari wao kutoka kwa mgeni na pia kutoka kwenye baadhi ya vitabu ambavyo Bwana Msane alikuwa anavyo. Walifanya kazi pamoja kwenye makundi yao na kuandika. Mwishoni, kila kundi lilitoa lilichoandika kwa darasa zima.

## Shughuli ya 2: Kutafiti ufundi wa mahali hapo

Waambie wanafunzi, wawili wawili, wachague ni zana zipi wanataka kuzitafiti zaidi.

Kila kundi la wanafunzi wawili wawili linaweza kuchagua kati ya kutafuta maelezo kwenye vitabu au kumhoji mtu katika jamii yao, ikiwa ni hatua ya kuanzia.

Halafu, waambie wafikirie aina ya maswali wanayouliza ili yawaongoze wapate maelezo sahihi, kama vile: “Nini matumizi ya asili ya hili bakuli?” Jadili baadhi ya majibu na muamue kwa pamoja kama yanatoa mwelekeo kuhusiana na lengo la utafiti. Kila kundi la wanafunzi wawili lichague maswali yake.

Kila kundi lifanye utafiti kwa kutumia maswalli yake, na njia yao ya utafiti waliyochagua. Kwa wale ambao watatumia vitabu kama vyanzo vya habari, utahitaji kutoa vitabu au makala kutoka vitabuni au magazetini, na wengine uwape muda wa kufanya mahojiano.

Kama wanapata tatizo la kupata habari kwa kutumia njia moja, wanaweza kutumia njia nyingine vilevile. Wape muda wa kutosha kwa ajili ya utafiti na waongoze wanapopata ugumu.

Waambie kila kundi watengeneze bango ili kuonyesha majibu yao

Tathmini kazi ya wanafunzi wako kwa kutumia **Nyenzo rejea ya muhimu 2: Karatasi ya kutathimini mawasilisho ya utafiti** .

## Somo la 3

Unapojifunza mada ya vitendo kama kazi za ufundi, ni muhimu wanafunzi wako wakapata nafasi ya kutumia vifaa vya kujitengenezea wenyewe au walau waone mtu akivitumia kutengeneza vitu vya ufundi.

**Uchunguzi kifani 3** unaonyesha jinsi mwalimu mmoja alivyokusanya udongo wa mfinyanzi kutoka pembeni mwa mto ili wanafunzi wake waweze kutengeneza vyungu vya udongo wao wenyewe. Kwa kuwapa vifaa na kuangalia nini wanachoweza kufanya, wanafunzi wanapata mwanga mzuri wa ujuzi wanaohitaji. Kama una uhakika wa upatikanaji wa vifaa,

waandalie wanafunzi wako watengeneze stadi zao wenyewe.Hizi zinaweza baadae kuonyeshwa kwa wanafunzi wengine au kwa wazazi. Kwa wanafunzi wakubwa, wahimize wathamanishe kazi zao-nini walichohisi kimeenda vizuri? Nini wangeweza kuboresha hapo baadae?

**Shughuli muhimu** inaelezea jinsi ya kuandaa maonyesho ya ufundi. Hii ni njia nyingine ya kuwahamasisha wanafunzi na kuwawezesha kuelewa vizuri uwezo wa ufundi wa mahali hapo.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kutengeneza vyungu

Bi. Kapunga alikuwa anafundisha somo juu ya vyungu vya asili. Alianza kwa kuwataka wanafunzi watoe uzoefu wao juu ya vyungu vya asili na vifaa vingine. Wanafunzi walikuwa na uelewa mzuri juu ya matumizi ya vifaa hivyo wakati wa mavuno na wakati wa sherehe za ndoa na za kidini. Wanafunzi vilevile waliongelea juu ya vyungu tofauti wanavyovifahamu, kama vile vya kuhifadhia mapambo. Wakati wanaongea hayo, Bi. Kapunga alitengeneza orodha ya vyungu vya asili ubaoni.

Bi. Kapunga alikuwa ameleta baadhi ya vyungu ambavyo alivipata kwa watu katika jamii anayoishi. Aliwaambia wanafunzi nao wapeleke vyungu walivyokuwa navyo nyumbani ili waweze kuangali maumbo n.k. Baadae, aliwaonyesha jinsi ya kutengeneza chungu kidogo kutokana na udongo aliokuja nao kutoka mtoni. Aliwapa kila kundi la wanafunzi wawili udongo kidogo watengeneze chungu na kukipamba kwa njia yoyote ile waliyoipenda.

Aliwahimiza waangalie mitindo ya asili, na kutoka hapo ndipo wajenge mitazamo yao wenyewe. Vyungu vya wanafunzi viliachwa ili vikauke pembeni mwa darasa ambapo kila mmoja angeweza kuviona. Bi. Kapunga alifurahishwa sana na kazi ya wanafunzi.

**Nyenzo rejea muhimu 3: Kutengeneza vyungu inatoa taarifa za msingi.**

## Shughuli muhimu

Wanafunzi wako wanapokuwa wamemaliza kufanya utafiti juu ya zana waliyoichagua, mualike mtaalamu mmoja wa mahali hapo aje awaonyeshe jinsi zana hizo zinavyotengenezwa, kwa mfano, utungaji shanga au uchongaji, ndipo wanafunzi wanaweza kutambua zaidi ni kwa nini na kwa jinsi gani wanafanya ufundi.

Halafu, waulize wanafunzi wako ni kwa jinsi gani wangependa kuwasilisha utafiti wao na wangependa wafanye hivyo kwa nani. Lipangilie darasa lako katika makundi ambayo yanapendezwa na ufundi wa aina moja au unaofanana ili wajadili mawazo yao.

Jadili baadhi ya mawazo yao.

Kubaliana nao kuhusu tarehe na sehemu kwa ajili ya hili.

Toa muda wa kutosha kwa kila kundi kuandaa kitabu chake, bango, onyesho, uthibitisho wa jinsi ya kutengeneza zana au mawasilisho kwa kutumia mdomo.

Wafanye majaribio ya tukio na waambie kila kundi liwasilishe kazi zake

Siku yenyewe, darasa au shule nyingine, au wazazi wanaalikwa kuja na kuona kazi za wanafunzi. Kila kundi linasimama na kazi zake na kuelezea kwa wageni. Maelezo kwa mdomo yanafuata baada ya kuwa watu wameona zana zilizoonyeshwa.n.k.

## Nyenzo-rejea ya 1: Maswali ya utafiti juu ya vifaa vya jadi na kazi zake

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**

Angalia picha hii kwa makini. Fikiria juu ya mambo yote unayoyaona kwenye picha hii.



*Imenakiliwa kutoka: Verizon 827, Website*

1. Ni vifaa gani unaviona kwenye picha?
2. Ni nani anavitumia?
3. Huyo anayevitumia, anavitumia kwa ajili gani?



*Imenakiliwa kutoka: IFAD, Website*

1. Ni zana gani unaziona kwenye picha?
2. Nani anazitumia?
3. Huyo anayezitumia, anazitumia kwa ajili gani?

## Nyenzo rejea 2: Tathimini ya mawasilisho ya utafiti

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**

Jina la mwanafunzi: ______________________

Tarehe: ___

Darasa: _____

| **Kipindi cha maonyesho mwanafunzil:** | **Alifani Kiwa vena** | **AlifaniKiwa** | **Anahitaji msaada** |
|---|---|---|---|
| Alionyesha kifaa halisi cha ustadi, mchoro, au mfano wa picha. | | | |
| Alikipa hicho kifaa jina. | | | |
| Alijibu swali la utafiti. | | | |

Maoni ya mrejesho: ______________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

Mwalimu: ________________

## Nyenzo rejea 3: Kutengenza vyungu

**Taarifa za msingi/welewa wa somo wa mwalimu utangulizi**

**Mfano wa kutumia gurudumu la ufinyanzi**

Udongo wa mfinyanzi unaweza kutengenezwa vyombo kutokana na sifa zake za pekee. Muundo wa udongo wa mfinyanzi una tabia ya 'plastiki' unayoufanya utengenezwe katika maumbo mbalimbali. Vifaa hivi vikiwekwa kwenye joto la kutosha vinabadilika kuwa katika hali ya mwamba mgumu, na hivyo kuwa vya kudumu. Udongo wa mfinyanzi unatokana na vitu asilia vinavyopatikana ardhini, kwa maana hiyo, unapatikana duniani kote, chini ya miguu yetu. Udongo wa mfinyazi uliwahi kutumiwa karibu na tamaduni zote, na kwa matokeo ya pekee kabisa. Vyungu vinaweza kutenengezwa kwa kutumia mikono na udongo uliochanganywa na maji.

Mfinyazi, anauandaa udongo kwa mikono yake. Vidole vinatumika kutengeneza sehemu ya chini ya chungu, halafu zinafuatia kuta katika umbo la silinda. Halafu mfinyanzi taratibu hutengeneza umbo analolitaka, kwa kutumia ncha za vidole vyake, kadiri gurudumu linavyozidi kuzunguka. Pindi kazi itakapokuwa tayari, gurudumu lililoko kwenye chungu huondolewa. Mchakato huu hurudiwa kwa ajili ya kutengeneza chungu kingine.

Wakati chungu kinapokuwa kimekauka, kinaweza kusawazishwa. Vishikio vinawekwa kwenye hatua hii. Baadhi ya aina ya mapambo yanaweza kuongezwa.

Pindi vyungu vinapokuwa vimekauka kabisa, vinaweza kuchomwa kwenye tanuru. Hii hutoa vyombo vigumu na vyepesi.

Kila chungu kinatumbukizwa moja kwa moja kwenye ndoo yenye malai kwa ajili ya kung'arishwa.

Pindi tanuru linapojaa, mlango wake unafungwa. Moto unaachwa uendelee kwa masaa 18. Vyungu vinaungua taratibu hadi joto linafikia nyuzi 1,250 °C. Katika hatua anuwai wakati moto unawaka, tanuru linaishiwa hewa ya oksijeni. Hali hii husababisha oksijeni iondolewe kwenye udongo wa mfinyanzi na ving'arisho, kitendo ambacho hupelekea mng'aro zaidi

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

**Mfano wa kutumia mfinyo kwenye kutengeneza chungu**

Kwa kuufinya udongo, unaweza kutengeneza vitu kama wanyama au bakuli, chungu, kikombe n.k. Wakati aina hii ya ufinyanzi inaonekana kuwa ya msingi, unaweza kuelewa tabia za udongo unaofanyia kazi pamoja na kujua mipaka yake (Unakunjika kirahisi? Unakauka haraka? n.k)



Kutengeneza bakuli, chungu au kikombe, anza na fundo la udongo. Kandamizia kidole gumba chako katikati, halafu finya kuta zake kwa juu.



Geuza chungu wakati unafinyanga. Hii itakusaidia kuweka unene wa kuta unaofanana.



Taratibu weka sehemu ya chini kwenye uso wa kitu ulio sawa ili kutengeneza usawa katika sehemu ya chini ya chungu.

**Mfano wa chungu cha jadi – chungu cha kutunzia bangili cha Kiafrika**



Chungu hiki cha jadi kuhifadhia bangili.

*Imenakiliwa kutoka: Hoboken Pottery, Website and JH Pottery, Website.*

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

# Sehemu ya 3: Kutumia ngoma kujifunza

**Swali Lengwa muhimu:** Ni kwa jinsi gani unaweza kutumia ngoma kukuza ujifunzaji na ustawi wa mtu?

**Maneno muhimu:** Ngoma, Utamaduni, Mila, Mabadiliko

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- Umegundua njia za kuonyesha namna mila ya ngoma za kiafrika zinavyoweza kueleza mahitaji ya jamii na maadili yake;
- Umewasaidia Wanafunzi wako kuelewa asili ya mabadiliko ya mila kupitia ngoma ya kufaa;
- Umeielezea mila ya ngoma ili kuboresha ujifunzaji na makadirio, na kujenga ustawi wa mwanafunzi.

## Utangulizi

Sanaa kwa ujumla ni sehemu muhimu ya utamaduni wa watu na ngoma ina nguvu na kipimo tosha cha tamaduni nyingi. Ngoma ni sehemu ya kila sura ya maisha ya Kiafrika. Aina nyingi za ngoma zenye asili ya Afrika, ingawa zina mizizi katika wakati uliopita, zimebadilika au zimepotea; hivyo kuhamasisha utashi katika ngoma kutazilinda zile ambazo bado zinatumika.

Sehemu hii itakusaidia kujenga njia za kutumia ngoma darasani. Inachunguza mila na tamaduni za ngoma katika Africa, pamoja na njia mpya unavyoweza kutumia ngoma katika mtaala.

## Somo la 1

Kuwasaidia wanafunzi wako watambue thamani ya ngoma za kimila za Kiafrika ni sehemu muhimu ya kufundisha sanaa. Kujifunza kuhusu sanaa mara nyingi kumejikita katika masimulizi ya zamani.

Pia, sanaa inawawezesha watu kuelezea maana katika maisha yao ya kila siku na kuwasaidia kujenga hisia za kujitambua na kujithamini.

**Uchunguzi Kifani 1** na **shughuli 1** itakusaidia kuzingatia pamoja na wanafunzi wako namna mila zinavyobadilika na kutoweka, na mdahalo iwapo hili ni jambo zuri au baya.

## Uchunguzi kifani ya 1: Kuchunguza Wavenda na domba

Bi. Sylvia Msane anafundisha katika shule ya msingi Sebokeng, mji ulioko kusini mwa jiji la Johannesburg Afrika Kusini.

Sylvia ameolewa na mwanaume mwenye asili ya Kizulu na wanaongea kiingereza na Kizulu nyumbani. Hata hivyo, mababa wamama yake wanatoka venda. Sylivia anahusisha kwamba wanafunzi wake kama walivyo vijana katika Afrika kusini, wanajua kidogo kuhusu vyanzo vya kimila. Sylvia anafikiria msemo uliorithishwa kwake 'Umuntu ngu muntu nga bantu' 'Mtu ni mtu kwa sababu ya watu wengine'

Ameamua kuwaambia wanafunzi wake hadithi ambazo bibi yake alimhadithia alipokuwa mtoto kuhusu watu wa Venda (angalia **nyenzo rejea muhimu 1: Hadithi za ngoma za Wavenda)**. Baada ya kuwaeleza namna watu wa venda walivyokuja kuishi kaskazini mwa Afrika ya Kusini, anawaonyesha nguo za kimila za kivenda na picha ya mabinti wakicheza domba. Mwanafunzi mmoja anauliza wanachofanya hao wanawake. Sylvia anafafanua kuwa hawa wanawake ni kama wamemaliza kufundwa/jando na wanacheza kama nyoka.Anawaeleza hadithi nyingine kuelezea umuhimu wa nyoka huyu na wanagundua namna ya ngoma ya domba inavyosherekea uwezo wa kuzaa wa mabinti (angalia **nyenzo rejea muhimu 1**). Mwanafunzi mwingine alimuuliza kama alifundwa katika njia hii na anaelezea kuwa hakufanyiwa hivyo. Maisha ya watu na vipaumbele vimebadilika na mila nyingi tokea zamani zimekufa. Wanajadili iwapo ni vizuri au vibaya kwa hili lililotokea.

**Nyenzo rejea ya muhimu 2**: **Mila za kienyeji** inakueleza kuhusu mitindo ya ngoma katika Tanzania.

## Shughuli ya 1: Kuchunguza ngoma za asili za Kiafrika hapo zamani

Chunguza kutoka darasani mwako, wanafunzi wenzio au wanajamii kama kuna wachonga ngoma za asili katika eneo.

Muulize mwalimu mkuu kama unaweza kumwalika mtu. Wasiliana na mtu na mwalike aje azungumze na darasa lako juu ya ngoma za asili na utoe mfano wa ngoma moja au mbili.Waambiwe waje na nguo wanazovaa.

Andaa darasa lako kwa ajili ya ugeni (angalia **nyenzo ya muhimu: kwa kutumia jumuiya/mazingira kama nyenzo rejea** ). Fikiria kuhusus maswali ambayo wanafunzi wanaweza kutaka kuuliza.

Andaa darasa lenye nafasi kwa mgeni kukaa na kucheza ili wanafunzi wote waone.

Mkaribishe na kumtambulisha mgeni.Mgeni aongee na kucheza kwa takribani nusu saa.

Wahimize wanafunzi wako kumuuliza mgeni maswali.

Baada yaugeni, jadili na wanafunzi wako walivyojifunza kuhusu ngoma. Nani wameipenda? Nani wanapenda kufanya zaidi/Kuendelea? Fikiria cha kufanya baadaye.Labda mgeni atarudi kuwafundisha baadhi ya ngoma?

# Somo la 2

Kucheza ngoma darasani kunafaa kwa kazi za mtaala, kwani unagundua mawazo ndani ya ngoma, umuhimu wa mavazi (maalumu) na kujifunza namna ya kucheza ngoma.

Ngoma ni shughuli halisi na inaweza kufanywa kama sehemu ya elimu ya viungo au inaweza kutumika kugundua mawazo katika maeneo ya masomo mengine kama vile fasihi na sayansi.

Katika **uchunguzi kifani 2** na **shughuli 2** za ngoma inatumika kuwasaidia wanafunzi kuonyesha kile wanachojua juu ya mada au kuhadithia hadithi.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kufanya kazi kwenye makundi ili kutengeneza mpangilio wa ngoma

Bibi Msane amekuwa akifanya kazi na darasa lake namna ubongo anavyotuma ujumbe mwilini. Anaamua kutumia mada hii katika masomo yake ya PE ambapo anafanya mfululizo wa masomo juu ya ngoma.

Bibi Msane anawaambia wanafunzi wake kuwa atawagawanya katika makundi ya watu kati ya sita na kumi. Kundi linatakiwa kufikiri njia za kuonyesha namna ujumbe unavyokwenda kutoka kwenye ubongo mpaka kwenye sehemu ya mwili kuiambia ijongee na ujumbe mwingine kurudi

kwenye ubongo kujenga au kusimamisha mjongeo. Anawapa muda wa kufikiri juu ya hili na anawazungukia kuwasaidia wanapozungumza.

Baada ya dakika 15, anapendekeza wanavyofikiri namna ya kucheza ngoma na kuanza kufanya kwa vitendo.Anawatahadharisha/anawakumbusha kuwa waeneze ujumbe/mawazo yao kwa myumbo bila maneno.

Baada ya kufanya kwa vitendo kila kundi linaonyesha namna lilivyofanya baada ya kila tukio/Sehemu ya darasa iliyobaki wanatakiwa kubuni kinachotokea na wanaweza kuuliza maswali.

Anaamua kuwapa muda wa kujenga mawazo yao na kuyaonyesha kwa darasa juma linalofuata, kundi moja mwishoni mwa kila siku.

Bibi Msane anagundua kuwa kila mmoja amefurahia na anafikiri kwamba wanafunzi wake pia wanafahamu umuhimu wa ngoma kama nyenzo ya kujieleza na kama njia ya kuwasiliana.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Shughuli ya 2: Kutumia ngoma kutoka zamani mpaka sasa kuwasiliana

Kumuulizia kila mwanafunzi kutafiti ngoma ambayo mzazi ndugu au mtu wa makamo alikuwa akicheza au bado anafanya. Siyo lazima iwe ngoma ya asili.

Watambue

Ngoma inatoka wapi?

Kwa nini ngoma ilichezwa na ilikuwa na lengo gani? Ilichezwa wapi?

Namna ilivyochezwa?

Wape nafasi ya kufanya hivyo na kuadika namna ya kucheza ngoma (angalia pia **nyenzo muhimu rejea: kutafiti darasani** )

Kinachofuata, kwa kutumia moja ya ngoma za asili kama msingi, waulize wanafunzi wako kuorodhesha inachokusudia (ngoma) kuonyesha)

Sasa waambie wanafunzi wako kuandaa ngoma zao wenyewe kwa kutumia mbinu yoyote wanayopenda, kueleza mawazo yanayofanana. Haya yanaweza kuwa yanahusu.

Kufikia utu uzima; Kuzaliwa kwa mtoto; Mavuno mazuri

Wape nafasi ya kutenda na kushiriki katika ngoma zao

Wakumbushe wanafunzi wako kuwa wanatakiwa kuonyesha hisia zao; kama vile furaha, dukuduku, mshtuko, huzuni pamoja na miili yao na nyuso wanapocheza.

Jadili hisia hizi na wape muda wa kufanya mazoezi tena. Shiriki nao utendaji tena na jadili namna walivyoboresha.

## Somo la 3

Ngoma inaweza kuwa na mvuto kwa mtu binafsi lakini pia imejikita kwenye uchezaji wa kikundi na kuwaruhusu wanafunzi wako wakue katika

kujiamini na kujithamini. Hii ni muhimu kwani inaweza kuinua mtazamo wao juu ya kujifunza na mafanikio yao.

Kama mwalimu, ni muhimu katika nafasi ya vitendo kutambua watu katika kundi na mafanikio yao, pamoja na mafanikio ya pamoja ya kundi.

**Uchunguzi kifani 3** na **shughuli muhimu 3** inapendekeza njia za kutoa mrejesho kwa wanafunzi wako utakaowasaidia kujiandaa kucheza mbele ya hadhira. Utagundua pia namna rika linavyoweza kupima na kupeana mwisho nyuma ili kujenga uelewa wao na kuboresha kazi zao.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kuandaa na kutoa burudani ya ngoma kwa mafanikio

Bibi Msane anasikia kutoka kwa mmoja wa washiriki kwamba shule itakuwa na siku ya wazi mwishoni mwa muhula. Wazazi na watu kutoka kwenye jumuiya wataalikwa kuhudhuria. Bibi Msane amevutiwa na shauku ya wanafunzi wake kutokana na kazi ya kucheza ngoma waliyokuwa wakifanya na anaamua kuwasaidia kutengeneza/kuendeleza ngoma walizotengeneza darasani ili zichezwe kwenye 'Siku ya Wazazi' (Open Day).

Anawahimiza kufanya mazoezi wakati wa chakula cha mchana na kutenga muda wakati wa masomo ya elimu ya viungo. Juma moja kabla ya 'siku ya wazazi', wanacheza wenyewe kwa wenyewe na kutoa mrejesho juu ya ubora wa ngoma na njia za kuboresha. Anatumia mfululizo wa maswali kuwasaidia kufikiri juu ya kuboresha uchezaji wao (angalia **nyenzo rejea 3: Kuboresha ngoma yetu** ). Wanafanya mazoezi na kukamilisha ngoma yao. 'Siku ya wazazi', kila mtu alishangaa namna wanafunzi wa Bibi Msane walivyofikisha mawazo kuhusu namna akili inavyofanya kazi kwa kutumia ngoma. Hatimaye, bibi Msane anawaambia kutafakari uzoefu walioupata; hii inampa mrejesho wa kufaa juu ya mchakato wa kujifunza, pia kuwasaidia wanafunzi wake kufikiri juu ya kile walichopata (angalia **nyenzo rejea 4: Tafakari juu ya ngoma).**

## Shughuli muhimu: Kujiandaa kucheza

Kabla ya somo la kwanza, soma nyenzo rejea 3 na 4

Waeleze wanafunzi wako kuwa watacheza ngoma jioni inayofuata kwa wazazi na kwamba mwalimu mkuu anaalika wanajamii pia waje.

Kabla hujaanza hakikisha kuwa wanafunzi wako wanajua mahitaji ya kuwa waangalifu. Wape maelezo ya kina namna utakavyokuwa unawasimamisha wanapocheza na watahadharishe kuwa wanapaswa kujua walipo wanadarasa wenzao.

Panga darasa lako latika makundi.Kiambie kila kikundi kuandaa ngoma kulingana na mada walizokuwa wanasoma. (Unaweza kuamua au waruhusu wanafunzi wapigie kura kutoka kwenye orodha.

Yape makundi muda wa kufanya mazoezi.

Ruhusu kila kikundi kucheza mbele ya darasa. Wahamasishe wanafunzi wako kupeana yanayofaa yatakaowasaidia kuboresha michezo yao.

Wasaidie wanavikundi wanapofikiria namna ya kuboresha na kuziremba ngoma zao ili ziwe tayari kuchezwa mbele ya hadhira

Jadili mavazi na vivaa vya ngoma na uviandae

Andaa ratiba

Cheza

Jadili pamoja namna ilivyoenda. Wamejifunza nini kuhusu ngoma? Wamejifunza nini juu ya mada?

# Nyenzo-rejea ya 1: Hadithi za ngoma ya Venda

**Taarifa za msingi/welewa wa somo wa mwalimu utangulizi**

**Hadithi ya ngoma takatifu ya Venda**

Hapo zamani za kale, miungu ya mababu iitwayo Mwari iliwapa watu wa Venda ngoma yao takatifu ikiitwa ngoma Lungundu. Katika siku hizi za kale, mababu wa venda waliishi Zimbambwe. Siku moja walipokea ujumbe wa kimungu kwamba wanatakiwa kuchukua ngoma yao takatifu, Ngoma Lugundu, na waelekee kusini.

Ngoma hii ilikuwa kubwa na nzito na ilipaswa kubebwa na wanaume wengi. Ili watunze nguvu za ngoma, ilitakiwa isiguse chini/ardhi.Ikipigwa na mfalme inaweza kusababisha ukungu, mvua ya mawe, mvua, radi au miale ya radi. Kwa muda fulani Mungu mkuu Mwari anaipiga yeye mwenyewe. Wakati huu ngoma ingeonekana kama inajipiga yenyewe. Maadui walikimbia kwa hofu, walizimia au kufa waliposikia midundo yake yenye nguvu.

Nguvu hizi zilisaidia kuwalinda hawa mababu wa Venda wakati wa hii safari na mwishowe walifika wanapoishi leo hii kaskazini mwa Afrika kusini. Hapa kuna ziwa linaloitwa funduzi ambalo ni takatifu kwa wavenda.

Miaka mingi iliyopita, shujaa wa wavenda, aitwaye Thoyo ya Ndou, alipotelea katika ziwa hili akiwa amebeba ngoma hiyo. Watu wengi wanafikiri kuwa haijawahi kuonekana tangia wakati huo, lakini wengine wanaamini kuwa imelindwa na kufichwa katika pango.Thoyo ya Ndou, au mkuu wa Tembo, alikuwa anatamaniwa kwa sababu aliwaunganisha watu wa Venda na kulikuwa na amani na ustawi. Tangu alipopotea, wengi wanasema kuwa kumekuwa na kutoelewana mafarakano/migongano katika familia ya kifalme ya Venda.





*Chanzo halisi: Catalogue: Ten Years of Collecting (1979–89), Standard Bank Foundation Collection of African Art, Editors: Hammond-Tooke & Nettleton, 1989*

**Nyoka/Joka (Chatu)**

Katika jimbo la Limpopo kuna ziwa zuri liitwalo Fundulizi.Watu wa Venda wanalichukulia kuwa muhimu sana, eneo lililotakaswa, kwani wanaamini kuwa kuna joka kubwa jeupe linaloishi chini ya Fundudzi. Joka hili ni Mungu wa mtuba. Kwa maneno mangine anahakikisha kuwa watu wana afya nzuri na wana watoto wengi.

Hapo zamani, Mungu huyu aliishi nchi kavu.Alikuwa na ngozi nzuri; na alioa wanawake wanadamu wawili; mmoja mzee na mwingine kijana. Ilitokea kuwa alikuwa akiwatembelea hawa wake zake wawili kila siku usiku sana. Alitembelea vibanda vyao walipokuwa wametingwa na kazi za shamba. Hivyo hawakuwahi kumuona mume wao au kujua alikuwa anafananaje.

Siku moja, mke mdogo aliingiwa na tashwishwi na kuamua kurudi toka shambani mapema na kuchungulia dirishani. Alitishika alipoona kuwa mume wake alikuwa ni joka nene na kupiga kelele. Joka lilikimbia na kuingia ziwani. Tokea hapo kulikuwa na ukame na njaa juu ya ardhi. Wanyama walikufa na hakukuwa na maji ya kutosha kwa ajili ya mazao.

Hakuna anayejua kilichosababisha balaa hili na wazee walikutana ili kujadiliana juu ya tatizo hilo. Hatimaye, mke mdogo alikiri kuhusika kwa yale yaliyotokea. Walimwomba awasaidie kurudisha rutuba kwenye ardhi. Siku moja alichukua mtungi wenye pombe na kuelekea ziwani. Wanaume walipiga filimbi zao ili kumtia ujasiri. Alitembea kwenye kina kirefu hadi maji yalipofunika kichwa chake, na hakuonekana tena.

Baada ya hili, mvua ilirudi na ukame ukakoma. Mpaka leo, wafalme wa Venda na waganga wa kienyeji/jadi huenda kwenye ziwa Fundudzi na kumwaga pombe majini. Wanaamini kuwa kama pombe itazama, ni dalili za furaha ya Mungu Nyoka na kukubali kwake zawadi yao. Katika mila ya Venda, vijana kuhudhuria shule maalumu ya jando.Hii huwaandaa kwa majukumu yao kama waume na wake ndani ya jamii. Vijana hujifunza ngoma ya domba wanapohudhuria dombani au shule ya jadi. Kabla ya domba haijaanza, kiongozi wa ngoma anaita: ‘Tharu ya mahbidighami!’ (‘Joka linajikunjua’). Wanapocheza ngoma, hutengeneza mstari mrefu kama ‘nyoka’ kwa kuzunguka moto.

## Nyenzo-rejea ya 2: Mila za kienyeji: Mbinu za kuchezangoma katika Tanzania

**Taarifa za msingi/welewa wa somo wa mwalimu utangulizi**

Kimila/ kiasili, makabila katika Tanzania walitumia muziki na ngoma kuashiria tukio maalumu kama vile uvunaji, sherehe za jando na harusi. Ngoma, moja ya vifaa muhimu vya muziki, hutumika pia kama njia ya mawasiliano. Kila kabila ya makabila 120 ya Tanzanaia wana ngoma yao au mbinu yao ya uchezaji. Kwa mfano, wanapocheza Wamakonde hutikisa viuno vyao katika msisimko wa sindimba; wakati Wasukuma hutumia nyoka kama vile chatu katika ngoma yao ya Bugobogobo” Wazaramo wanarukaruka katika mdundiko, wakati wanapocheza ngoma ya asili kama vile ‘mitamba yalagala kumchuzi’ .

Wamasai wana ngoma ya kuruka inayoendana na mdundo wa kuguna wa sauti zao nzito.

*Chanzo halisi: Tanzanian Culture, Website*

Kama unaweza kupata mtandao unaweza kuwaonyesha wanafunzi wako mikanda ya video ya ngoma za asili, kwa mfano:

http://www.youtube.com/watch?v=9ifeNAP-AXM Ni mkanda wa video wa ngoma za asili mkoani mwanza

## Nyenzo rejea 3: Kuboresha ngoma zetu

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**

Tumia maswali yafuatayo kuongoza mjadala juu ya ngoma ya kila kundi. Kumbuka kuwa hulazimiki kufuata maswali haya katika mapangilio fulani.

Ubunifu;

Unaweza kubuni tofauti/mabadiliko yaliyomo ndani ya ngoma yako ili uwasilishe mawazo yako?

Unaweza, kwa mfano, kubadilli uelekeo kutumia sehemu tofauti za nafasi, kutumia sehemu tofauti za mwili au kubadilisha eneo kati ya wacheza ngoma?

Kufanya kazi pamoja

Kuna njia tofauti za kufanya kazi pamoja katika ngoma ya kundi. Angalia baadhi ya tofauti zifuatazo:_

Kufanya kazi kwenye kundi kubwa m.f wawiliwawili; Kuangaliana, kucheza jirani, kugeukiana na kuegemeana; Kutofautisha umbali kati ya wachezaji;

Kubuni mtazamo wa mmoja au wachezaji zaidi katika muda fulani; Kuruhusu mchezaji mmoja aongoze na wengine wafuate.

Nafasi ya kuchezea

Je, Unahitaji kujibana kwenye ngoma ili utimize nafasi ya kuchezea? Ni namna gani utajipanga kwenye nafasi ili uanze?

Ni namna gani utajipanga kwenye nafasi utakapomaliza?

Ni namna gani utajipanga kwenye nafasi wakati wa kucheza? Utayari wa hadhira

Ni rahisi kwa hadhira kuwaona wacheza ngoma katika kundi?

Unaweza kujibana ngoma ili hadhira ione vizuri

Mambo mengine ya kufikiria

Kuna mtu yeyote ndani ya kundi lako anayehitaji kuungwa mkono au msaada?

Unaweza kuiboresha kwa kuvaa kofia ile ile, rangi fulani n.k?

# Nyenzo rejea 4: Kutafakari juu ya ngoma

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**

Unaweza kutumia haya maswali hapa kuwasaidia wanafunzi wako kurudi nyuma kwenye uzoefu wao. Waambie wasome na kutafakari juu ya maswali haya kwa uangalifu na kuyajibu kwa uaminifu na undani.

1. Andika maneno matatu au zaidi kueleze jinsi ulivyojisikia wakati wa hatua zifuatazo:-
   a) Ulivyotoa ngoma yako kwa darasa
   b) Kushuhudia wengine wakicheza
   c) Kuicheza ngoma yako mbele ya hadhira
2. Ni nini ulichofurahia zaidi juu ya masomo hayo? Kwa nini?
3. Ni nini ulikiona kama changamoto juu ya masomo hayo? Kwa nini?
4. Unafikiri ni jambo gani la mafanikio juu ya ngoma yako? Kwa nini?
5. Unafikiri kuna njia za kuboresha ngoma yako? Kama ndivyo namna gani?
6. Ni uigizaji/uchezaji gain mwingine uliopenda? Kwa nini?
7. Umejifunza kitu chochote kipya kuhusu wewe mwenyewe?
8. Umejifunza nini kutoka kwa michezo mingine/nyingine?

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

# Sehemu ya 4: Kutumia muziki darasani

**Swali Lengwa muhimu:** Kuna mbinu gani tofauti ambazo zinatumika kutengeneza muziki darasani?

**Maneno muhimu:** muziki; wimbo wa kusifu; kazi ya kikundi;jamii; vifaa; utamaduni

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- Umetumia mazingira na jamii kama nyenzo za kujifunzia;
- Umepanga shughuli za muziki kwa vitendo;
- Umewahusisha wanafunzi kutengeneza muziki wao, kwa akutumia muziki wa tamaduni na desturi mabalimbali.

## Utangulizi

Muziki ni sehemu muhimu ya maisha na tamaduni za watu. Uelewa wa nafasi ya muziki na namna ya kuufanya muziki uwasaidie wanafunzi kujitambua na kujiamini ni muhimu.

Msisitizo katika sehemu hii ni kugundua sauti mabalimbali na kufanya kazi pamoja. Katika shughuli zote hizi, wahamasishe wanafunzi wako kusikiliza kwa umakini,kuuliza maswali na kujaribu.

## Somo la 1

Mazingira ni nyenzo ya thamani katika kugundua sauti na namna vifaa tofauti vinavyoweza kutoa sauti.

Madhumuni ya sehemu hii ni kupanua uelewa wa wanafunzi wako na uzoefu wa aina mbalimbali za sauti, na kuona namna wao wenyewe na mazingira yao ya karibu yalivyo nyenzo za muziki. **Uchunguzi kifani 1** na **shughuli 1** vinaonyesha namna sauti katika maisha yetu ya kila siku zilivyo mwanzo mzuri wa mada hii.

Shughuli hizi zingeweza kupanuliwa kwa kuwaambia wanafunzi watengeneze zana zao wenyewe kutokana na vifaa vya kawaida* (makopo, chupa n.k) au unaweza ukabahatika kuwapata wanafunzi wanoweza kupiga zana au kuimba. Wapangie namna watakavyoonyesha ujuzi wao darasani.

Angalia Nyenzo rejea 1: Kugundua sauti ili kupata taarifa za msingi na moduli ya **SAYANSI 3, Sehemu ya 2** kwa taarifa zaidi juu ya sauti na vifaa vya muziki.

## Uchunguzi kifani ya 1: Kutengeneza ramani akilini kuunganisha vifaa na sauti

Katika darasa lake la msingi la Soweto, Afrika ya Kusini, Bi Simelane anagundua wavulana wawili wakigonga dawati. Anasikiliza kwa makini jinsi wanavyotengeneza mapigo kwa kutumia dawati kama ngoma. Halafu wanagonga makasha yao ya penseli. Bi Simelane anafuatilia kwa makini muziki wao, na anawaambia wanadarasa wafumbe macho yao na kusikiliza. 'Wanatengeneza muziki? Kwa jinsi gani?' 'Unaweza kusikia

sauti gani tofauti?' Wanafunzi wanavutiwa kutumia madawati yao, kalamu zao na makasha ya penseli kutengeneza sauti. Anawaacha wagundue sauti tofauti wanazoweza kutengeneza kwenye madawati yao kwa kutumia vifaa vinavyowazunguka. Wanasikiliziana sauti na kutoa maoni ya jinsi zinavyotengenezwa.

Bi Simelane anawaambia wanafunzi wapendekeze zana zinazotengeneza sauti akilini mwao na kuzirekodi ubaoni. Anawahimiza kufikiria juu ya uhusiano kati ya vifaa na sauti. 'Ni aina gani ya sauti tunaisikia tunapogonganisha chupa na kijiko? Au kupuliza mdomo wa chupa ulio wazi?' 'Ni sauti gani zinatengenezwa na ngoma za ukubwa tofauti?'

'Tunailezeaje sauti?' anaongezea mawazo yao kwenye ramani ya akilini mwao.

Anaridhishwa na majibu yao na anaona huu kama ni mwanzo wa wanafunzi kutengeneza zana zao kwa kutumia vifaa vilivyo kwenye maznagira ya kawaida. (Angalia **Nyenzo rejea 2: Kutengeneza zana** ).Mwishoni mwa somo, anawaambia waende nyumbani na kukusanya vifaa vingi tofauti kadri watakavyoweza na kuvileta shuleni kuongezea kwa vile vilivyokwisha kusanywa. Juma lijayo watatengeneza na kuonyesha zana hizi.

## Shughuli ya 1: Kusikiliza sauti

Kabla ya somo, soma Nyenzo rejea 3: Kusikiliza sauti katika maisha ya kila siku.

Waambie wanafunzi wako wakae kimya na kusikiliza sauti wanazoweza kuzisikia darasani.

Katika makundi, au darasa zima likiwa limekuzunguka, wachangie mawazo juu ya sauti zote wanazoweza kusikia kwenye karatasi kubwa au ubaoni. (angalia **Nyenzo rejea muhimu: Kutumia ramani za akilini na chemsha bongo kugundua mawazo** .)

Baadaye, panga makundi madogo ya wanafunzi (nne/tano) kwenda nje kwa muachano na kutembea kwenye viwanja vya shule. Wasimame katika maeneo manne na kusikiliza kwa makini chochote wanachoweza kusikia. Wachukue kalamu au penseli na vitabu vyao au karatasi kwa ajili hii.

Kila kundi wachukue dondoo kwa kila sauti mpya wanayosikia na mahali walipoisikia, na wajaribu kuainisha ni nini kinatengeneza hizo sauti na kwa namna gani zinatengenezwa.

Wanaporudi darasani, waambie kila kundi wachore ramani zao za kufikirika juu ya sauti walizosikiliza.

Haya yanapoisha, yaonyeshwe ili wote waone na kujadili mawazo yao namna sauti zinavyotengenezwa.

# Somo la 2: Kufanya kazi katika vikundi ili kutunga ushairi wa wasifu yaani utenzi

Utenzi na uimbaji ni uzoefu muhimu wa Kiafrika, wa kale na wa sasa. Majina ya Kiafrika huambatanisha nafsi yako na wapi utokako. Huwataarifu watu kuhusu uzoefu wako, furaha na mapambano yako, na jinsi ulivyo, ili watu wakutambuwe. Watu hutunga nyimbo zao wenyewe za sifa. Watunzi wa mashairi huburudisha kwa kuonyeshwa kwenye sherehe, ada za asili na sikukuu ili kutoa wasifu wa mtu au kikundi. Nyimbo za sifa na utenzi zimekuwa sanaa staarabu, ambayo hufanywa na tamaduni nyingi kwa kupitia muziki, dansi na uimbaji.

Utawasaidia wanafunzi kufanya utafiti na kubuni tenzi zao wenyewe au nyimbo, ukilenga mawasiliano ya kujitambulisha na urithi wa ukoo. Hii itawasaidia wanafunzi wako kupata uhusiano baina yao wenyewe na uzoefu wa muziki.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kutumia mashairi ya kusifu kujenga uelewa wa muziki

Ndugu Mtui ni mwalimu wa muziki, sanaa na utamaduni ambaye amekulia Kilimanjaro. Anafundisha shule ya msingi iliyoko mjini, ambako wanafunzi wake wanawakilisha, tamaduni, dini na lugha mbalimbali. Anapiga wimbo wa kichaga wa zamani kwenye gitaa lake anapokuwa anafikiria juu ya somo lake la muziki la mwezi ujao. Atajengaje dhamira ya utambulisho kwa kutumia muziki? Anapoimba, muziki unamrudisha nyuma wakati wa utoto wake, nyumba yao, wazazi na mababu na mabibi. Anakumbuka alivyokuwa anasikia nyimbo za kutaja majina na kujisifu kama mtoto. Anaukumbuka wimbo wake wa majigambo unaoelezea kuzaliwa kwake na ukoo wake. Kumbukumbu zake zinatengeneza mwanzo wa wazo lake kwa darasa lake.

Ndugu Mtui anakusanya baadhi ya mashairi ya kusifu na nyimbo na kuvitungia maswali. Anasikiliza muundo wa nyimbo za kuita na kujibu na anaziunganisha na mchezo wa kujigamba uliozoeleka ambao wanafunzi wake wanaucheza kiwanjani. Anapanga kufundisha somo juu ya mashairi ya kusifu kwa kuanzia kwenye nyimbo zilizozoeleka. Halafu anawahimiza wanafunzi wake kutengeneza na kuimba nyimbo na mashairi ya kusifu rafiki zao. Angalia **Nyenzo rejea 4: Kuimba kwa kusifu** kwa habari zaidi za kina.

## Shughuli ya 2: Nyimbo na mashairi ya kusifu

Kabla ya shughuli hii, tazama **Nyenzo rejea 5: Nyimbo za kusifu za mwanafunzi.**

Imba wimbo wa kusifu unaofahamu darasani kwako au mwambie mwanafunzi aimbe darasani. Waeleze wanafunzi namna muundo wa wimbo unavyofanya kazi na washirikishe kutoa majibu.

Imba wimbo tena wakati wanafunzi wakitunza mdundo kwa kupiga makofi, kugonga madawati au kutumia zana.

Ongea nao juu ya wazo la nyimbo za kusifu, nani wanaziimba na kwa nini

Imba nao shairi la kusifu, ukifuatilia mapigo ya maneno na kuwasilisha hisia za shairi kwa sauti yako. Ongeza sauti za vifaa zitakazoongeza hisia za shairi kama inawezezekana.

Halafu, ligawe darasa katika makundi ya wanafunzi sita. Waambie kila kundi wafanye kazi watatu watatu na waandike shairi lao la kusifu. Kila wanafunzi watatu waimbe shairi lao kwa wenzao watatu kisha waeleze maana na hisia zilizopo kwenye shairi. Kwa pamoja, kundi zima linachagua kiitikio na kujaribu kuimba mashairi yao mawili. Wanaweza kuongeza sauti nyingine kama wanapenda.

Baada ya siku chache zijazo, waambie kila kundi liimbe shairi lake la kusifu kwa darasa zima.

## Somo la 3

Upigaji muziki ni aina ya mawasiliano: vyombo na sauti 'huzungumza', kuwasilisha hisia, mawazo na fikra. Muziki huakisi na kujenga utamaduni, na daima huwa na vuguvugu – linalobadilika na kuendelea. Barani Afrika, muziki ni muhimu kwa kujenga mshikamano wa kijamii (umoja) na unaweza kuwa muhimu darasani.

Katika sehemu hii, utaendeleza vitendo vilivyopita kwa kuandaa maonyesho ya darasa zima. Jinsi ulivyokipanga kitendo ndivyo hivyo kitakavyochangia katika maarifa ya ushirikiano na usikilizaji wa wanafunzi.

## Uchunguzi kifani ya 3: Thamani ya kuandaa muziki wa kikundi

Uchu wa Goodluck ni kutengeneza muziki katika kikundi. Hisia anazopata akiwa anapiga marimba, au anapoimba katika kwaya ni maalumu kwa mshikamano. Anataka kuwashirikisha wanafunzi wake hisia hizi; wapate uzoefu wa namna inavyokuwa kutengeneza muziki wa pamoja wakati kila mmoja anamsikiliza mwenzake kwa umakini.

Goodluck anasafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma iliyoko katikati mwa Tanzania, na kutembelea Shule ya Msingi Umoja iliyoko mbalil na mjini. Anamtembelea mwalimu wa sanaa na utamaduni. Anapofika, anakuta kuna sherehe. Makundi ya wavulana wadogo yanapiga filimbi na ngoma wakati wa maandalizi.Kwenye uwanja wa vumbi, Goodluck anasikiliza na kuliona kundi la watoto 50wakisogea na kufanya muziki kwa pamoja-kila mmoja akichangia, akitazama na kusikiliza wanapoeleza hadithi ya ngoma.

Akivutiwa na wapiga filimbi na ngoma, aliamua kuwa wanafunzi wake Dar es Salaam wanahitaji kupata uzoefu wa jinsi gani ilivyo ‘kuwa mmoja’ kwa kutumia muziki. Baada ya kuongea na waalimu na kujifunza zaidi juu ya umuhimu wa muziki kiutamaduni na ngoma ya Mheme, anarudi nyumbani kuandaa somo ambapo wanafunzi wake watatengeneza muziki kwa pamoja.

Nyenzo rejea 6: Kutengeneza muziki inaonyesha ni jinsi gani zana za muziki zinaweza kutengenezwa kwa ajili ya wanafunzi wako kuzitumia.

## Shughuli muhimu: Kutengeneza muziki

Waulize wanafunze kama mmoja kati yao anapiga kifaa cha muziki. Kama wanapiga, waambie wavilete shuleni.

Siku inayofuata, waambie wanafunzi walioleta vifaa wavionyeshe na kuvipiga darasani.

Waulize wanafunzi wako kama wanajua nyimbo au mashairi ya majigambo. Kama wanajua, waambie wakuambie maneno, na yaandike ubaoni.

Mwambie mwanafunzi aimbe ushairi/wimbo halafu waambie wanafunzi darasani waungane nawe utakapoimba ushairi/wimbo tena.

Rudia hadi darasa litakapoimba barabara.

Sasa, waambie wale wanaopiga vifaa nao waungane na wenzao. Fanyia mazoezi wimbo mzima hadi kila mmoja atakapofurahi na waimbe kwa darasa lingine au 'siku ya wazazi'.

## Nyenzo-rejea ya 1: Kugundua sauti

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**

**Shughuli A: Maswali ya kimuziki kuhusu sauti**

Anza kwa kuchunguza sayansi ya sauti na wanafunzi. Gundua haya maswali na wanafunzi wako kwa kutengeneza sauti mbalimbali, katika njia tofauti, kwa kutumia vitu vinavyokuzunguka: dawati, sakafu, kalamu, chupa, ubao au dirisha. Kumbuka, kuongelea juu ya sauti lazima

kuendane na uzoefu tulionao juu ya sauti.

Sauti ni nini?

Nini kitokee ili sisi tusikie sauti? Sauti inasafirije kutufikia sisi?

Nini kinafanya kitu kuwa kifaa cha muziki?

Tunaweza kutumia mwili wetu kama kifaa cha muziki? Kwanini unafikiri kuwa watu wanatumia vifaa vya muziki

kutengeneza muziki? Inatimiza malengo gani?

Unafahamu vifaa gani vya muziki? Unaweza ukaviainisha katika makundi?

Ni kigezo gain ulitumia kuainisha hivyo vifaa?

**Shughuli B: Muunganiko wa kisayansi – jinsi gani sauti inasafiri**

Umewahi kuona"wimbi la Kimeksiko" ('Mexcan Wave') kwenye tukio kubwa la kimichezo? Sauti husafiri kwenye njia sawa na mwendo wa wimbi la Kimeksiko; molekyuli za hewa, kama watu katika mkusanyiko, zinakwenda mbele na kurudi nyuma, zikiungana na kutengeneza wimbi. Molekyuli mojamoja hazisafiri kutoka eneo moja kwenda jingine: molekyuli hutetemeka, kila moja kwenye nafasi yake, isipokuwa

kunapokuwa na kitu kingine karibu na molekyuli zinasogea. Hizi molekyuli zinazotetemeka zinavuta molekyuli nyingine, hivyo basi zinatoka kwenye sehemu zao.

Sauti inaweza kusafiri kwenye hewa kitu chochote kilichotengenezwa kwa molekyuli kama maji, chuma au mti. Sauti husafiri kwa kasi tofauti kutegemeana na kitu inamosafiria.

**Shughuli C: Kutengeneza wimbi la sauti**

Tengeneza mstari wa wanafunzi kumi waliosimama kwa kufuatana. Upande mmoja, mwambie mwanafunzi mmoja apige chombo cha muziki kama mbiu na mwingine alama kubwa inayosema SAUTI. Upande mwingine, mwabie mwanafunzi abebe picha kubwa ya SIKIO. Wanafunzi wengine kwenye mstari wawe na alama ya HEWA.

Mwambie mwenye mbiu aipige. Mwanafunzi wa kwanza.anayumba mbele na nyuma kwa kutumia mwili wake (huku miguu ikiwa imesimama ardhini); mwanafunzi anayefuata naye anayumba baada ya kuhisi uwepo wa mtetemo wa mwanafunzi wa kwanza, na hivyo hivyo kwa mstari mzima.Mwnafunzi wa mwisho anashikilia alama ya KUSIKIA anapohisi myumbo wa mwanafunzi anayemfuata.

*Chanzo halisi: Stomp Online Lessons, Website*

## Nyenzo-rejea ya 2: Kutengeneza zana

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**

'Zamani za kale, kabla vitu vya kutengenezwa na binadamu kuwepo,watu katika jamii za asili ya Afrika walitengeneza zana za muziki kulingana na vifaa vilivyokuwa karibu yao…Katika jamii za vijijini walitengeneza pinde kutokana na miti, njuga kutokana na matunda au magamba ya kokuni yaliyojazwa mbegu au mawe, na ngoma kutokana na ngozi za wanyama na miti'

*(Traditional Music of South Africa by Laurie Levine, 2005)*

**Orodha ya vifaa vya kutengenezea zana**

Tengeneza mkusanyiko wa vitengeneza sauti, kwa kutumia aina zifuatazo kama mwongozo.

Vifaa vya miti. Vifaa vya chuma.

Vifaa vyenye mashimo.

Nyuso zinazoweza kukwanguliwa. Nyuso zinazoweza kugongwa.

Vitu vinavyoweza kutundikwa. Vitu vinavyoweza kutikiswa.

Vifaa vinavyoweza kunyonyolewa. Vyombo kwa ajili ya ngoma:

Chupa ndogo za glasi au chupa ya plastiki, vikombe, viberiti, masanduku ya unga wa kusafishia, ubao wa kubania karatasi au

mabomba ya plastiki, makopo ya kahawa, makopo ya vinywaji baridi, chupa za plastiki za vinywaji.

Vipande bapa vya Makasha ya kutengenezea sinia la sauti.

Chupa za glasi za ukubwa na maumbo mbalimbali (zijaze maji na uzigonge kwa kifaa cha chuma).

Vitu ya kujaza kwenye vitikisio na vigoma

Mawe, mbegu, mchele, maharage, misumari, mchanga,shanga, vifuniko vya chupa, vizibo vya chupa, vitoboleo vya karatasi, mawe.

Vifaa kwa ajili ya gitaa:

Masanduku ya viatu, madebe makuukuu, tepe zinazovutika, vipande bapa vya miti, nyaya nyembamba au mishipi ya kuvulia samaki.

Vifaa vya kutengeneza zana zinazoweza kutoa sauti zaidi ya moja: Birika kuukuu, vyombo vya jikoni, visu, kifuniko cha habu ya gari,

mbuzi ya kukunia nazi, brashi ya kupangusia nguo, chujio,

Vifaa vya chuma vya kuning'iniza kutoka kwenye stendi, kining'inizio chaa chuma au cha mti

Misumari ya chuma iliyofungwa pamoja, boliti kubwa ya chuma, vipande vya chuma vikuukuu, kiatu cha farasi kikuu, na bomba la shaba.

Vipigaji:

Kisu kikuu, msumari mrefu, fimbo imara ya mti, mswaki, rula na, kijiti. Vifaa zaidi:

Maganda ya mbegu au vibuyu vikavu, gazeti, nyaya za kuning'inizia makoti, povu, uzi na nyaya za chuma za ukubwa na uimara tofauti, fimbo za miti au matofali na mifuko ya plastiki.

# Nyenzo rejea 3: Kusikiliza sauti katika maisha ya kila siku

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**

Shughuli hii inawahimiza wanafunzi kusikiliza sauti zinazowazunguka. Unaweza kuitumia kama mradi wa darasa au mradi wa ‘utafiti wa sauti’ nyumbani.

**Msako wa sauti**

Waambie wanafunzi wafanye kazi katika makundi ya watu wawili wawili kutambua na kurekodi sauti zifuatazo kwa kutumia maneno, alama au michoro. Msako unaweza ukafanyika nyumbani, mitaani au shuleni.

Malengo ni kutumia masikio yao, na sio macho yao! Waambie watambue:

Sauti ya muziki;

Sauti ya kukarahisha;

Sauti ya juu kabisa wanayoweza; Sauti fupi na kali;

Sauti zinazowafanya wajisikie kutulia na kuburudika; Sauti endelevu;

Sauti yenye mpangilio unaoeleweka;

Sauti inayowafanya watake kujongea au kucheza; Sauti ya vitisho

sauti ndogo sana;

sauti ambayo iko mbali sana;

sauti ambayo iko karibu;

sauti ya kimdundo; sauti ya mlio wa njuga sauti yenye mkwaruzo; Sauti nzito.

Kwa kuanzia, tumieni sauti chache kati ya hizi wewe na wanafunzi wako, kwa kuchagua zilizo rahisi (kama sauti nzito), halafu ongeza orodha kila wanapoelewa zoezi. Waache watengeneze maelezo ya sauti wenyewe na wajaribu kutengeneza sauti ambazo zinafanana na maelezo yao.

# Nyenzo rejea 4: Kusifu uimbaji

**Taarifa za msingi/welewa wa somo wa mwalimu utangulizi**

Mada za uimbaji wa kusifu zinaweza kuwa kati ya rasmi na zisizo rasmi. Kwa vile zinashawishi, zinasisimua, zinachokoza na kupendezesha suala linalosifiwa, kila kitu ni sawa/haki. Mbinu rahisi kabisa za kusifu na za kawaida mara nyingi zinaleta usikivu wa sura sahihi ya mtu anayehusika. Mwimbaji anaweza kuelezea juu ya uzuri wao au ujeuri wao, umbo lao (urefu, ufupi, wembamba au upana) au rangi ya ngozi zao.

Hapa kuna baadhi ya mifano ya hizi aina rahisi za kusifu:

*E wo geele ya ya* – Tazama mmiliki wa hiki kichwa cha kifaa cha kuwindia wanyama.

*E wa woo* – Njoo uone (hii ingefuatiwa na majina ya mtu majisifu ya muonekano wao).

Kwa undani, mwimbaji wa kusifu anaweza akachukua mafanikio ya mtu au familia yake ya karibu. Iwe biashara, siasa au mafanikio ya kimila, yanaweza yakasifiwa moja kwa moja.

Bibi ire ko se f'owo ra oti daju – Huwezi kununua uzaliwe kwenye ukuu. Ki a bi ni ko to ka tuntun ara eni bi – Kuzaliwa kwenye ukuu hakuna

maana ukilinganisha na ulichokifanya ulipopewa nafasi…….(weka jina la mtu hapa)

Au wanaweza kusifiwa kwa kuelezea sifa zao za jumla, za majina ya familia zao au miji yao.

Kwa undani zaidi, waimbaji wa kusifu huchukua kwenye mila na desturi za jamii fulani, historia ya maneno na ushairi kupandisha hadhi ya mtu ambaye anawamwagia fedha. Hii inafanyika ufahamu wa majina ya familia, miji au mikoa, na historia za kabila. Kwa mfano, katika Wayoruba wa Nigeria, kila mtu, familia na mji ana kile kinachotambulika kama 'Oriki' au mashairi ya kusifu. Mashairi haya ya kusifu yanasema vitu rahisi lakini vya maana sana juu ya watu na vitu vilivyowafunga kijamii (kwa mfano kifamilia, kimiji, na kikabila).

Mwimbaji mkuu wa kusifu ana uelewa na mtazamo mzuri wa jamii kuchukua haya na kutoa mchanganyiko wa simulizi ambazo zinabadilika mara kwa mara na zinaburudisha, kusifu na kuchekesha,ambazo zinahusisha hadhira inayoangalia onyesho na kusubiri nafasi yao ya kummwagia mtu fedha ili wasifiwe mbele ya macho ya halaiki. Mwimbaji wa kusifu anatakiwa mara kwa mara aitathmini hadhira na kuliongoza kundi / kwa mwelekeo wowote ule linakoelekea kuchemka, hadhira itajihusisha na fedha zitamwagika.

Mfano mzuri wa wimbo wa kupokezana kutoka Tanzania ni 'Twendeni

Tukajenge Taifa'. Twendeni tukajenge Taifa Twendeni tukajenge Taifa... Twendeni tukajenge Taifa!

Nyerere maua mama popote chanua... Nyerere maua mama popote chanua!

*Chanzo halisi: E. Songoyi, 'Memories of National Services Songs', 2004, unpublished.*

# Nyenzo rejea 5: Nyimbo za kusifu za mwanafunzi

**Taarifa za msingi/welewa wa somo wa mwalimu utangulizi**

**Gracie – Wimbo wa kusifu**

Imba shairi hili na waambie wanafunzi wako wabuni kiitikio kinachoendana na mwito.Chagua vifaa au sauti zinazooana na maneno: juu, iliyojikita, miito, chachu, miongozo na mwezi.

**Mwito:**

Gracie

Anayeishi kwenye jangwa kuu

Amejikita katika amani

Anaita roho za ngedere na simba Anachachua pamoja na kereng'ende Anaongoza kalamu

Mwezi ukazama

***Mstari 1.*** Gracie (jina langu).

***Mstari 2.*** Anayeishi kwenye jangwa kuu (nilizaliwa na kulelewa hapa

Bend ambalo ni jangwa kuu).

***Mstari 3.*** Amejikita katika amani (babu zangu Mfalme Joseph wa kabila la

Nez Perce alifahamika kwa tabia yake ya amani).

***Mstari 4.*** *Anaita roho za ngedere na simba* (wanyama wangu wanaowakilisha mizimu ni ngedere na simba. Ngedere huonyesha hulka yangu ya ututoni na simba huonyesha nguvu, ufahari na ukatili).

***Mstari 5.*** *Anachachua pamoja na kereng'ende* (Kereng'ende anawakilisha mawazo yangu, mapenzi na ndoto).

***Mstari 6.*** *Anaongoza kalamu* (Napenda kuchora na haya ni mapenzi yangu).

***Mstari 7.*** *Mwezi ukazama* (Wakati wa usiku ndipo ninapopata faraja, nyota hunipa matumaini na mwezi ndio naweza kuuamini katika matatizo yangu).

**Kuandaa shairi la kusifu au wimbo (maelekezo kwa mwanafunzi)**

Anza na jina lako.

Rejea kwenye kitu kinachoelezea wapi na namna ulivyozaliwa

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Ongea kitu chochote juu ya urithi wa familia yako;asili ya familia yako. Taja kitu, mnyama, kitu asilia ambacho ni cha maana au maalumu kwako.

Ongea kitu kukuhusu wewe: unapenda nini, unataka nini na ndoto zako.

Andaa shairi kati ya mistari mitano na minane. Shairi liwe fupi, kila neno libebe picha, (kila neno liwe na maana nyingi, likitueleza mambo mengi).

Chagua maneno yako kwa uangalifu. Tumia kifaa chako kuboresha hisia na maana ya shairi lako. Chagua lini na ni vipi utaitengeneza sauti. Fikiri kwa makini kuhusu namna utakavyotumia sauti yako kujieleza.

Unaweza kuona zaidi nyimbo za kusifu za mwanafunzi katika tovuti ifuatayo: http://web.cocc.edu/catagucci/ ambako yaliyopo hapo ya juu ndiko yalikonakiliwa.

## Nyenzo rejea 6: Kutengeneza muziki

**Taarifa za msingi/welewa wa somo wa mwalimu utangulizi**

**A. Kutengeneza na kupiga filimbi za Tshikona**

**Kutengeneza kundi la wapiga filimbi**

(kutoka Talking Drum, April 1999, Sandra Bonnett, p. 17–18)

Wapiga filimbi ni makundi maalumu ya muziki kwa sababu kila mtu anapiga nota moja tu-lakini, zinawekwa pamoja, mara nyingi katika njia za kutatanisha, zinatengeneza muziki wa kustaajabisha. Wavha Venda, Watswana na Wabapedi wanafahamika kwa makundi yao ya wapiga filimbi za mitete, ambazo zinasemekana kwenda sambamba na ngoma kama Venda Tshikona na Bapedi Dinaka. Filimbi zimetengenezwa kwa matete (sehemu za vijijini) au filimbi za chuma (sehemu za mijini au kwenye machimbo ya madini). Filimbi zinatofautiana kwa ukubwa kutoka

sentimeta 20 hadi mita moja kwa urefu, ikitoa nota kuanzia za juu hadi za chini.

Shughuli hii imeelemea kwenye muziki kiTshikona na filimbi iliyochezwa na Wavenda wanaoishi kaskazini kabisa mwa Afrika ya Kusini (Jimbo la Limpopo). Filimbi za kiTshikona ni ndefu zikiwa na urefu wa kutofautiana, kila moja ikitoa nota tofauti. Unaweza kutengeneza filimbi zako kwa kutuma mabomba ya plastiki kama vile yale ya kupitishia nyaya za umeme, vipande vya mabomba ya plastiki, mabomba ya umwagiliaji (kipenyo cha mm 12-15). Tengeneza filimbi za urefu uliotofautiana ili uwe na nota tofauti. Vile vile ungeweza kutumia chupa za ukubwa mbalimbali na kupuliza kwa juu ili kutoa sauti.

**Jinsi ya kupiga filimbi**

1. Weka sehemu ya wazi ya kifaa kwenye midomo ya chini.
2. Shikilia filimbi kati ya vidole vyako, kidole cha shahada na kidole gumba.
3. Weka vidole vilivyobaki kuzunguka eneo la katikati la kifaa.
4. Anza kupuliza taratibu juu ya shimo hadi hapo nota itakapotokea.
5. Jaribisha kwa kuziba sehemu ya chini ya filimbi kwa mkono wako.

**B. Kutengeneza muziki wa kidemokrasia**

Wagawe wanafunzi katika makundi ya watu kumi na jaribisha filimbi za mitete, ili waweze kusikilizana kwa umakini. Tengeneza nafasi katika mapigo yako ili wanafunzi waweze kujaza nafasi hizo. Halafu ongeza na mbinu za kucheza. Huna haja ya kucheza muda wote. Pokezaneni.

**Unganisha- kujaza nafasi**

Wazo la kuunganisha ni la msingi kwa muziki wa kiafrika. Unapojiunganisha na sauti unakuwa unajaza nafasi katika muziki (ukimya) kwa kutumia sauti. Kwa maneno mengine unasubiri hadi upate nafasi ya kutoa sauti yako. Huu ni ujuzi muhimu unaofundisha wajifunzaji kusikiliza kwa makini, achianeni na kuweni makini. Huu ni msingi wa kutengeneza muziki wa kikundi kama picha za sauti.

**C. Kutumia chupa kutengeneza filimbi za muziki wa makundi.**

Kama ulitengeneza chupa za muziki badala ya filimbi, zituni chupa zako ili kuwe na namba sawa ya chupa zilizokuwa zimewekwa kwenye sauti A, E, G and D (kuanzia ya juu hadi ya chini). Utahitaji kitunio au kinanda ili kukagua tuni zako na kurekebisha maji kwenye chupa yako.

Wagawe wanafunzi wako katika makundi mawili. Hapa kuna mpangilio wa muziki kwa kila kundi uliogawanywa katika mapigo 8. Jaribisha kwanza kwa kupiga makofi kwenye namba zilizokolezwa wino, wakati mtu mwingine akipiga ngoma ya besi kuhifadhi mapigo. Utunze huo mdundo wa ngoma katika hali yake ya taratibu. Halafu puliza kwenye chupa yako katika muda sahihi, ukitunza mapigo kwa kutumia ngoma (lazima ujue ni nota gain ngoma yako inasikika!)

**Kundi A**

Chupa zote za A katika kundi la ‘lahani’ zinapuliza kwenye namba 1 na 5;

chupa zote za G zinapuliza kwenye namba 2 na 6, n.k.

**Kundi A**

**Hesabu/Idadi ya nota**

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | **1** | 2 | 3 | 4 | **5** | 6 | 7 | 8 |
| G | 1 | **2** | 3 | 4 | 5 | **6** | 7 | 8 |
| E | 1 | 2 | **3** | 4 | 5 | 6 | **7** | 8 |
| D | 1 | 2 | 3 | **4** | 5 | 6 | 7 | **8** |

**Kundi B**

**Hesabu/Idadi ya nota**

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | 1 | 2 | **3** | **4** | 5 | 6 | **7** | **8** |
| E | **1** | 2 | 3 | 4 | **5** | 6 | 7 | 8 |
| D | 1 | **2** | 3 | 4 | 5 | **6** | 7 | 8 |

Weka makundi yote mawili pamoja, sikiliza kwa umakini kwenye ngoma ili ujue ni mdundo gani wa kupiga. Muziki utakaopatikana unatakiwa uwe wa kuvutia. Ukishafanyia mazoezi, tengeneza muziki wako, kwa kucheza nota hizo kwa mapigo tofauti.

*(Kazi ya Sandra Bonnett, 1997. In Talking Drum April 1999)*

**D. Nyenzo katika jamii na bendi**

**Kwa ajili ya mwalimu:**

Endelezeni mradi huu kwa kuunda kabendi, kwa kutumia vifaa vilivyotengenezwa na wanafunzi. Hakikisha kuwa kila kundi lina vifaa kadhaa. Jenga dhamira ya utambulisho wa kundi na aina ya nyimbo za kusifu ili kila kundi litengeneze shairi kwa kutumia vifaa, ikiwasilisha jambo kuwahusu wao wenyewe. Kutengeneza nyimbo za makundi kunahitaji muda kama mchakato wa kujifunza namna ya kutengeneza muziki kwa pamoja unavyojengeka. Shirikiana pamoja na mwalimu na shule yako rafiki. Andaa mchezo wa pamoja ambapo kila kundi linacheza nyimbo zake na kuonyesha vifaa walivyotengeneza.

Tafuta nini kinatokea kimuziki katika jamii yako. Kunaweza kuwa na wanamuziki wazuri ambao wangeweza kuja na kuimba kwa wanafunzi wako, na kushiriki nao katika shughuli za muziki na utamaduni. Tumia jamii kama nyenzo ya kujifunzia.

**Kwa ajili ya wanafunzi: Mawazo ya mradi wa utafiti**

Tafuta mwanamuziki anayeishi kaitka eneo lako na umhoji. Muulize:

Kifaa chako ni nini?

Ni aina gani ya muziki unaimba?

Muziki unamaanisha nini kwenye maisha yako? Wapi na vipi ulijifunza kuimba?

Tafiti aina mbalimbali za makundi ya muziki: kwaya, bendi, muziki wa pop/rock/kizazikipya/ ngoma za asili na aina nyingine ya makundi.

Tafuta:

Ni nini kinachofanya kila kwaya au bendi iwe ya kipekee? Wanacheza muziki gani?

Wanatumia vifaa gani?

Muziki wao umerekodiwa? Kama ndiyo walirekodi vipi?

Ni akina nani waliohusika katika kutoa wimbo au albamu iliyorekodiwa? Wanafanya nini?

Ni hatua gani muhimu za kuchukua ili kuunda kundi la muziki lenye mafanikio?

Mazoezi ya mwisho yanafanyaje kazi?Ni namna gani kikundi au kwaya inafanya mazoezi?Wapi?Kwa muda gani?

Ni namna gani bendi au kwaya inavyojiimarisha yenyewe na matamasha yao?

**Kutengeneza bendi yangu mwenyewe**

Kwa kutumia taarifa ambazo umekusanya unda kundi na baadhi ya rafiki zako na tumia vifaa vyako kutengeneza kibendi chako mwenyewe. Ipe bendi hiyo jina. Fikiri kuhusu aina ya muziki ambao ungependa kuucheza. Tengeneza sauti zako mwenyewe. Endelea kubuni vifaa. Endelea kusikiliza na kugundua sauti za kuvutia ambazo unaweza kutengeneza na ziweke pamoja ili utengeneze muziki wako mwenyewe.

Kuona jinsi wanafunzi wengine walivyounda vibendi vyao, nenda www.soundhouse.co.uk/mixedup/

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

# Sehemu ya 5: Sanaa ya kuhadithia hadithi

**Swali Lengwa muhimu:** Kwa jinsi gani unaweza kuwasaidia wanafunzi wazikubali/hadithi na kujijengea ujuzi wa kuhadithia hadithi?

**Maneno muhimu:** hadithi jamii, kuhadithia hadithi, kuandika, utamaduni kazi ya kikundi.

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- Umepanga na kusimamia kazi za madarasa ili kusimamia tathimini ya hadithi na kuhadithia;
- Umetumia mawasiliano ya ndani na rasilimali iliyojenga ufahamu wako juu ya utamaduni wa kuhadithia;
- Umebuni na kutumia mbinu/mkakati wa kuwasaidia wanafunzi kuandika hadithi zao.

## Utangulizi

Hadithi zimekuwa sehemu muhimu ya historia ya binadamu kwa karne ya sasa. Siku za nyuma, hadithi maranyingi zilitoa ujumbe muhimu. Waskilizaji wangecheka, kulia na wakati mwingine kuimba pamoja na mtoa hadithi.

Ni uwezo wa kubeba ujumbe unaozipa hadithi thamani kwako, kama mwalimu. Shughuli, uchunguzi kifani na nyenzo rejea katika sehemu hii zinalenga kukusaidia wewe kutumia utajiri huu wa kurithi ili uwajengee wanafunzi wako ujuzi wa sanaa ya kuandika, kuhadithia na kusimulia/ghani hadithi. Hii itawajengea hisia za kujitambua na kuwapa uelewa kuhusu urithi wao wa kitamaduni.

## Somo la 1

Hadithi inaweza kusemwa, kuandikwa, kusomwa na kusimuliwa. Inaweza kuwa hadithi ya kweli au ya kutunga. Mara nyingi hadithi zina ujumbe

ndani yake juu ya taratibu za jamii, namna ya kuishi maisha yetu na namna ya kuwajali wangine.

Wewe na wanafunzi wako yawezekana mmeshawahi kuhadithia au kusikia hadithi. Yawezekana pia mmeshaandika baadhi. Sehemu hii itakusaidia kuwajengea wanafunzi wako uelewa wa sanaa ya kuhadithia hadithi na kwamba kuhadithia hadithi kumejikita ndani ya utamaduni wa jamii yenu.

Unaweza kuwa na bahati kwa kumfahamu mtu ndani ya utamaduni wa jamii yenu. Unaweza kuwa na bahati kwa kumfahamu mtu ndani ya jamii yenu mwenye ujuzi wa kuhadithia na ukaweza kuja kuhadithia hadithi darasani kwako (angalia nyenzo rejea muhimu; **kutumia jamii/mazingira ya asili kama nyenzo rejea**). Au, katika **uchunguzi kifani 1** , unaweza kumtembelea wahadithiaji na kuwarekodi kwenye kanda ili uitumie darasani kwako. **Shughuli 1** inapendekeza njia za kuwaandaa wanafunzi kushirikishana hadithi wazipendazo.

## Uchunguzi kifani ya 1: Kutumia watu wa kawaida kujifunza umuhimu wa kiutamataduni wa hadithi

Bibi Biyela anafundisha katika Shule ya Msingi Furaha nchini Tanzania. Anajiandaa kwa mada yake unayofuata, ambayo ni 'Hadithi'. Anapitia vitabu na nyenzo rejea za tovuti juu ya uhadithiaji wa hadithi, uandishi na usomaji. Anajifunza kuwa kuhadithia hadithi kuna umuhimu wa ndani wa kiutamaduni, na anatafuta baadhi ya njia za kufikisha umuhimu huu kwa wanafunzi wake.

Amesikia habari za ajuza/kikongwe mmoja, Bibi Koku, anayeishi jirani ni maarufu kwa uhadidhiaji. Mchana mmoja, anaamua kumtembelea Bibi

Koku na akamuuliza kama atakuwa tayari kuhadithia hadithi wanafunzi wa mwalimu Biyela. wa darasa la nne. Kikongwe huyu anakubali lakini anasema 'jioni tu'. Anasisitiza kuwa watu wanaohadithia hadithi mchana wanakaribisha njaa katika jamii yao naye hayuko tayari kufanya hivyo.

Haraka, suala hili linakuwa jambo la kuvitia kwa Bibi Biyela-Ana uhakika litavuta usikivu wa wanafunzi wake na kuwapa uelewa zaidi wa utamaduni wa kuhadithia hadithi.

Kwa hiyo anapanga kuleta chombo cha kurekodi/kinasa sauti ili amrekodi Ma'Koku akihadithia hadithi, pamoja na kuongelea miiko ya kuhadithia mchana. Anajitahidi na kuhakikisha kuwa kikongwe huyu anaongelea suala hili namna ambayo wanafunzi wake wataelewa. Inavyoonekena, Ma'Koku ametatua tatizo lake kwa kuhadithia kinachowatokea watu wanaohadithia hadithi mchana.

Siku ya somo, Bi Biyela anakagua kinasa sauti chake na anahakikisha kuwa kote kote kiko sawa. Anatoa utangulizi wa somo, anawauliza wanafunzi kama wamewahi kusikia hadithi zilizotolewa na watu. Watoto wanahamasika -wanamsikiliza Ma'Koku akihadithia hadithi.

Baadaye, Bibi Biyela anaendesha majadiliano kuhusu kwa nini Ma'Koku hakuja kuwahadithia hadithi shuleni asubuhi ile. Anashangazwa na ukweli kwamba wanafunzi wengi wanaijua desturi ya kutohadithia mchana. Kufikia mwishoni wa kipindi, walikuwa wamejenga uelewea mkubwa wa mila na miiko inyohusiana/ambatana na suala hili.

## Shughuli ya 1: Kuchagua hadithi murua/inayopendwa

Kabla ya somo, muulize kila mwanafunzi kuamua hadithi fupi aipendayo ili ashirikishe wenzake darasani.

Liandae darasa katika makudi madogo madogo ya watu kati ya wane hadi sita. Mtake kila mwanafunzi kuwahadithia hadithi yake kwenye kundi lake. Kabla hawajaanza, sisitiza kuwa kila mmoja apate nafasi ya kuhadithia pia wasikilize hadithi za mwenzao.

Baada ya hapo, waambie kila kundi kuchagua hadithi moja kutoka kwenye makundi yao. Hizi wataziwasilisha darasani. Kama ukigundua kuwa kuna kundi lolote linapata shida ya kukubaliana, ingilia kati kuwasaidia wachague hadithi.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Wape nafasi vikundi wajiandae. Ikiwezekana, andaa, mavazi, zana, midoli, vifaa vya muziki, n.k. au waambie wanafunzi wavilete, ili kufanikisha hadithi zao na kuwasaidia kufikisha ujumbe/maana.

Kila kundi liwasilishe hadithi yao kwa darasa zima na kufafanua kwa nini wanaipenda.

Hatimaye, jadiliana na darasa lako sehemu muhimu za hadithi, mwanzo? Hadithi yenyewe, mtiririko wa visa, mandhari, wahusika na mwisho/tamati.

Ulishangazwa na hadithi ambazo wanafunzi wako walichangua? Ni vizuri kiasi gani wanafunzi wako walifanya kazi pamoja katika makundi madogo? Je, unahitaji kupanga makundi tofauti kazi ijayo?

## Somo la 2

Mila nyingi na imani zinaenezwa kupitia hadithi. Katika sehemu hii, tunashauri namna ya kujenga uelewa wa wanafunzi juu ya umuhimu wa hadithi katika urithisha/eneza mila hizi na kutoa ujumbe jinsi/namna watu wanavyopaswa kuishi.

Inavutia/sisimua kwa wanafunzi wasikiliza wataalamu wa hadithi akihadithia hadithi zao. **Katika uchunguzi kifani 2** , mwalimu anaandaa ziara kwenda kwa mwadithiaji. **Katika shughuli 2,** unatumia mbinu ya kuchangia mawazo kuchunguza ufahamu wa wanafunzi wako juu ya ngano/kisa cha asili na kugundua njia za kuziweka hadithi hizi pamoja (angalia **nyenzo rejea muhimu: Kutumia ramani kifani na kuchangia mawazo kugundua mawazo**).

## Uchunguzi kifani ya 2: Kuwapeleka wanafunzi kumtembele/ kuzuru msimuliaji hadithi

Bwana Bakari ni mwalimu wa masomo ya sayansi ya jamii na sanaa katika shule moja umasaini. Bwana Bakari alimtembelea kiongozi wake wa kijiji Mzee Sokoine, na kumuuliza iwapo awalete wanafunzi wa darasa la sita(6) nyumbani kwake. Pia alimuuliza kiongozi huyo kama atawaeleza ngano wanafunzi. Hili lilikubaliwa.

Siku moja kabla ya siku ya mapatano, ndugu Bakari aliliambia darasa kuwa atawapeleka nje ya shule kutembelea boma ya Mzee Sokoine ili wasikilize ngano za wamasai. Ili kuwaandaa wanafunzi wake, aliandaa mjadala mfupi juu ya uzoefu wao juu ya hadithi na nini wanafikiri watapata kesho yake na kuwatengenezea ramani ya kufikirika ya mawazo yao ubaoni.

Ngano/kisa alichosimulia mzee Sokoine kiko katika **Nyenzo rejea 1: sauti ya kiwavi**. Ngano hiyo ilikuwa na ujumbe muhimu na masomo ya kujifunza. Mwalimu Bakari, alivyosikiliza hadithi, alikuwa tayari anaandaa maswali atakayouliza darasani juu ya hadithi ili kutoa mafundisho haya. Kwa vile Mzee Sokoine alikuwa Mzee wa kuheshimiwa, aliweza kuwavutia watoto juu ya utajiri wa ukoo/jadi unaoambatishwa na hadithi za mila za kimasai ambazo zilitolewa kwa muda mrefu na maana zake ili kuziimarisha kutoka kizazi hadi kizazi nyingine. Ndugu Bakari aligundua kuwa alifanya maamuzi ya busara kwa kuwapeleka wanafunzi kwenye boma, badala ya kuwaeleza hadithi yeye mwenyewe.

## Shughuli ya 2: Kutengeneza Ngano za Kiasili

Kabla ya somo, kusanya masimulizi yaliyoandkiwa na ya mdomo ya hadithi za kimila kadri utakuvyoweza. (Angalia **Nyenzo rejea 2** : Hadithi na hekaya/ngano kutoka Afrika kwa ajili ya tovuti na soma **Nyenzo rejea muhimu: kutumia teknolojia mpya.**

Waambie

Mwanafunzi kujadiliana kuhusu ngano za asili kama ambavyo wanakumbuka kuzisikia.

Kisha, gawanya darasa lako katika makundi ya wanafunzi wanne wanne. Litake kila kundi kuchagua hadithi iliyoainishwa wakati wa kujadiliana na kuiandika kwa kirefu wakiweka wakiweka na michoro.

Toa maelekezo, kama

Jina la ngano?

Ngano hiyo inatoka jamii/ukoo gani? Ngano hiyo inatoa ujumbe gani?

Ni somo/mafundisho gani yanaweza kupatikana kwenye ngano?

Nani huhadithia hadithi?

Ni hadhira gani imelengwa na kwa nini hadhira hii imelengwa? Ni muda/wakati gani ngano husimuliwa? Kwa nini?

Ni muda gani kwa siku ngano husimuliwa? Kwa nini?

Hadithi zilizotolewa zinaweza kutenenezwa na kutumika kama vijitabu vya rejea shuleni. Inawezekana kuzichapisha na kutumika katika jamii au zaidi ya hapo.

## Somo la 3

Kuwa na uelewa mzuri wa ngano za asili ni msingi mzuri kwa wanafunzi wako kubuni hadithi zao. Kusikiliza hadithi zilizohadithiwa kwa kuigizwa na kutumia maneno zinawafanya kujiamini na kuwa tayari kushiriki katika kuandika na kuzalisha/kutoa ngano zilizobuniwa vyema.

Lengo la sehemu hii ni kutumia nyenzo rejea za kawaida ili kuwajengea wanafunzi wako ujuzi wa kuandika hadithi na mashairi yao. Utaweza pia kujenga ujuzi wa kupanga shughuli za ujifunzaji unaowashirikisha wanafunzi.

Katika **Uchunguzi kifani 3** mwalimu anatumia kipindi cha radio kuhamasisha wanafunzi kuhusu hadithi. **Shughuli muhimu** picha zinatumika kama kichocheo. Kwa watoto wadogo zaidi wanaweza kuchora picha kama hadithi zao. Ni muhimu kila mwanafunzi kuweza kutoa hadithi bila kuhangaika na kuandika maneno kwa usahihi au kwa mwandiko mzuri.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kujifunza kutoka kwa mtaalam wa kuhadithia hadithi

Huku akisikiliza radio, Bi Sala, Mwalimu wa mafunzo ya jamii, alisikia kuwa Ijumaa inayofuata kutakuwa na programu/kipindi ambacho msimuliaji hadithi maarufu na mwandishi atahojiwa.

Bahati nzuri, programm/kipindi kilipangwa kwa muda mwafaka, wakati wa kawaida wa shule. Hivyo Bi Sala alikuja shuleni na radio yake. Amejiandaa pia kurekodi kipindi hicho.

Kabla ya kipindi hicho kuanza, alijadiliana na wanafunzi wake walichokijua juu ya mwandishi, na walitegemea nini kutokana na maongezi atakayotoa wakati atakapokuwa anahojiwa.

Wakati wa kipindi, mwandishi alieleza juu ya muundo wa hadithi, dhamira/wazo kuu, wahusika na mandhari. Alitoa ushauri juu ya mchakato wa unadishi. Pia alizungumzia juu ya kilichomvuta na mawazo yake aliyapata wapi. Baada ya kipindi, Bi Sala aliuliza maswali yafuatayo ili kuchochea mjadala kwa wanafunzi wake:

Unaweza kujifunza nini kutoka kwa mwandishi huyu yanayoweza kukufanya uwe mwandishi mzuri ?

Kipi kinamkuchochea ? Je kuna mambo katika maisha au jamii yako unayotoka kuandikia ?

Uandishi mzuri/maandishi mazuri yana muundo na habari zipi ? Aliuliza swali la mwisho mwishoni mwa kipindi kwa sababu alitaka

kichochewe na mambo makubwa.

Mwishoni mwa somo, alisema kuwa kwenye uandishi wa ubunifu utakaofuata, utawataka wanafunzi kujaribu mbinu zilizopendekezwa na mhadithiaji. Ataangalia ushahidi kama wamezingatia masuala haya na kwa uangalifu atatoa mrejesho.

## Shughuli muhimu: Kuandika na kusimulia hadithi

Wape wanafunzi kichokoo ili kupata mawazo juu ya maisha, Jamii au Jamii pana. Angalia Nyenzo rejea 3: Picha za hadithi kwa ajili ya taswira zinazofanyakazi vizuri, lakini unaweza kuchagua kitu kingine cha kufanana/aina hiyo.

Tumia Nyenzo rejea 4: kutumia picha kama kuchokoo cha kuandika hadithi ili ikuongoze, jadili picha ambayo darasa limechagua.

Waambie wanafunzi waandike hadithi zao wenyewe. Wahamisishe kuongeze mawazo yao na matukio/ wanapoandika. Kwa mfano: Nini kilitokea kabla kilichosababisha picha itokee na nini kitafuata?

Siku inayofuata, wanafunzi walisomeane hadithi zao katika makundi madogo madogo na kila kundi linamchagua mtu mmoja wa kusomea darasa zima. Wasisitize umuhimu wa kutumia sauti na 'vichocheo' kama inawezekana ili viwasaidie.

Unaweza kuziweka hadithi zote kwenye vitabu vya darasa

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

# Nyenzo-rejea ya 1: Sauti ya kiwavi

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**

Hapo zamani za kale, kiwavi kilitambaa hadi ndani ya nyumba ya sungura, wakati sungura akiwa hayupo, na kukaa kwa raha zake. Sungura aliporudi, aligundua alama mpya ardhini pangoni mwake. Aliita

‘Nani yuko ndani ya nyumba yangu? Kiwavi akalipuka kwa sauti kubwa, “Ni mimi ! Ndiyo, ni mimi ninaye sagasaga kifaru hadi ardhini na kukanyaga tembo kwenye vumbi”.

Sungura akanyong’onyea na kulia akisema, ‘kiumbe mdogo kama mimi atamfanya nini kiumbe anayesagasaga kifaru na kukanyaga kanyaga tembo ?’

Punde alikutana na mbweha na kumuuliza/kumwomba aongee na kiumbe huyo wa kutisha aliyejitwalia mji wake (sungura) ili amshawishi kuoondoka. Mbeha alikubali, na walipolifikia eneo alibweka kwa nguvu na kusema ‘Nani yuko ndani ya nyumba ya rafiki yangu Sungura ?’

Kiwavi akajibu kwa sauti iliyotetemesha nchi, ‘Ni mimi ! Ndiyo, mimi ninaye sagasaga kifaru hadi ardhini na kukanyagakanyaga tembo mavumbini !’ Alivyosikia haya, mbweha akafikiri ‘kwa vyovyote siwezi kufanya chochote juu ya kuimbe hicho,’ akaondoka mbiombio.

Sungura akamleta chui, na kumwomba amsaidie. Chui akamhakikishia kuwa hakutakuwa na tatizo. Alipofika kwenye tukio, chui alikwaruza kwa kucha zake na kusema, ‘Nani yuko ndani ya nyumba ya rafiki yangu sungura ?’ Kiwavi alimjibu katika hali aliyowajibu wawili waliopita. Chui alihadharishwa na kufikiri, ‘kama kusagasaga kifaru na kukanyagakanyaga tembo, sitaki hata kufikiri atakachonifanya !’

Kilichofuata sungura akamwona kifaru. ‘Bila shaka, ni mnyama mwenye kutisha,’ kifaru alijigamba. Kifaru alitembea kwenda kwenye pango la sungura, alipokoroma na kuparura ardhi kwa miguuyake mizito.

Lakini kifaru alipouliza aliyeko ndani na kusikia sauti ya kutisha ya kiwavi, akafikiri ‘Nini, anasema anaweza kunisagasaga ardhini ?’ Na kifaru akatoweka, akitokomea msituni.

Akiwa amekata tamaa, Sungura akamjaribu tembo kwa kumwomba masaada wake. Lakini kama wengine, aliposikia maneno ya kiwavi tembo akajua kuwa hakuwa anatamani kukanyagwakanyagwa kama mavumbi, akaondoka zake.

Kwa kusikitishwa na hoja hii, Sungura alimwomba chura aliyekuwa anapita kama anaweza kumsaidia na kumfanya kiumbe aliyowatisha wanyama wote aondoke nyumbani mwake. Chura alikwenda kwenye mlango wa pango na kuuliza aliyekuwa ndani. Alipokea jibu lilelile walilopewa wengine. Kisha chura alisogea karibu na kupiga kelele, ‘Mimi niliye na nguvu kuliko wote, nimekuja hatimaye. Mimi husagasaga wale wasagao vifaru ! Mimi huwakanyagakanyaga tembo !’

Kiwavi aliposikia hayo kule ndani alitetemeka. Alihisi kivuli cha chura kikisogea na kufikiri, ‘Hata hivyo mimi ni kiwavi tu ! Na kiwavi akajificha kwenye tundu lililokuwa kwenye pembe ili asionekane. Wanyama waliokusanyika karibu na nyumba ya sungura walimkamata na kumtoa nje. ‘Nani, wewe ?’ Wote walipiga kelele kwa kutoamini.

‘Siwezi kufikiri kukaa ndani ya pango hilo !’ Kiwavi aliyasema pua akawa amebinua juu, ‘mwangwi wake anatisha kwa kiumbe mungwana kama mimi !’ Alivyo ondoka zake, wanyama wengine wakacheka kwa matatizo/usumbufu aliowasababishia.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

# Nyenzo-rejea ya 2: Hadithi na hekaya kutoka Afrika

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**

Tovuti hapa chini imekupa zaidi ya hadithi 50 na ngano katoka Afrika http://www.gateway-africa.com/stories/

Kama hii hapa chini

Radi na mwale wa radi

Hapo zamani za kale radi na mwale waliishi hapa duniani pamoja na watu. Radi alikuwa kondoo jike na mwale ulikuwa 53 asu kondoo dume. Hakuna mnyama aliyekuwa maarufu kwa watu, kwani pale mtu alipomkosea mwale, angepaa kwa ghadhabu na kuanza kuunguza chochote alichokutana nacho. Hii ilihusisha vibanda, vihenge na hata miti

mikubwa. Wakati mwingine angeharibu mazao shambani kwa moto wake na muda mwingi aliua watu waliopita kwenye anga zake. Radi alipojua kuwa wanae alikuwa na tabia ya aina hii, aliinua sauti na kumpigia kelele na zilikuwa kilele kweli kweli. Kiuhalisia, majirani walikuwa wamehuzunishwa, kwanza kwa hasara, iliyosababishwa na mwale na kwa sauti zisizovumilika zilizotoka kwa mama yake zilizokuwa zinafuatia upasukaji wake. Wanakijiji walilalamika kwa mfalme matukio mengi hadi pale alipowaagiza wote wawili kuishi kwenye mpaka wa kijiji na kuwaambia kuwa wasjie wakachanganyika tena na watu. Hata hivyo, hii haikusaidia kwani mwale aliendelea kuwaona wanakijiji walipokuwa wakitembea kijijini/Mitaani hivyo kupata urahisi wa kuendelea kukwaruzana/kuzozana nao.

Mfalme akawatumia ujumbe tena aliwaambia ‘Nimewapa fursa nyingi kuishi maisha mazuri, lakini naona kuwa haijafaa chochote. Kuanzia sasa na kuendelea, mwende mbali na kijiji chetu, mkaishi kwenye pori. Hatutaki kuona sura zenu hapa tena.’ Radi na mwale iliwabidi watii mfalme na kukubali kufuata hukumu yake. Hivyo waliondoka kijijini, wakiwa na hasira na wakazi wake. Bado kulikuwa na matatizo makubwa kwa hifadhi za wanakijiji, kwani mwale alikasirika kwa kufukuzwa kiasi

kwamba aliwasha moto kwenye pori lote, na kwa vile ilikuwa wakati wa kiangazi, hali hii ilikuwa mbaya zaidi.

Moto aliambaa kwenye mashamba madogo ya watu na wakati mwingine kwenye nyumba zao, sasa walikuwa kwenye mashaka tena. Mara nyingi walisikia sauti ya kondoo jike (mama wa kondoo dume) akimwita mwanae akimuonya aache lakini kwa vile aliyafanya baada ya tukio, haikuleta tofuati yoyote. Mfalme aliwaita washauri wake ili wamshauri. Baada ya mdahalo mkubwa, wakapata mpango. Kwa nini tusiwafukuze radi na mwale jumla watoke duniani, na kuwasukumia kuishi angani? Hivyo mfalme akaafiki. Radi na mwale walitupwa/sukumwa angani ambapo

watu walitumainia kuwa hawasabisha madhara tena.
Lakini mambo hayakwenda kama walivyotarajia; hata hivyo mwale bado anaonyesha hasira yake mara kwa mara na hawezi kuacha kutupa moto duniani anapokasirika. Unaweza kumsikia mama yake akimkemea kwa sauti yake ya kutisha.

*Imepatikana katika chanzo: Gateway Africa, Website*

## Nyenzo-rejea ya 3: Picha za hadithi

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi.**





*Chanzo asilia: Arthus-Bertrand, Y. 2004. 365 Jours. Editions de la Martiniēre : Paris*

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

# Nyenzo rejea 4 : Kutumia picha kama kichokoo cha kuandika hadithi

**Nyenzo ya Mwalimu kwa kupanga au kubadili nyenzo ili zitumike na wanafunzi**

Picha zinaweza kuwa kichokoo kizuri cha uandishi wenye ubunifu kabla wanafunzi hawajaandika hadithi au ushairi wao. Unaweza kuijadili picha iliyochaguliwa na darasa zima au uwe na makala nyingi 55 asura hiyo hiyo au sura tofauti ili wanafunzi wajadiliane katika makundi yao. Kama una darasa kubwa unahitaji kuwa na sura nyingi au ufanye kazi na nusu darasa kwa wakati mmoja wakati wengine wakifanya kazi nyingine.

Maswali yafuatayo yanaweza kutumika pamoja na picha yoyote ili kuchokoa mawazo na ubunifu. Unaweza kuandika maswali ubaoni na kuyajadili na darasa zima au lipe kila kundi maswali yake na waambie watoe majibu ndani ya muda mfupi/dakika chache. Baadhi ya maswali hayatafaa kwa kila picha. Itabidi uchague yale yanazoendena na malengo au waambie wanafunzi kuibua maswali juu ya picha.

1. Unafikiri kinatokea nini kwenye picha hii?
2. Unafikiri inaitwaje?
3. Nini kinakuvutia kwenye picha hii? Kwa nini?
4. Unapenda nini kwenye picha hii?
5. Hujapendezwa na nini kwenye picha hii?
6. Kuna hadithi gani kwenye picha hii?
7. Nini/kipi kilisababisha picha hii ipakwe rangi/picha hii ichukuliwe?
8. Unafikiri nini kitatokea baadaye?

Nakili majibu ya wanafunzi ubaoni ili wayatumie ukiwapa kazi ya kuandika hadithi; lakini wahamasishe kuwa wabunifu na kutumia mawazo yao.

Wahamasishe kufikiri kilichotokea hapo kabla ya picha na ikiwezekana waanzie hadithi yao pale.

Kurudi Mafunzo Ya Jamii Na Sanaa ukurasa

TESSA

Teacher Education in Sub-Saharan Africa

www.tessafrica.net